MFULULIZO WA VITABU VYA KUMBUKUMBU ZA ANSARI

# YALIYOMO


MATOLEO YA KUMBUKUMBU YA ANSARI ........ 11

**Dibaji kwa toleo la pili** ........ 17

**Dibaji kwa toleo la pili** ........ 19

**Utangulizi** ........ 20

Taifa la Khilafah la Kiislamu na mfumo bandia mbadala unaotumika ........ 20

Kuanzia Utawala wa Kikristo wa Ulaya hadi Kufikia kwenye utamaduni wa Kimagharibi wa Dajjal ........ 29

Kuanzia kwa Ufalme wa Ottomani uliofungamana na magharibi hadi Taifa la Saudia lililofungamana na magharibi ........ 31

Kuanzia kwenye kuvunjwa kwa Khilafah hadi kuvunjwa kwa Hajj ........ 34

**Sura ya kwanza** ........ 36

Diplomasia ya Kiingereza na mashambulizi dhidi ya Khilafah ........ 36

**Sura ya Pili** ........ 49

Kuanguka kwa Khilafah ya Ottomani na Kuinuka kwa Serikali ya Kitaifa ya Wahhabi wa Saudia inayojengwa kwa Msimamo wa Sera za Kidunia ........ 49

Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia na Kusitishwa kwa Khilafah ya wa-Ottomani ........ 49

Wazalendo (Nationalists) wa Kituruki na Khilafah ........ 52

Majibu na msimamo wa Chuo Kikuu cha Al-Azhar kuhusu kusitishwa kwa Khilafah ya Ottomani ........ 54

**Sura ya Tatu** ........ 58

Kongamano la Khilafah, Kairo *(Mwezi wa Tano, 1926)* ........ 58

Ajenda ........ 59

Wajumbe ........ 59

Vikao vya Kongamano ........ 60

Kamati ya Pili ........ 61

Eskatolojia ya Kiislamu na kuvunjwa kwa Taifa la Khilafah ........ 64

........ 74

Kamati ya Tatu ........ 75

Maazimio ya Kongamano ........ 78

**Sura ya Nne** ....................................................................................................................80
Ulaghai wa Utawala wa Wahhabi wa Saudia ukijifanya ni Mbadala wa Utawala na Mamlaka ya Khilafah ya Kiislamu ..................................................................................................80
Kongamano la Kiislamu la Kimataifa la Makkah Mwezi wa Sita - Saba, mwaka 1926 .....80
Wajumbe wa Kongamano ....................................................................................................86
Mfalme na Kongamano.........................................................................................................87
**Sura ya Tano** ....................................................................................................................94
Ulimwengu wa zamani wa Kiislamu – Jaribio la mwisho la ufufuzi ..................................94
Kongamano Kuu la Kiislamu la Jerusalem Mwezi wa Kumi na Mbili mwaka 1931..........94
Tarehe na Jukwaa..................................................................................................................96
Wajumbe ...............................................................................................................................97
Majukumu ya Kongamano....................................................................................................98
Yaliyojizi baada ya Kongamano.........................................................................................103
**Hitimisho**..........................................................................................................................106
Kiambatanisho na.1 ............................................................................................................109
Kumbukumbu za Talaat Pasha (1874 -1921) .....................................................................109
Kiambatanisho na. 2 ...........................................................................................................114
Fatwa ya wa-Ottomani ya Jihad .........................................................................................114
Fatwa ..................................................................................................................................114
Kiambatanisho na. 3 ...........................................................................................................116
Tamko la Sharif Hussein bin Ali kwa Dunia ya Waislamu.................................................116
Faharisi ...............................................................................................................................121

# KHALIFA - HEJAZ NA TAIFA LA WAHHABI WA SAUDIA

**Mwandishi: Imran N. Hosein**

**Tafsiri: Abdul H. Akida**

## MSIKITI WA DARUL QUR'AN, LONG ISLAND, NEW YORK

Haki za uchapishaji© Imran N. Hosein 2002
Barua: inhosein@hotmail.com
Tovuti: www.imranhosein.org

Kimechapishwa kwa mara ya kwanza mwaka 1996
Masjid Darul Qur'an,
1514 East Third Avenue,
Bayshore, NY 11760
USA

Kimechapishwa kwa mara ya pili mwaka 2013
Masjid Jami'ah
Mtaa wa Mucurapo
San Fernando
Trinidad na Tobago

Msanii wa jalada la kitabu hiki ni ‘Abdullah Abu Muhammad ‘Abdurrahmani wa Skopje, Macedonia, linaonyesha mipaka ya himaya ya Ufalme wa Ottomani katika kipindi ambacho Ufalme huo wa Konstantinopoli ulipovunjwa mnamo mwaka 1924. Nafasi ya Khalifa wa Ottomani ilichukuliwa na Khalifa wa Kiarabu wa Makka, siku chache zilizofuata, na Khalifa huyo wa Kiarabu ndiye aliyeteketezwa na Wahhabi wa Saudia ambao walikuwa washirika wa Wazayonisti wa Kiyahudi na Kikristo wa *Taifa Tawala* la Uingereza. Na tangu kipindi hicho, haujaweza kurudishwa tena. Hata hivyo, elimu ya eskatolojia ya Kiislamu inatupatia ushahidi wa uhakika, kuwa Khalifa wa Kiislamu (*ikim. Taifa la Kikhalifa*) litarudishwa upya katika kipindi cha kuibuka kwa *Imam al-Mahdi* (*rehma na amani juu yake*)

Kimechapishwa Malaysia

Toleo hili ni kwa heshima ya

ndugu zangu wapendwa katika Uislamu

*Abid Siddiqui*

(wa kituo cha Kiislamu cha New York)

na pia

*Munir*

(wa Bangladeshi)

ambao wote wawili wamenipa msaada na mapenzi makubwa kupita kiasi katika jitihada zangu za kinyenyekevu katika kufanya kazi hii.

# *Pembe ya Shetani*

"O Allah, zijaalie baraka zako juu ya Sham yetu."

"O Allah, zijaalie baraka zako juu ya Yemeni yetu."

Maswahaba wakasema, "Ewe Mjumbe wa Allah, na Najd yetu?"

Nafikiri mara ya tatu Mtume (*rehma na amani juu yake*), akasema,

"Kule (Najd) patatokea matetemeko ya ardhi, matata na majaribu,

nako patajitokeza Pembe ya Shetani."

(Sahih Bukhari)

Wahhabi wa Saudia, ambao wana asili ya Najd, wanatimiza ubashiri huu mbaya na wa kuogofya.

# MATOLEO YA KUMBUKUMBU YA ANSARI

Vitabu katika Matoleo ya kumbukumbu ya Ansari vinachapishwa kumuenzi Mkufunzi mashuhuri wa Kiislamu, mwanafalsafa na *Sekhe wa Kisufi*, *Maulana* Dk. Muhammad Fadlur Rahman Ansari (1914-1974). Vitabu chini ya mpango huu vimeanza kuchapishwa mwaka 1977 katika kuadhimisha miaka 25 baada ya kifo chake.

*Maulana* Ansari alikuwa ni Mkufunzi wa Kiislamu, mwalimu na mchungaji wa kiroho ambaye alitumia muda wote wa maisha yake katika kupigania Uislamu katika dunia ambayo imemkifu Mwenyezi Mungu. Jitihada zake katika kujaribu kutimiza lengo hili takatifu lilimlazimu kufanya safari kadhaa kuzunguka sehemu mbalimbali za dunia huku akitoa hotuba na masomo ya dini ya Kiislamu katika miaka ya 1950 hadi 1970. Alikuwa akiondoka kutoka kwenye makazi yake mapya mjini Karachi (baada ya kuhamia hapo kutoka India mnamo mwaka 1947 baada ya kuundwa kwa nchi ya Pakistani) na kuelekea Magharibi, na kisha kurejea nyumbani kwake miezi kadhaa baadaye akitokea Mashariki.

Wito na kujitolea kwake kwenye maisha kulikuwa wazi na wingi wa utakatifu. Aligundua kuwa kuurejesha Uislamu kama Utawala (Nchi), na kama mfumo wa kijamii, kiuchumi na kisiasa, hakuwezekani bila ya kurejesha imani binafsi ya kila mtu. Wakati huo huo, imani hiyo hiyo binafsi ya kila mtu ndiyo imekuwa lengo la mashambulizi makali yanayotumia nyenzo za kisasa, udanganyifu na ya hatari yasiyokuwa na kikomo, kuliko wakati wowote kabla yake katika historia ya binaadamu. Mashambulizi hayo yalianzishwa na mataifa yaliyomkifu Mwenyezi Mungu duniani, mwanzo wake kuanzia Visiwa vya Uingereza, baadaye kufuatiwa na Marekani na mwishowe na Nchi ya Israeli. Lakini, kwa wakati wote huo, mashambulizi hayo yalikuwa yanaendelea kuongozwa na Wazungu ambao wamejivalisha nguo za Wayahudi.

Hususan mapambano haya ndiyo ambayo *Maulana* alikuwa akipigana nayo katika maisha yake yote huku akizunguka dunia nzima – mapambano ya kufufua imani ya Mwenyezi Mungu, Allah, Mtukufu. Alitumia rasilimali kubwa sana aliyojaaliwa kuwa nayo, nayo ni akili timamu ikiambatana na elimu ya kina kikubwa kupigana kielimu kwa niaba ya *Uislamu*. Na alitumia mvuto wa tabia unaotokana na nguvu za kiroho kuigusa mioyo ya wale wote aloweza kukutana nao. Kutokana na kazi na jitihada zake katika kupigania Ukweli, Waislamu wengi waliokuwa Mashariki na Magharibi waliweza kurudisha na kuongeza nguvu juu ya imani zao binafsi katika *Uislamu.* Maelfu wakawa wanafunzi na wafuasi wake kiroho, na wengine wengi wakaingia kwenye Uislamu kufuatia mafundisho na hubira zake.

Maulana alikuwa amehitimu kutoka Chuo Kikuu cha Aligam, India ambapo alisomea Falsafa na Dini. Alipata mafunzo yake ya Falsafa ya Kiislamu na Elimu ya kiroho kutoka kwa Dk. Muhammad Iqbal. Iqbal ndiye mwandishi wa kitabu mashuhuri kuliko vyote katika karne hizi za mwisho katika Uislamu: "*Ujenzi (upya) wa Mawazo ya Kidini katika Uislamu*." Mchango mkubwa na mzito wa *Maulana* Ansari katika Uislamu, "*Misingi na Mfumo wa Jamii ya Kiislamu*", wenyewe ni majibu ya wito wa Dk. Iqbal katika "*Ujenzi (upya) wa Mawazo ya Kidini*."

Alipata mafunzo ya kiroho kutoka kwa *Maulana* Abdul Aleem Siddiqui, msomi wa Kiislamu, *Shekhe wa Kisufi*, na mmishenari mtembezi wa Kiislamu. Na muhimu kuliko yote, alipata mafunzo ya Kisufi ya Epistomolojia kutoka kwa wote wawili, yaani Dk. Iqbal na *Maulana* Siddiqui na akafikisha mafunzo hayo kwa wanafunzi wake. Epistemolojia ya *Kisufi* inatambua kuwa wakati mtu anapokea na kuukubali Ukweli (anapoukubali *Uislamu*) na akaishi kwa usafi wa roho na ukamilifu wa ibada kwa Mwenyezi Mungu, mwishowe huingia moyoni (*Uislamu* unakua na kuwa *Imani*). Katika Hadithi al-Qudsi inasimulia kuwa Mwenyezi Mungu, Allah amesema:

"*Mbingu zangu na Ardhi yangu ni vidogo sana kuweza Kunitosheleza Mimi, lakini moyo wa mtumishi Wangu muaminifu unaweza kunitosheleza Mimi*." *Hadithi* hii kwa wazi kabisa inaelezea matokeo ya kuingia kwa Ukweli kwenye moyo.

Wakati Ukweli unaingia kwenye moyo, hapo nuru ya Mwenyezi Mungu huingia moyoni (*nurullah*), nuru ambayo inamwezesha muumini na kumpa nguvu za kuangalia na kuona kwa jicho la ndani la hisia za kiroho na kuweza kupenya magamba ya 'nje' na hivyo kuona ukweli halisi wa ndani wa kila jambo. Katika awamu hii ya kukua kwa Ukweli katika moyo, muumini sasa anakuwa anaona kwa kutumia macho mawili – jicho la 'nje' na jicho la 'ndani' (*Dajjal*, Mtume wa Uongo, anaona kwa kutumia jicho moja – jicho la 'nje'). Muumini ambaye anafuata '*Jihad Fillah'* (mapambano kwa ajili ya Mwenyezi Mungu) anabarikiwa kwa kukua kwa Imani kufikia hatua ya *Ihsan*. Hii pia inajulikana kwa jina kama *Tasawwuf*. Kwa kupitia hiyo nuru ya ndani, ndipo moyo wa muumini wa uhakika unapambanua kwa yakini, unazitambua na kuzielewa Alama za Mwenyezi Mungu (*Ayatullah*), na ndiyo njia pekee ya kuweza kuisoma vizuri na kuielewa vyema dunia ya leo. Wale ambao wanaweza kuutambua ukweli halisi wa dunia ya leo wanajua kwamba tunaishi kwenye zama za majaribu (*Fitan*), ikiwa ni Zama za Mwisho kabla ya *Qiyamah* (mwisho wa dunia).

*Maulana* ansari alijitolea miaka yake kumi ya mwisho ya maisha yake (1964-1974) katika kuanzisha Taasisi ya Aleemiyah ya Masomo ya *Kiislamu* katika mji wa Karachi ambapo alifanya juhudi za kufundisha kizazi kipya cha wasomi wa *Kiislamu* – wasomi ambao wangeweza kwanza kuielewa dunia ya kisasa kiroho na kielimu kwa kutumia *Qur'ani* na *Hadithi*, na kisha kuweza kutoa majibu muafaka kwa changamoto hizo nzito na kali. Kutokana na jitihada zake, wamefuzu wasomi kama vile Dk. Waffie Muhammad, Dk. Abul Fadl Muhsin Ibrahim, Siddiq Ahmad Nasir, Ali Mustafa, Muhammad Ali Khan, Basheer Ahmad Keeno, Raouf Zaman, Muhammad Saffie, Imran N. Hosein na wengine wengi waliofuzu kutoka katika Taasisi ya Masomo ya Kiislamu ya Aleemiyah, Karachi, Pakistani.

Wale ambao walipokea nafasi ya Maulana Ansari kuhusiana na mwelekeo na uongozi wa Chuo cha Kiislamu cha Aleemiya walikuwa ni watu ambao, hadi leo hii, wamekosa elimu ya kitaalamu ya Kiislamu na, matokeo yake, jaribio la kuunda chombo cha elimu ya juu cha Kiislamu chenye uwezo wa kutayarisha wasomi wa Kiislamu wenye uwezo wa kupambana na changamoto za dunia ya kisasa, wameshindwa kuleta mafanikio hayo baada ya kifo chake.

Toleo la Kumbukumbu ya Ansari linajumuisha vitabu vinane vifuatavyo, vyote vikiwa vimeandikwa na mmoja kati ya wanafunzi wake waliotajwa hapo juu:

- *Jerusalem katika Qur'ani*
  *Mtazamo wa Qur'ani kuhusu hatma ya Jerusalem;*

- *Sura al-Kahf*
  *Tafsiri na maoni ya kipindi kipya cha kisasa*
- *Surah al-Kahf na Zama za Kisasa*
- *Dini ya Abrahamu na Nchi ya Israeli – Mtazamo wa Qur'ani*
- *Umuhimu wa kuzuia Riba katika Uislamu*
- *Kuzuia Riba katika Qur'ani na Sunnah*
- *Ndoto katika Uislamu – Ufunguo kwenye: Ukweli na Moyo*
- *Khalifa – Hejaz na Nchi ya Wahhabi wa Saudia*
- *Umuhimu wa Mkakati wa Mfungo wa Ramadhani na Isra na Miraj*
- *Umma Mmoja Amiri Mmoja – Mpangilio wa Jumuiya ya Kiislamu katika zama za Majaribu*
- Mtazamo wa Kiislamu juu ya Ya'juj na Ma'juj katika Dunia ya Kisasa
- Dinari ya Dhahabu na Dirham ya Fedha
- Madina kurudi katikati ya Jukwaa katika Akhir al-Zaman
- Iqbal na Wakati wa Ukweli
- Maelezo juu ya Ajenda za Kiajabu za Kibeberu za Israeli
- Kufunga na Nguvu zitokana nako

Toleo hilo, ambalo linaonyesha japo kwa uchache, 'matunda' ya 'mti' ambao ulipandwa na *Maulana*, vimejikita kwa nguvu zote katika kuuelewa 'ukweli' wa dunia ya leo, kuielezea kinaga ubaga, na kujibu changamoto zake ipasavyo. Jitihada hizo, bila ya shaka, siku zote ziko wazi kufanyiwa mapitio na tathmini za kifalsafa za kidini na kielimu.

Vitabu kadhaa vipya muda si mrefu uliopita vilijumuishwa kwenye Toleo. Vitatu kati ya hivyo, kuhusu *Surah al-Kahf*, vinawakilisha pendekezo la vitabu vine vinavyohusiana na *Surah* hiyo. Kitabu kuhusu *Ya'juj na Ma'juj* ni cha tatu katika Toleo wakati pendekezo la kitabu kuhusu *Mtazamo wa Kiislamu juu ya Dajjal, Mtume wa Uongo au Anti-Christ* kitakuwa cha nne na cha mwisho.

Mwenyezi Mungu, Mtukufu, amewabariki waumini kwa kuwapa chombo ambacho kwacho wanaweza kupokea uthibitisho kuwa wamebarikiwa na kupewa huo uwezo wa elimu na maarifa ya 'ndani' (elimu na maarifa ambayo moyo inaona). Chombo hicho ni 'ndoto nzuri, za kweli na maono', vitu ambavyo vinajumuisha sehemu ya mwisho ya Utume, *nabuwah*, ambayo bado imebaki duniani baada ya kifo cha Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*). Toleo la Kumbukumbu ya Ansari, hivyo inajumuisha sehemu ndogo ya kazi ya awali katika fani iliyosahaulika, ikimaanisha, "*Ndoto katika Uislamu.*"

Ujuzi na maarifa yanayoashiria (kupitia jicho la 'ndani') pia ndiyo chombo muhimu katika kuweza kupenya na kuona kwenye somo lenye mkakati mkubwa wa kisasa kama vile, "*Kukatazwa*

*kwa Riba kwenye Qur'ani na Sunna*." Na "*Dini ya Abrahamu na Nchi ya Israeli – Mtazamo wa Qur'ani",* hivyo masomo hayo yamefanyiwa kazi katika toleo hili. Kwa hakika, ni kweli kusema kuwa, 'kigezo pekee kinachoweza kuchanganua' kuwepo au kutokuwapo kwa nguvu za kiroho katika hizi Zama za Mwisho kinapatikana kenye: i) uwezo wa kuwa na muono unaopenya, ukaelewa na ukatoa majibu ya kukabiliana ipasavyo dhidi ya changamoto nzito za *Riba* katika uchumi wa kisasa wa kidunia (usiokuwa wa Mwenyezi Mungu) na *Shirk* za kisiasa za Nchi zenye mfumo wa kisasa wa kidunia (usiokuwa wa Mwenyezi Mungu), na ii) uwezo wa kuwa na muono unaopenya, ukaelewa na ukatoa majibu ya kukabiliana ipasavyo dhidi ya tukio la ajabu na la kipekee katika siasa za kisasa za kimataifa, tukio la kurejea kwa Wayahudi kwenye Ardhi Takatifu na kuanzishwa kwa Taifa la Israeli. Wasomi wa *Kiislamu* wenye nuru za kiroho katika zama hizi lazima wajikite kwenye jitihada dhidi ya *Rib*a na *Shirk*

Kitu cha kustaajabisha kuliko vyote, chenye fumbo la hali ya juu na kinachokosa maelezo kuliko matukio mengine yaliyowahi kutokea kuanzia mwanzo wa historia ya dini na binaadamu ni kitendo cha kurejea kwa Wayahudi kwenye Ardhi Takatifu miaka takriban 2000 baada ya kuondolewa hapo na Mwenyezi Mungu Mtukufu. "*Jerusalem katika Qur'ani"* inaendeleza somo kuanzia pale ambapo "*Dini ya Abrahamu na Nchi ya Israeli – Mtazamo wa Qur'ani"* ilimalizia katika kujaribu kutumia *Qur'ani* kuelezea hadhi ya ya Jerusalem na kuipitia historia ya mji mtakatifu kama ilivyoelezewa katika *Qur'ani.* Muhimu zaidi, "*Jerusalem katika Qur'ani"* inajaribu kufumbua na kuelezea hatma ya Jerusalem na ile ya Ardhi Takatifu. Kilichojitokeza baada ya uchunguzi wa kina wa jambo hilo ni mchanganuo na maelezo ya kina yanayogusa na kuyahusisha matukio ya kimataifa ya kisiasa na kiuchumi ya zaidi ya karne moja yanayohusiana na tukio hilo ambalo bado linanendelea kujitokeza na kuendelea kupevuka iku hadi siku katika Ardhi Takatifu. Tunagundua pia kuwa, hivi sasa tuko katika hatua ambamo moja ya "*Nchi Tawala*", ikimaanisha Marekani, imo mbioni kubadilishwa na nafasi yake kuchukuliwa na "*Nchi Tawala*" nyingine, ikimaanisha Nchi ya Israeli, katika mfumo kama ule ambapo Uingereza ilibadilishwa kama "*Nchi Tawala*"na nafasi yake kuchukuliwa na Marekani baada ya vita kuu ya Kwanza ya Dunia. Mabadiliko hayo yalifanikishwa kwa kitendo cha kigaidi kilichotokea kiangazi cha mwaka 1914. Mabadiliko hayo hivi sasa yanatokea katika mfumo unaolingana na ule wa kabla yake. Wakati ule, mwaka 1914, wahusika waliwatuhumu Warusi kwa kitendo hicho cha ugaidi. Mara hii, wanaolaumiwa kwa kitendo cha mashambulizi ya mwezi Septemba tarehe 11 ni Waarabu na Waislamu.

Ni kwa kutumia uwezo wa ujuzi wa maarifa yanayoashiria peke yake (Firasa) ndipo mtu anaweza kuthibitisha kuwa sasa tunaishi katika zama za majaribu (*Fitan*), zikiwa ni hatua ya mwisho katika mchakato na mpito wa historia. Ujuzi na elimu za kisayansia na za majaribio zinaweza tu kudhani, lakini hazitaweza kupenya na kuona moja kwa moja, hali halisi ya zama ambazo hivi sasa tunaishi. Hatua inayofuatia baada ya kuthibitisha kuwa tumo katika zama za majaribu (*Fitan*), ni kuwa jamii za Waislamu wa kweli (*Jama'ah*) wakiwa na *Maimamu / Maamiri* wa kweli, lazima sasa wajikusanye, wawe na washikamane pamoja, kwa nguvu kubwa zaidi hivi sasa kuliko wakati mwingine wowte, na waumini wote lazima washikamane nao kwa *as-sam'u wa-ta'-atu* (kusikiliza na kufuata amri), kwani hiyo ndiyo amri ya Mtume (*rehma na amani juu yake*). Jamii hizo ndogo ndogo za Kiislamu zikiwa na maosko yake madogo madogo zinaweza kuanzishwa vizuri tu ikiwa Waislamu wataiacha miji isiyokuwa na iliyomkifu Mwenyezi Mungu na kuhamia mashambani kuanzisha Vijiji vya Kiislamu. Kitabu, "*Umma Mmoja Amiri Mmoja – Mpangilio wa Jumuiya ya Kiislamu katika zama za Majaribu"* kinaelekeza na kufafanua suala hili muhimu. Kazi nzuri na muhimu sana aliyoifanya Dk. Ansari katika kitabu chake "*Misingi ya Qur'ani na Mfumo wa jamii ya Kiislamu"*

iliyo katika sehemu mbili, pia inatoa muongozo mzuri na muhimu wa *Qur'an*i kwa wale ambao wangejikita katika jitihada hizo na ambao wangehitaji misingi ya *Qur'an*i na mfumo wa jamii ya Kiislamu (katika vijiji hivyo au Nchi hizo).

*Uislamu* katika hatua hizo za Vijiji vya Kiislamu (micro-*Islam*) na masoko yao umependekezwa kwa kuwa 'macro-*Islam*' (*Dar-al-Islam*) haziwezi kuanzishwa katika dunia iliyokuwa imemkifu Mwenyezi Mungu, dunia ambayo imeshikwa na wenye nguvu ambao wamo katika vita kuupiga *Uislamu*. Vita hiyo ilikwishafanikiwa kuuvunja Ukhalifa wa Kiislamu. Hivyo vita hiyo haikuanza Septemba 11 wakati Wayahudi na washirika wao walipoishambulia Marekani na kuwalaumu Waislamu. Kwa muda wote ambapo vita hiyo itakuwa ikiendelea haiwezekani kwa *Uislamu* wa kweli kuchukua Nchi yoyote ile duniani na kuanzisha utawala wa Kiislamu popote pale duniani. Sehemu pekee ambayo hilo linawezekana, ni ardhi au eneo ambalo Mtume (*rehma na amani juu yake*) alilitaja kama *Khorasan* (Afghanistan iko katikati ya *Khorasan*). Muda umefika kwa Waislamu kuamka na kugundua hali halisi na ukweli huu mchungu na kutoa majibu dhidi ya hali hiyo kwa kuelekeza juhudi zao (bila kujali watu wangapi watapoteza maisha yao na itchukua muda gani) kurudisha na kusimamisha upya *Dar-al-Islam* katika ardhi hiyo. Kiini cha wazo la 'Kijiji cha Kiislamu' kimo katika uwezekano wa kulea Waislamu ambao wangeishi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Allah, na ambao, mwisho wake, wangekufa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mmoja, Allah!

Hakuna ambaye ataweza kukabili changamoto hizo bila ya kwanza kufahamu na kuelewa asili na mfumo mzima wa changamoto hizo. "*Khalifa – Hejaz na Nchi na Taif la Wahhabi wa Saudia"* inaelezea historia katika kiwango cha 'macro'-*Islam*, Uislamu Kitaifa ambacho ni kitabu kinachojibu maswali yafuatayo:

- Nani alivunja Ukhalifa?
- Kwanini ulivunjwa?
- Jinsi gani ulivunjwa?
- Kitu gani kiliwekwa badala yake (Ukhalifa)?
- Ni namna gani dunia ya Kiislamu ilijibu tukio la kuvunjwa kwa Ukhalifa?
- Nini hatma ya Ukhalifa?

Uchunguzi wa kina wa matukio na historia kwa kutumia vyanzo visivyo na shaka vimeonyesha kuwa pamefanywa usaliti wa hali ya juu kabisa kwa dini ya *Kiislamu* uliofanywa na *Wahhabi wa Saudia* katika kuvunja Ukhalifa na kuzuia usirudishwe. Hivyo kuna kushabihiana kati ya Nchi ya Israeli (ya kidunia, isiyomtambua Mwenyezi Mungu) katika Ardhi Takatifu na Nchi ya kidunia ya Saudi Arabia katikati ya ardhi ya Kiarabu ambapo ndipo penye moyo wa *Uislamu*. Katika kuanzishwa kwa nchi hizi zote mbili, Waingereza wamejihusisha moja kwa moja. Nchi hizi zote mbili zimeweza kuwapo hadi leo kwa kusaidiwa mwanzo na (visiwa vya) Uingereza na baadaye Marekani. Nchi ya sasa ya Israel, imeanzishwa au imerejeshwa kilaghai, imewasaliti Wayahudi na inawapeleka kwenye kuangamizwa, na Saudi Arabia pia ni Nchi ya kilaghai na inatimiza lengo kama hilo kati ya Waislamu. Nchi zote mbili, Israeli na Saudi Arabia zitapata pigo hilo hilo wakati *Imam al-*

*Mahdi* atakapojitokeza na Ukhalifa wa Kiislamu kurejeshwa, zote zitateketezwa na zitaelekezwa kwenye fuko la takataka la historia. Wafuasi wengi wa Kiislamu wa *Kisalafi* wanakubaliana na mtazamo huu kuhusu historia ya kuvunjika kwa Ukhalifa na usaliti wenye kuangamiza uliofanywa na *Wahhabi wa Saudia*.

*Maulana* Ansari alimtuza *Shekhe* wake, *Maulana* ‘Abdul Aleem Siddiqui, kwa kuanzisha Taasisi ya Aleemiyah ya Masomo ya Kiislamu nchini Pakistani, na kwa kutayarisha Toleo la Kumbukumbu ya Aleemiyah. Toleo la Kumbukumbu ya Ansari, ikiwemo pendekezo la Kitivo cha Ansari cha Eskatolojia ya Kiislamu ambacho punde kitaanzishwa, *Insha Allah*, linawakilisha jaribio la jitihada za kinyenyekevu katika kufuata mfano huo mtakatifu wenye wingi wa utiifu.

# *Dibaji kwa toleo la pili*

Kitabu hiki, kilichoandikwa miaka 37 iliyopita, mnamo mwaka 1976, ukweli kabisa ni sura kutoka katika tasnia yangu kuhusu '*Uislamu baada ya Ukhalifa na Kutafuta Mfumo Mpya wa Utaratibu wa Kijamii'* ya shahada ya uzamivu katika Uhusiano wa Kimataifa kwenye Chuo cha Kimataifa cha Masomo ya Uhusiano wa Kimataifa kilichopo Geneva, Uswisi. Niliondoka Geneva mwaka 1979 bila kuwakilisha tasnia yangu (ambayo ilikuwa karibu imekamilika na nilitumia miaka mitano iliyofuatia nikiwa nimeajiriwa na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ya Serikali ya Trinidad na Tobago.

Hatimaye niligundua baada ya kuondoka Geneva kuwa utafiti wangu juu ya somo hilo litabaki kwa kiwango kikubwa bila kukamilika bila ya kujikita kusomea na kuelewa vizuri elimu ya eskatolojia ya Kiislamu. Ilinichukua miaka mingi na jitihada kubwa sana kuweza kuielewa elimu hii ya eskatolojia ya Kiislamu, na hata kufikia hapo, nalazimika kukiri kuwa kuna sehemu kadhaa za elimu hiyo ambazo bado zinaniwia ugumu kuzielewa. Hata hivyo, nimeamua kuanzisha, Insha Allah, chuo cha Eskatolojia ya Kiislamu, mahali ambapo somo hilo litafundishwa. Kwa kadiri ya uelewa wangu, hakuna chuo wala kitivo cha namna hii popote pale duniani katika ulimwengu wa Kiislamu.

Toleo hili la kitabu hiki, kikiwa na 'Utangulizi' mpya, linajumuisha uchambuzi wa kieskatolojia wa somo hilo, mada ambayo ilikosekana kwenye toleo la kwanza.

Hivi sasa tunajua kuwa, kwa sababu ya eskatolojia ya Kiislamu, utawala wa Khalifa wa Kiislamu utarejeshwa upya pale atakapojitokeza Imam al-Mahdi na atakaporejea Nabii Isa (alayhi al-Salaam) huenda ndani ya miaka 25-30, lakini pia tunajua kwamba hayo hayawezekani kutokea ikiwa mfumo wa Ya'juj na Ma'juj unaendelea kuwapo duniani.

Ukosefu wa muda hauniruhusu kupata fursa ya kukiandika upya kitabu hiki, hivyo basi nalazimika kuridhika na kuandika Utangulizi mpya na kuongezea hapa na pale baadhi ya sehemu za kitabu hiki. Hata hivyo, kuna mihadhara yangu mingi kuhusiana na mada kadhaa kama vile 'Imamu al-Mahdi na Kurejea kwa Ukhalifa', 'Imamu al-Mahdi na Zama za Mwisho', 'Pax Islamica: Mfumo wa Mpangilio wa Kimataifa', 'Kutekwa kwa Konstantinopoli katika Zama za Mwisho' n.k. vitabu kama vile 'Jerusalem katika Qur'ani' na tungo kama vile 'Je, Waislamu wanaweza kupiga kura kwenye Changuzi za Taifa la Kisasa la Kidunia' ambavyo, ikiwa vitangaliwa au vitasomwa pamoja na kitabu hiki, vitatoa fursa nzuri na bora kabisa ya kuweza, Insha Allah, kulielewa vizuri somo na kina cha mada ya elimu ya kieskatolojia.

Nyaraka tatu muhimu sana zimejumuishwa kama viambatanishi. Zote zina umri usiopungua takriban miaka 100 na zote ziko kwenye mifumo iliyo wazi ya kijumuiya.

Mwenyezi Mungu ambariki Monowara Begum, ambaye muda si mrefu uliopita alifariki dunia huko Bangladeshi, ambaye kwa jina lake, nimepokea mchango uliowezesha kukidhi gharama za uchapishaji wa toleo hili jipya la kitabu hiki. Pia naishukuru Taasisi ya Kumbukumbu ya Syed-Syeda ya Bangladeshi (iliyoanzishwa na Marhuum Mohammad Ezharul Hoque kwa kumbukumbu ya wazazi wake Marhuum Syed Ahmed na Marhuuma Syeda Khatuun) kwa mchango wao ambao pia umesaidia

kukidhi gharama za uchapishaji wat oleo hili. Mwenyezi Mungu awarehemu na kuzifanyia wepesi roho zao na awajaalie *Jannah al-Firdaus. Amin!*

Imran N. Hosein
Gombak, Kuala Lumpur
Rabi al-Thani 1434 / Machi 2013

# *Dibaji kwa toleo la pili*

Hiki ni kitabu cha tatu katika mfululizo wa kumbukumbu za Ansari, vinavyochapishwa kumuenzi mwalimu wangu na shekhe, *Maulana* Dr. Muhammad Fadlur Rahman Ansari (1914 – 1974). Vitabu viwili vilivyotangulia hiki ni: '*Dini ya Abrahamu na Nchi ya Israeli – Mtazamo wa Qur'ani'* na *'Umuhimu wa kuzuia Riba katika Uislamu'.*

Sehemu kubwa ya utafiti kwa ajili ya kuandika kitabu hiki ulifanywa mnamo miaka ya 1975 – 1979 katika maktaba ya Jumuiya ya Umoja wa Mataifa iliyopo *Palais des Nations*, Geneva, wakati nikiwa mwanafunzi wa shahada ya juu ya ukufunzi (Ph.D.) katika fani ya Uhusiano wa Kimataifa katika kitivo cha Uhusiano wa Kimataifa cha Geneva, Switzerland.

Katika muda huu ninapoandika kitabu hiki, tunajikuta leo hii tumo katika wakati mgumu katika Umma wa Waislamu huku pakiwa na vita vya umwagaji damu na matatizo magumu yanayosababishwa nayo ambayo ni magumu mno kupita kiasi cha kufikirika na kuelezeka huko Bosnia, Kashmir, Algeria, Palestina, Chechnya n.k. Jana ilikuwa wanawake wa Kiislamu walionajisiwa Bosnia, leo tunasikia habari za mtoto aliyelazimishwa ang'oe kwa meno sehemu za siri za baba yake huko Bosnia, huku Shekhe Omar Abdul Rahman ambaye ni kipofu, bila kuwa na hatia, amehukumiwa kifungo cha maisha huko Marekani (kisa ameonekana kuwa ni tishio kubwa kwa watawala wenye msimamo wa kidunia wa Egypt amabo wamejiweka sambamba na mwelekeo wa kimagharibi), ambaye anadhalilishwa kingono kila anapokuwa na mgeni kuja kumtembelea hapo jela alipofungwa.

Hivi sasa nimejitosheleza kihoja kuwa muda umefika kwa kazi hii kuwafikia umma wa Waislamu ambao huenda hadi sasa wamekwishapata mshtuko wa kutosha ili tuweze kujiangalia kwa mwanga mpya na kutambua je, ni kitu gani kilichotusababishia kukosa nguvu za, na uwezo wa kujikinga na hizi athari zote zinazotukuta. Huenda, kutokana na kazi hii, wakatilia maanani na kukubaliana na mtazamo huu, na hivyo kuweza kutojali na kuyakana makanusho ninayoyatarajia kutoka kwa wasomi walio chini ya himaya, pamoja na serikali wanazoziunga mkono, kote katika dunia na jamii za Kiislamu.

Ninasali na kumuomba Allah aukubali na kuupa rehma zake huu mchango wangu mdogo katika kupigania Ukweli. Uwawezeshe Waislamu kugundua na waone kwa kufunguliwa macho yao jinsi gani utawala wa Wahhabi wa Saudi ambao sasa una mamlaka juu ya *Haramain* na *Hejaz* ulivyojikita kwa vitendo katika kuuangusha utawala wa Kiislamu wa Khalifa na tangu hapo kujiweka kuwa ni kikwazo katika jitihada zote za kufufua nguvu za *Umma wa Waislamu. Amin!*

Imran N. Hosein
Masjid Dar al-Qur'an, Long Island, New York,
Mwezi wa kumi na moja. Jumadi al-Thani 1417 / Novemba 1996

# KHALIFA - HEJAZ NA TAIFA LA WAHHABI WA SAUDIA

## *Utangulizi*

“Mfumo wa Khilafah katika Uislamu hauwakilishi ofisi za Taifa la Kiislamu peke yake. Unawakilisha Taifa lenyewe.”

## *Taifa la Khilafah la Kiislamu na mfumo bandia mbadala unaotumika*

Mfumo wa Dajjal wa nchi za Kitaifa zenye mwelekeo na msimamo wa kidunia, iwe ni jamhuri au za kifalme, ambao umeikumba dunia nzima – zikiwemo nchi za Kiislamu – ni mfumo bandia, usio halali na wa kughushi, unaotumika kama mfumo mbadala wa Khilafah ya Kiislamu. Ukweli huu wa kimsingi unaonyesha dalili za ajabu za kumpiga chenga Dr Muhammad Iqbal, mtu ambaye alikuwa mmoja wa wanazuoni mashuhuri sana wa Kiislamu katika zama hizi mpya za kisasa. Mtazamo wa Iqbal juu ya suala hili, aliouelezea kwenye moja ya kazi zake muhimu kuliko zote za kitaalamu ‘*The Reconstruction of Religious Thought in Islam’ – ‘Uundaji Upya wa Fikra za Kidini katika Uislamu’* ilikubaliana kabisa na msimamo bandia na wa kughushi wenye mwelekeo wa kidunia wa Ijtihad uliofanywa na Waturuki ambao kwao “kwa mujibu wa msimamo wa Kiislamu, Khilafa au Mamlaka ya Kadhi yanaweza kukabidhiwa kwenye chombo cha watu au Bunge lililochaguliwa.” (tazama fn 8, ukurasa wa 82, kupata nukuu nzima na kamili.)

Bila kujali kama nchi hiyo ni Pakistani, Saudi Arabia, Uturuki, Malaysia, Iran au Egypt, zote hizi ni nchi za kisasa zenye msimamo na mwelekeo wa kidunia kwa mujibu wa mantiki kuwa zote ziko chini ya himaya ya chombo chenye msimamo na mwelekeo wa kidunia ambacho ni Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, ambalo limeanzishwa na Wazayonisti. Wote wanalazimika kutii amri na masharti ya International Monetary Fund (IMF) - Shirikisho la Fedha la Kimataifa (SFK) ambalo limepiga marufuku matumizi ya Dinari za dhahabu kutumika kama pesa.

Pale ambapo Waislamu wanashiriki kwenye siasa ndani ya Taifa la kisasa lenye msimamo na mwelekeo wa kidunia, kwa mfano kwa kupiga kura kwenye chaguzi au kugombea nafasi za madaraka kwenye chaguzi hizo kwa kuwakilisha vile vinavyoitwa vyama vya Kiislamu, au kutamka au kwa vitendo kutoa matamshi ya kutii amri na maamuzi ya Mfalme, Raisi, *Amir*, Katiba n.k. wote wanakuwa wanahalalisha hilo taifa bandia mbadala na la kizushi. Zaidi, wanakuwa wanapigilia msumari wa ziada kwenye jeneza na Taifa la *Khilafa.*

Kitabu hiki kinawekwa wazi kwa Waislamu wa aina hiyo ili kuhakikisha kuwa itakapofika Siku ya Qiyama hawatoweza kuomba msamaha kwa kutoa sababu isiyokuwa na uzito ya madai kuwa: “Sikujua!”

Baada ya hapo tujiulize, je, Taifa la Khilafa ni kitu gani?

Moja kati ya wasifa muhimu wa dini ya Kiislamu ni msisitizo wake kuwa pale pote ambapo watu wanamtambua Allah, Mwenyezi Mungu Mtukufu kuwa ni (*al-Malik*) ‘mfalme huria’, basi wanapaswa kuhakikisha kuwa Nchi na vyombo vyake vyote vya utawala vinakiri na kufuata sheria zake na amri zake Allah kuwa ni amri na sheria kuu zisizokuwa na upinzani.

Ikiwa Nchi, badala ya Allah, Mtukufu, inatambuliwa kuwa ni utawala huria, basi kwa mujibu wa Kiislamu, huo ndio mwanzo na kiini cha mfungamano na mwelekeo wa kidunia (secularism), na huitwa (*Shirk*) kufuru na hiyo ni dhambi kubwa kuliko dhambi zote na ni dhambi isiyokuwa na msamaha mbele ya Mwenyezi Mungu, *Subhanna wa Talaa*. Tafakari matamshi yafuatayo ya Allah, Mtukufu wa Daraja, yaliyomo ndani ya Qur’ani kuhusu suala la ‘msamaha kwa kutenda *Shirk*’:

إِنَّ ٱللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَن يُشْرَكَ بِهِۦ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَٰلِكَ لِمَن يَشَآءُ ۚ
وَمَن يُشْرِكْ بِٱللَّهِ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَٰلًۢا بَعِيدًا ﴿١١٦﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu hasamehi kushirikishwa (*kunakojumuisha hadhi ya utakatifu, nguvu au uwezo, mamlaka na majukumu tegemezi ambayo ni Yake*) na kitu (*au mtu*) (*ikimaanisha, kutenda Shirk*). Lakini Yeye husamehe yasiyo kuwa hayo kwa amtakaye. Na anaye mshirikisha Mwenyezi Mungu basi huyo amepotea upotovu wa mbali.”
(Msomaji anatahadharishwa kuwa yaliyo kwenye mabano ni masherehesho ya mwandishi)

(Qur’ani, al-Nisaa, 4:116)

إِنَّ ٱللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَن يُشْرَكَ بِهِۦ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَٰلِكَ لِمَن يَشَآءُ ۚ وَمَن
يُشْرِكْ بِٱللَّهِ فَقَدِ ٱفْتَرَىٰٓ إِثْمًا عَظِيمًا ﴿٤٨﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu hasamehe (*na hatosamehe*) kushirikishwa (*Shirk*), na husamehe yaliyo duni ya hilo kwa amtakaye. Na anaye mshirikisha Mwenyezi Mungu (*Shirk*) basi hakika amezua dhambi kubwa.”

(Qur’ani, an-Nisa, 4:48)

لَقَدْ كَفَرَ ٱلَّذِينَ قَالُوٓا۟ إِنَّ ٱللَّهَ هُوَ ٱلْمَسِيحُ ٱبْنُ مَرْيَمَ ۖ وَقَالَ
ٱلْمَسِيحُ يَٰبَنِىٓ إِسْرَٰٓءِيلَ ٱعْبُدُوا۟ ٱللَّهَ رَبِّى وَرَبَّكُمْ ۖ إِنَّهُۥ مَن يُشْرِكْ
بِٱللَّهِ فَقَدْ حَرَّمَ ٱللَّهُ عَلَيْهِ ٱلْجَنَّةَ وَمَأْوَىٰهُ ٱلنَّارُ ۖ وَمَا لِلظَّٰلِمِينَ مِنْ
أَنصَارٍ ﴿٧٢﴾

Hakika wamekufuru walio sema: Mwenyezi Mungu ni Masihi mwana wa Maryamu! Na hali Masihi mwenyewe alisema: Enyi Wana wa Israili! Muabuduni Mwenyezi Mungu, Mola wangu Mlezi na Mola wenu Mlezi. Kwani anaye mshirikisha (anayetenda *Shirk)* Mwenyezi Mungu, hakika Mwenyezi Mungu atamharimishia Pepo, na mahala pake ni Motoni. Na walio dhulumu hawatakuwa na wa kuwanusuru.

(Qur’ani al-Maida, 5:72)

Ni wazi kutokana na aya tulizoziweka wazi hapo juu, kwamba wana wa Israeli walikuwa wakitenda Shirk (wakimshirikisha Mwenyezi Mungu) – na ndipo walipopewa onyo na Mwenyezi Mungu la moto wa Jahannamu.

حُنَفَآءَ لِلَّهِ غَيْرَ مُشْرِكِينَ بِهِۦ ۚ وَمَن يُشْرِكْ بِٱللَّهِ فَكَأَنَّمَا خَرَّ مِنَ
ٱلسَّمَآءِ فَتَخْطَفُهُ ٱلطَّيْرُ أَوْ تَهْوِى بِهِ ٱلرِّيحُ فِى مَكَانٍ سَحِيقٍ ﴿٣١﴾

“Kwa kumtakasisishia Imani Mwenyezi Mungu, bila ya kumshirikisha. Na anaye mshirikisha Mwenyezi Mungu ni kama kwamba ameporomoka kutoka mbinguni, kisha ndege wakamnyakua au upepo ukamtupa pahala mbali.”

(Qur’ani, al-Hajj, 22:31)

Tulikwishasema hapo mwanzoni kuwa pale ambapo Taifa linatambulika au linajitambua kuwa ni huria (*al-Malik*) badala ya Allah, Mtukufu, hilo tendo linajumuisha *Shirk* ndani yake. Lakini pia Shirk inatendwa pale ambapo Taifa (na serikali) linapopitisha sheria na kulifanya jambo fulani kuwa Haram au kinyume na sheria, ilhali jambo hilo hilo Mwenyezi Mungu ameliamrisha kuwa ni Halal au linalokubalika. Ushahidi wa msimamo huu unapatikana katika Surah al-Taubah ya Qur'ani:

اتَّخَذُوٓا۟ أَحْبَارَهُمْ وَرُهْبَـٰنَهُمْ أَرْبَابًا مِّن دُونِ ٱللَّهِ
وَٱلْمَسِيحَ ٱبْنَ مَرْيَمَ وَمَآ أُمِرُوٓا۟ إِلَّا لِيَعْبُدُوٓا۟
إِلَـٰهًا وَٰحِدًا ۖ لَّآ إِلَـٰهَ إِلَّا هُوَ ۚ سُبْحَـٰنَهُۥ عَمَّا
يُشْرِكُونَ ﴿٣١﴾

"Wamewafanya makuhani wao na wamonaki (*wachungaji*) wao kuwa ni Miungu na Mabwana watawala badala ya Mwenyezi Mungu, na pia (wamefanya hivyo hivyo kwa) Masihi bin Maryamu. Na wala hawakuamrishwa (*hivyo*) isipo kuwa (waliamrishwa) wamuabudu Mungu Mmoja, hapana mungu (*mwingine*) ila Yeye. Subhanahu, Ametakasika na hayo wanayo mshirikisha nayo."
(Msomaji anatahadharishwa kuwa yaliyo kwenye mabano ni masherehesho ya mwandishi)

(Qur'ani, al-Taubah, 9:31)

Qur'ani ilikwisha lizungumzia suala la ibada za Wakristo na Wayahudi zilizoelekezwa kwa Makasisi, Wachungaji na Marabbai wao katika aya nyingine kama ifuatavyo:

قُلْ يَـٰٓأَهْلَ ٱلْكِتَـٰبِ تَعَالَوْا۟ إِلَىٰ كَلِمَةٍ سَوَآءٍۭ بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمْ أَلَّا
نَعْبُدَ إِلَّا ٱللَّهَ وَلَا نُشْرِكَ بِهِۦ شَيْـًٔا وَلَا يَتَّخِذَ بَعْضُنَا بَعْضًا أَرْبَابًا
مِّن دُونِ ٱللَّهِ ۚ فَإِن تَوَلَّوْا۟ فَقُولُوا۟ ٱشْهَدُوا۟ بِأَنَّا مُسْلِمُونَ ﴿٦٤﴾

Sema: Enyi Watu wa Kitabu! Njooni kwenye neno lilio sawa baina yetu na nyinyi: Ya kwamba tusimuabudu yeyote ila Mwenyezi Mungu, wala tusimshirikishe na chochote; wala tusifanyane sisi kwa sisi kuwa Miungu Mitukufu badala ya Mwenyezi Mungu. Na wakigeuka basi semeni: Shuhudi- eni ya kwamba sisi ni Waislamu.

(Qur'ani, Ale-Imran, 3:64)

Hata hivyo palijitokeza swali: Je, Wakristo na Wayahudi kweli waliwaabudu Makasisi na Marabbai wao?

> 'Adi bin Hatim, ambaye alikuwa Mkristo kabla ya kuupokea na kuslimu na kuwa Muislamu, alikuja kwa Mtume (*rehma na amani juu yake*). Alipomsikia akiisema aya hii hapo juu, alisema, "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, lakini (Wakristo na Wayahudi) hawawaabudu (Makasisi na Marabbai wao)." Mtume (*rehma na amani juu yake*) akamjibu, Ndiyo, lakini wanawakataza watu yale yaliyo Halal na kuwaruhusu yale ambayo ni Haram. Na hili ndiyo linawafanya wawe wanawaabudu.'
>
> (Sunan Tirmidhi)

Siyo tu kuwa sasa tunajua ni tendo gani la *Shirk* lilikuwa likifanywa na Waisraeli, bali pia tuna haki ya kuuliza swali jepesi na rahisi kama ifuatavyo: Ikiwa tendo ni Shirk likifanywa na Makasisi na Marabbai, je, haitokuwa ni Shirk ikiwa tendo hilo hilo au kama hilo likifanywa na Taifa au serikali?

Qur'ani inaweka msisitizo mkubwa katika kurudia tena na tena maonyo kwa wale (kama walivyo Waislamu) ambao wameteremshiwa Andiko / Neno na kisha baada yah apo wanawageukia wale wasiokuwa Allah na kuukabidhi uhuru kwenye Taifa, na kujipa mamlaka ya juu kabisa kwenye utawala na sheria za nchi. Onyo hilo linabeba uzito mkubwa kabisa pale ambapo Taifa linapitisha sheria kukataza (ikim. kufanya iwe *Haram*) kile au yale ambayo Allah ameyaruhusu (ikim. kayaamrisha yawe *Halal*)

Leo hii, duniani kote, Nchi za kisasa zenye msimamo na mfungamano wa kidunia zinatambulika kuwa ni Nchi huru. Mamlaka yake yanatambulika kuwa ni ya mwisho na sheria zake zinatambulika kuwa ni hivyo pia. Hivyo basi, leo hii duniani kote binaadamu wameukumbatia mfumo mzima wa kisiasa wenye msingi na mizizi ya kufuru (*Shirk*). Nchi hizo zimekataza mambo mengi ambayo Mwenyezi Mungu ameyaruhusu, na zimeruhusu mambo mengi ambayo Mwenyezi Mungu ameyakataza. Isitoshe, kote duniani binaadamu wote (*illa ma sha Allah*) wameyakubali yote ambayo Nchi au Taifa limeyafanya. Adhabu ya Mwenyezi Mungu kwa kosa hilo ni harsh.

Mifano inayojitokeza mwanzoni mwa yote miongoni mwa matendo hayo ya Shirk ni pale ambapo Taifa la kisasa linaporuhusu kukopesha pesa kwa riba na kukataza kutumika

kwa sarafu za dhahabu (Dinari) na fedha (Dirhamu) kama pesa au nyenzo mahususi kwa mauzo na manunuzi ya bidhaa na huduma.

Hebu tafakari aya ifuatayo ya Surah al-Maidah na hususan tafsiri ya maneno ambayo yako kwenye mlazo (italic):

إِنَّآ أَنزَلۡنَا ٱلتَّوۡرَىٰةَ فِيهَا هُدٗى وَنُورٞۚ يَحۡكُمُ بِهَا ٱلنَّبِيُّونَ ٱلَّذِينَ
أَسۡلَمُواْ لِلَّذِينَ هَادُواْ وَٱلرَّبَّٰنِيُّونَ وَٱلۡأَحۡبَارُ بِمَا ٱسۡتُحۡفِظُواْ
مِن كِتَٰبِ ٱللَّهِ وَكَانُواْ عَلَيۡهِ شُهَدَآءَۚ فَلَا تَخۡشَوُاْ ٱلنَّاسَ
وَٱخۡشَوۡنِ وَلَا تَشۡتَرُواْ بِـَٔايَٰتِي ثَمَنٗا قَلِيلٗاۚ وَمَن لَّمۡ يَحۡكُم بِمَآ
أَنزَلَ ٱللَّهُ فَأُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلۡكَٰفِرُونَ ٤٤

"Hakika Sisi tuliteremsha Taurati yenye uwongofu na nuru, ambayo kwayo Manabii walio nyenyekea kiislamu, na wachamngu, na wanazuoni, waliwahukumu Mayahudi; kwani walikabidhiwa kukihifadhi Kitabu cha Mwenyezi Mungu. Nao wakawa ni mashahidi juu yake. Basi (Enyi wana wa Israeli) msiwaogope watu, bali niogopeni Mimi. Wala msibadilishe Aya zangu kwa (vitu vya) thamani ndogo: *Na wasio hukumu kwa mujibu wa yale aliyo teremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio makafiri*."

وَكَتَبۡنَا عَلَيۡهِمۡ فِيهَآ أَنَّ ٱلنَّفۡسَ بِٱلنَّفۡسِ وَٱلۡعَيۡنَ بِٱلۡعَيۡنِ
وَٱلۡأَنفَ بِٱلۡأَنفِ وَٱلۡأُذُنَ بِٱلۡأُذُنِ وَٱلسِّنَّ بِٱلسِّنِّ وَٱلۡجُرُوحَ
قِصَاصٞۚ فَمَن تَصَدَّقَ بِهِۦ فَهُوَ كَفَّارَةٞ لَّهُۥۚ وَمَن لَّمۡ
يَحۡكُم بِمَآ أَنزَلَ ٱللَّهُ فَأُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلظَّٰلِمُونَ ٤٥

"Na humo (ndani ya Taurati) tuliwaandikia ya kwamba roho kwa roho, na jicho kwa jicho, na pua kwa pua, na sikio kwa sikio, na jino kwa jino, na (vivo hivyo) kwa majaraha kisasi. Lakini atakaye samehe basi itakuwa ni kafara kwake. *Na wasio hukumu kwa yale aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio madhaalimu."*

وَقَفَّيْنَا عَلَىٰٓ ءَاثَٰرِهِم بِعِيسَى ٱبْنِ مَرْيَمَ مُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ مِنَ ٱلتَّوْرَىٰةِ ۖ
وَءَاتَيْنَٰهُ ٱلْإِنجِيلَ فِيهِ هُدًى وَنُورٌ وَمُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ مِنَ ٱلتَّوْرَىٰةِ
وَهُدًى وَمَوْعِظَةً لِّلْمُتَّقِينَ ﴿٤٦﴾

"Na (katika nyayo zao) tukawafuatishia hao Isa bin Maryamu kuyahakikisha yaliyo kuwa kabla yake katika Taurati, na tukampa Injili iliyomo ndani yake uwongofu, na nuru na inayo sadikisha yaliyo kuwa kabla yake katika Taurati, na uwongofu na mawaidha kwa wachaMungu."

وَلْيَحْكُمْ أَهْلُ ٱلْإِنجِيلِ بِمَآ أَنزَلَ ٱللَّهُ فِيهِ ۚ وَمَن لَّمْ يَحْكُم بِمَآ أَنزَلَ
ٱللَّهُ فَأُو۟لَٰٓئِكَ هُمُ ٱلْفَٰسِقُونَ ﴿٤٧﴾

"Na wahukumu Watu wa Injili kwa yale aliyo teremsha Mwenyezi Mungu ndani yake. Na wasio hukumu kwa yale aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu basi hao ndio wapotofu."

(Qur'ani, al-Maidah, 5:44-47)

Kushiriki kwenye harakati za uchaguzi kwenye Taifa kunakuwa na lengo la kuteua serikali ambayo ingetawala kwa niaba ya Taifa, na wale ambao wanaunda vyama vya siasa (vikiwemo vyama vya siasa vya Kiislamu) na kugombea nafasi kwenye chaguzi hizo, nao wanakuwa wamejiingiza kwenye *Shirk.*

Leo hii duniani kote, ukiacha nchi chache sana, kama zipo, nchi zina mfumo wa kubuni wenyewe wa kisasa wenye msimamo na mfungamano wa kidunia (na hii inajumuisha nchi ya Pakistani – iliyoanzishwa kama nchi ya Kiislamu) huwa zinatambulika kama nchi au jamhuri huru, mamlaka yake hutambuliwa kama ni ya juu kabisa nay a mwisho na hivyo hivyo sheria zake. Hivyo basi, leo hii dunia nzima (ukiwemo pia ulimwengu wa Kiislamu) binaadamu ameukumbatia mfumo mpya uliotapakaa kote wa *Shirk* ya kisiasa. Hii, kwa

uhakika, ni moja ya alama kuu zinazoashiria kuwa hivi sasa tunaishi katika enzi za *Dajjal*, Masishi wa uongo au Anti-Kristo, ambaye amefuzu kuudanganya ulimwengu na wanaadamu ili wamwabudu yule asiyekuwa Allah, Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Inabaki kuwa ni moja ya maajabu ya sintofahamu ya umma wa kisasa wa Kiislamu, wanazuoni wa Kiislamu na vyama na makundi ya Kiislamu kama vile *Salafi*, makundi ya *Sufi*, *Ikwan al-Muslim* wa Egypt na mengine kwenye nchi za Kiarabu, *Jama'at-e-Islam* wa Pakistani, *Parti Islam* wa Malaysia, *al-Nahda* wa Tunisia, *Chama cha Haki na Maendeleo (AKP)* cha Uturuki n.k., ambavyo vinashiriki kwenye chaguzi za kisasa za kisiasa, wanaendelea aidha kutoweza au kutotaka kuelewa kuwa huu mfumo mbadala wa kisasa uliobuniwa na utamaduni wa kimagharibi uliopewa nafasi ya Taifa la *Khilafa* la Kiislamu una misingi iliyoegemea kwenye *Shirk*. Shekhe wa Kisufi na mpinzani wake wa Kisalafi / Kiwahhabi, wote wanaonyesha dalili ya upofu wa kushindwa kuliona wazi jambo hili!

Isitoshe, wanashindwa kugundua kuwa mfumo huu wa uchaguzi wa demokrasia wa kisiasa ulioletwa na kuasisiwa na *Dajjal* wa mtu mmoja / kura moja umetengenezwa ili kuvunja na kufuta anuwai za kikabila na kitaifa ambazo Mwenyezi Mungu Mtukufu ameziumba. Taswira na silika za kitaifa na kikabila ni sifa bainifu ambazo zimeumbwa na Mwenyezi Mungu mojawapo ikiwa ni kwa lengo la kuunda na kulinda mshikamano wa kijamii kuanzia kwenye kiwango cha awali, mshikamano ambao ungedhibiti mshikamano wa jamii pana kwa ujumla. Badala yake, mfumo wa kisiasa wa *Dajjal* unamtambua mtu mmoja binafsi kama ndiyo mshirika wa mwanzo katika kujenga mkusanyiko wa Taifa, kitu ambacho kwa ujumla wake kimevunja mshikamano na utiifu wa kikabila ambao umeumbwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Matokeo ya hili ni kuwa dunia nzima ya kisasa inashuhudia, kuvunjika kwa maadili na mshikamano uliokuwapo kiasi kufikia kuanguka kwa mpangilio na utulivu wa kijamii na kuongezeka kwa matendo ya uhalifu na uvunjaji wa amani kwa kiasi cha kuelekea kwenye vurugu kiujumla.

Yale yanayoitwa kuwa ni makundi na mashirika ya Kiislamu (na hapa anajumuishwa na Shekhe wa Kisufi) kijinga wanajisajili kama vyama vya kisiasa chini ya katiba iliyotungwa kwenye mfumo, msimamo na mshikamano wa Taifa la kidunia la kisasa na kisha wanashiriki kwenye jitihada na harakati za chaguzi za kisiasa kutaka kushinda hizo chaguzi na kupata wawakilishi kushika nafasi za uongozi kwenye serikali yenye mfumo na msimamo wa kidunia usiomtambua Mwenyezi Mungu. Kisha wanabaki na tamaa kuwa kwa kutimiza huu utaratibu wa "kitoto wa Disneyland", ambao wenyewe kwa wazi kabisa unapingana moja kwa moja na *Sunnah*, na hufanikiwa pale tu ambapo watatoa *Fatawa* (wingi wa *Fatwa*) kadhaa za kulaani ugaidi na kisha kujiweka sambamba na ugaidi wa Kizayonisti wa Kimagharibi (kama vile ambavyo *Ikhwan al-Muslim* wa Egypt wanavyoonekana kufanya), labda ndipo kwa namna fulani wataweza kuanzisha kile kinachoitwa *Taifa la Kiislamu*. Ni wazi kabisa kuwa Taifa lao la Kiislamu halishabihiani kabisa na *Khilafah* ya Kiislamu, na badala yake linaonekana kuwa ni umbile la kiajabu kwani kuzaliwa kwake kunalazimika

kukumbatiwa na sumu ya *Dajjal* iliyomo ndani ya mfumo wa Taifa la kisasa la kidunia ambalo limo kwenye Shirikisho la Umoja wa Mataifa, Shirikisho la Kifedha la Kimataifa, Benki ya Dunia, n.k.

Huenda sababu ya kushindwa kwa kishindo kikubwa sana kwa upande wa wanazuoni wa (kisiasa) wa Kiislamu na Mishikamano ya Kisufi ambao wamejikita kwenye chaguzi za kisiasa katika hizi zama za kisasa kunatokana na wao kutoweza kugundua undani wa hali halisia wa dunia mpya ya kisasa – uhalisia ambao akili inaweza kuupenya kuingia ndani yake na kuuelewa kupitia somo la Eskatolojia ya Kiislamu (*Ilmu al-Akhir al-Zaman*) au mtazamo wa Kiislamu wa zama za Mwisho.

Mtume wa uongo, *Dajjal*, ndiye muasisi na msanifu mkuu aliyebuni na kujenga mfumo wa kiajabu wa kisasa wenye msimamo na mshikamano wa kidunia usiomtambua Mwenyezi Mungu ambao *Hadithi* maarufu imeelezea kuwa katika kila watu 1000 basi 999 wataingia moto wa Jahannamu. Lakini, kwa bahati mbaya, hata Waislamu inaonyesha hawaifahamu *Hadithi* hii:

> "Amesimulia Abu Sa'id Al-Khudri: Mtume (*rehma na amani juu yake*) alisema: Siku ya Qiyama Allah atasema: Ewe Adam! Adam atajibu: Labbaik Mola wetu, na Sa'daik. Kisha patakuwa sauti kubwa (itakayosema): Allah anakuamrisha uwachukue kutoka miongoni mwa kizazi chako wakazi wa motoni (Jehannamu). Adam atasema: Ewe Mola! Ni wangapi hao wakazi wa motoni (Jehannamu?) Allah atasema: Katika kila 1000, chukua 999. Wakati huo kila mwanamke mwenye mimba atadondosha mzigo alioubeba (mimba itatoka) na mtoto atakuwa na nywele zenye mvi. "Na utawaona binaadamu kama vile wamelewa pombe, wakati hawajanywa pombe, lakini ukali wa adhabu ya Allah." (*Qur'ani, al-Hajj, 22:2*) (Wakati Mtume alipoyatamka maneno haya), maswahaba walishikwa na huzuni kubwa (na woga) kiasi nyuso zao zilibadilika (rangi) ndipo Mtume akasema: Kutoka kwa Ya'juj na Ma'juj watachukuliwa 999, na mmoja kutoka miongoni mwenu. Ninyi Waislamu (kulinganisha na idadi kubwa ya watu wengine wasiokuwa Waislamu) mtakuwa kama unywele mweusi kwenye ubavu wa ng'ombe mweupe au unywele mweupe kwenye ubavu wa ng'ombe mweusi na nina matumaini kuwa mtakuwa robo ya watu wa Peponi. Aliposema hayo tukasema: Allahu Akbar! Kisha akasema: Nina matumaini kuwa mtakuwa moja ya tatu (theluthi) ya watu wa Peponi. Tena tukasema: Allahu Akbar! Kisha akasema: (Nima matumaini kuwa mtakuwa) nusu ya watu wa Peponi. Ndipo tuliposema: Allahu Akbar!
>
> (Sahih Bukhari)

Waislamu wanapomtambua Allah kuwa ni 'mfalme huria' daima hawaitambui Katiba, Bunge, Mahakama Kuu, Serikali n.k. kuwa huru. Uhuru wa Allah unamaanisha kuwapo kwa mamlaka ya mwisho ya dini ya Kiislamu na, hususan, kuwepo kwa sheria takatifu au *Shariah*. Kuwapo kwa mfumo au taasisi ya *Khalifa* kunatambulisha utawala wa Kiislamu juu ya Nchi na maisha ya jumuiya inayoishi ndani ya mipaka ya nchi hiyo. *Khalifa*, ambaye pia alijulikana kama *Amir* au *Imam*, alikuwa ni kiongozi wa jumuiya ya Waislamu. Nao walitoa kiapo cha kumtii *Khalifa* kupitia taasisi ya *Baiy'ah.* Ardhi ambayo jumuiya hiyo iliishi iliitwa *Dar al-Islam*. Iliitwa hivyo kwa kuwa *Amir* alikuwa na uhuru na mamlaka ya kutekeleza sheria na amri takatifu za Allah katika eneo lote la ardhi hiyo.

# *Kuanzia Utawala wa Kikristo wa Ulaya hadi Kufikia kwenye utamaduni wa Kimagharibi wa Dajjal*

Jumuiya ya Kikristo ya bara la Ulaya ya Mashariki pia ilijengwa kwa misingi ya kumtambua Mungu na ufalme wake. Katika ustaarabu huo, hata hivyo, ni Kanisa ndilo lililokuwa likitambulika kama mwakilishi rasmi wa Mungu hapa duniani, na hivyo kupelekea Nchi au Taifa kuwa chini ya mamlaka ya, na amri za Kanisa.

Wakati Dajjal, Mtume wa Uongo, alipotayarisha uvunjaji wa uhusiano baina ya bara la Ulaya magharibi na Konstantinopol, baadaye aliendelea kutayarisha kwa ustadi mkubwa ugomvi baina ya dini na Taifa ambayo ilipelekea kuanguka kwa Kanisa barani Ulaya. Matokeo ya kuanguka huko kwa Kanisa kulisababisha Ulaya Magharibi kupitia mabadiliko ya kimapinduzi yaliyoitikisha misingi yake ya Ukristo na kusababisha Taifa na siasa kuacha kabisa misingi yake ya kumtambua Mungu na kujikita kwenye misimamo na mwelekeo wa kidunia. Shughuli na athari za kidini zilirudishwa nyuma na kuangushwa chini na kuishia kuyahusu maisha binafsi na ibada za mtu mmoja mmoja,

Lakini bara la Ulaya lilipitia migogoro na migongano baina ya dini na Taifa/Nchi iliyosababisha kushindwa kwa kanisa na kuondokewa kwa nguvu zake. Matokeo yakasababisha bara la Ulaya kupitia mapinduzi ya mfumo na misingi ya utamaduni uliokuwapo na hatimaye Nchi / Taifa na siasa zikaingia kwenye misingi ya mfumo mpya wa kidunia. Sura ya mwisho kwenye kitabu cha ugomvi huo, ambao ulipiga muhuri wa mwisho kuthibitisha kung'olewa kwa itikadi za kidini ya Kikristo kushika hatamu kwenye maisha ya jamii ya Ulaya ya Magharibi, iliandikwa na kuletwa na Mapinduzi ya Ufaransa na Amerika. a Shughuli na athari za kidini zilirudishwa nyuma na kuangushwa chini na kuishia kuyahusu maisha na ibada binafsi za mtu mmoja mmoja au ibada za kikundi cha watu binafsi, na dini ikaondolewa kwenye nyanja za siasa na shughuli za Taifa. Papa na Jumuiya ya Wakristo walitolewa kutoka kwenye kundi la wale wenye uwezo wa maamuzi yanayohusu mwenendo wa Taifa. Mungu hakuwa tena akitambuliwa kama mfalme huria (*al-Akbar*). Badala yake, watu walikuwa huru na wakautia uhuru kwenye mfumo mpya wa Taifa lenye misingi ya mfumo wa kidunia. Taifa sasa likawa *al-Akbar*. Kwa bara la Ulaya huo ukawa ndiyo mfumo mpya wenye misingi ya kidunia ambamo *Dajjal* akaanza kuabudiwa badala ya Mungu wa Abrahamu (*alaihi al-Salam*).

Msomaji anapaswa afahamu kuwa taifa la kisasa lenye mfumo wa kidunia lilikuwa ni sehemu muhimu ya mkakati mzima wa kisiasa ambao kutokana nao jumuiya ya Kikristo-Kiyahudi ya Ulaya iliutumia kujihakikishia utawala wa kisiasa duniani kote. Kwa maneno mengine, taifa la kisasa la kidunia lilikuwa limetayarishwa kiasi kwamba lingeuletea ushindi

mshikamano wa Kikristo-Kiyahudi wa Wazayonisti uliotayarisha mfumo mpya wa kisiasa wa dunia ambao ungewawezesha kuitawala dunia nzima. Mpangilio huo wa kisiasa wa dunia nzima, nao, umejumuishwa kwenye kuundwa kwa Taifa la Kiyahudi la Israeli ambalo hatimaye litakuwa Taifa Tawala la dunia. *Dajjal* ni muasisi na mbunifu wa mpango huu.

Wakati misingi ya utawala wa kidini ya Ulaya ya Magharibi imeangamizwa na kujikuta imeukumbatia mfumo na falsafa mpya ya kidunia ilikuwa ni jambo la ajabu kuwa Wakristo wa Ulaya ya Mashariki na wale wasiokuwa wa bara la Ulaya hawakuwa na pingamizi kubwa dhidi ya uvunjwaji huo wa mfumo mtakatifu wa Taifa uliojengwa na mitume David na Solomon (*rehma na amani juu yao wote wawili*), mfumo ambao haukutambua kutenganishwa baina ya dini na siasa na Kanisa na Taifa.

Michango wa kiajabu iliyosababishwa na kinachoitwa Ufalme wa Kiislamu wa Ottomani, mapinduzi ya Kibolsheviki yaliyotekelezwa na Wayahudi / Mabepari wa Wall Street, na vita zisizokuwa na mwisho za Ulaya ya Magharibi dhidi ya Wakristo wa Ulaya ya Mashariki kiujumla na ikiwa dhidi ya Urusi hususan, bado haijafanyiwa utafiti na uchunguzi wa kina wa Kieskatolojia ya Kiislamu. Inabidi iwekwe wazi kuwa, utafiti wa aina hiyo ni lazima utaibuka na Ushahidi kuwa *Dajjal* ndiye muhusika mkubwa akiwa kazini kujaribu kuvunja nguvu na kuugeuza Ukristo wa asili wa Ulaya ya Mashariki uushikilie mfumo na sera za kidunia.

*Dajjal* si tu aliubadilisha Ukristo wa Ulaya ya magharibi na kuifanya sehemu hiyo ya bara la ulaya iukumbatie utamaduni wa kisasa usiomtambua mungu, lakini pia aliupatia uwezo mkubwa sana na nguvu zisizo kifani. Aliweza kufanya hivyo kwa kupitia mageuzi ya kiajabu ya kisayansi na teknolojia ambayo hadi hivi tunavyoongea bado yanaendelea kujifungua duniani. Utamaduni wa kimagharibi ndipo ukazitumia nguvu hizi za aina ya kipekee kujikita kwenye krusedi zisizojali maadili na zisizokuwa na mwisho na kuzilazimisha sehemu zilizobaki za dunia – kwa kutumia ncha ya upanga wa mpiganaji wa krusedi – kuwa chini ya mamlaka ya wakazi hawa wa Ulaya. Hili lilifanikishwa, kwa kiasi kikubwa kwa mashambulizi ya kivita, na pia lilifanikishwa – wakati mwingine kwa kutumia hujuma za kijasusi au pia kwa kutumia kujiingiza kinyemela kwa makundi wakala, pale ambapo walipatikana wananchi waliokuwa tayari kuwa wateja (kama vile umoja wa *Wahhabi wa Saudia* na Kundi la Mustafa Kamal laVijana wa Kituruki) ambao walipigwa msasa kitaalamu na kuwa watumishi wa kujitolea wa magharibi au kuwa pembejeo muhimu ya magharibi bila wenyewe kujitambua.

Mapanga ya wapiganaji wa Krusedi hayakuwaacha salama hata ndugu zao katika imani wa Kikristo. Wapiganaji hao waliivamia Konstantinopol mnamo mwaka 1204 kuuteka nyara mji mzima wakiwa na lengo la kuulazimisha Ukristo wa mashariki uwe chini na kukubali mamlaka ya kiutawala ya Ukristo wa magharibi. Ingawa Ufalme wa Kirumi uliweza kuurudisha upya mji chini ya utawala wake miaka 80 baadaye, ushindi huo haukudumu kwa muda mrefu. Utamaduni wa magharibi ulipata rafiki, Ufalme wa kibeberu wa Ottomani

ambao uliendelea kuuweka Ukristo wa mashariki chini ya kisigino chake kilichotapakaa damu kwa miaka 500 iliyofuatia hapo.

Utamaduni wa kimagharibi uliomiliki nguvu na zana kubwa za kijeshi ulitumia uwezo huo mpya kusababisha na kupigana vita za mashambulizi zilizopelekea kujipatia makoloni ya karibu sehemu zote za dunia zilizokuwa nje ya Ulaya. Hapo ndipo utamaduni wa kimagharibi ukaanza kuitumia nafasi hiyo kubadili tamaduni zote zilizobaki – na kuziunda upya kufuatia mfumo wake mpya wa Ulaya wa Taifa lisilomtambua Mungu lenye msimamo na mwelekeo wa kidunia. Hata kufikia pale ambapo sehemu hizo za dunia zilipouangusha ukoloni, hazikuweza kuupata uhuru wake wote kwani zilikuwa tayari zimefungwa minyororo iliyokwisha tayarishwa na kuwa chini ya himaya ya nchi na watu wa magharibi kupitia mashirika ya kimataifa kama vile Shirika la Umoja wa Mataifa, Shirikisho la Kimataifa la Fedha, benki ya Dunia, n.k. Hiyo ilipelekea dunia nan chi zilizokuwa nje ya bara la Ulaya kujikuta zimenaswa kwenye mtego wa mfumo hatari wa kisiasa na kiuchumi wenye mwelekeo na misingi ya kidunia usiomtambua mungu, na kugeuzwa kwa mwendo mkali kuwa jamii zisizomtambua mungu. Hii ilijumuisha pia nchi na dunia ya Kiislamu. Dunia ya Kiislamu, kwa uhakika, iliwekwa kama lengo maalum la utamaduni huo wa kimagharibi uliotokea bara la Ulaya.

Mchakato wa kuigeuza dunia ya Kiislamu kuwa jumuiya isiyomtambua Mungu kulianza kwa kubadilisha mfumo mzima wa maisha ya jumuiya ukawa wa katika mfumo wa kidunia. Utawala wa Khalifa wa Ottoman, ambao kwa muda mrefu uliutumikia kwa moyo mmoja na kutekeleza malengo na majukumu ya kimkakati kwa faida ya Ulaya ya magharibi (hususan kujiingiza kupigana vita zisizokuwa na mwisho dhidi ya Ukristo wa Kirumi wa Mashariki ambao hadi leo bado ni mpinzani mkubwa wa Ukristo wa Magharibi), na pia katika kuhamisha Khilafah na kuitoa nje ya dunia ya Kiarabu, ukawa umejimaliza mvuto na matumizi yake mbele ya utamaduni wa kimagharibi na ukageuzwa kuwa lengo la kuangamizwa. Sasa iliwalazimu wauvunje. Na hii ikawa ni mfano maalum wa "kupiga ndege wawili kwa jiwe moja." Dunia ya Kiislamu ingepoteza Utawala wake uliokuwa na nguvu kubwa wa Kiislamu, na kwa kuwa Waarabu walishapoteza *Khilafah* kwa kipindi kirefu cha karne kadhaa, kuvunjwa kwa *Khilafah* kungeweza kusababisha kutoweka kabisa kwa mfumo wote wa *Khilafah*. Pigo hili pacha lingeweza kuwapumbaza Waarabu na Waislamu kwani lingeweza kuimarisha kuvutwa na kuingizwa nchi na mataifa hayo ya Kiislamu kwenye mfumo wa kisiasa wa Dajjal wa kimagharibi wenye msimamo na mwelekeo wa kidunia usiomtambua mungu. Hilo likishafanikiwa, lingemuwezesha *Dajjal* kuunda serikali moja ya dunia nzima ambayo ingetawala dunia kwa niaba yake.

## *Kuanzia kwa Ufalme wa Ottomani uliofungamana na magharibi hadi Taifa la Saudia lililofungamana na magharibi*

Uvunjwaji wa Ufalme wa Ottoman, ambao ulitimizwa katika Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia, uliishia kwa kujitokeza na kuanzishwa kwa Taifa la Uturuki lenye mfumo wa kidunia.

Serikali iliundwa na Waturuki wazalendo wenye msimamo wa siasa kali, waliojiweka sambamba na msimamo na mfumo wa ki-magharibi, ambao walikuwa na uhusiano wa karibu kiutendaji na jumuiya ya kisiri ya Kiyahudi. Mwanzoni walimpunguzia nguvu za kiutawala na utendaji Khalifa na kuifanya kuwa ni ofisi, inayofanana na ile ya Papa wa kanisa la Kikatoliki la Kiroma. Hata hivyo, baada ya kuanzishwa kwa mshikamano wa *Khilafat* India ambao ulisababisha mvutano uliokuwa unautishia utawala wa Waingereza juu ya India, Waingereza walimshauri Mustafa Kamal afanye kile kinachohitajika kufanywa na kuivunja *Khilafah* yenyewe.

Hata hivyo mchakato wa kuigeuza dunia ya Kiislamu kuwa jumuiya ya kidunia kuliimarishwa pale ambapo *Hejaz*, chini ya utawala wa Abdul Aziz ibn Saud, nayo ilipojiunga na Mustafa Kamal (Ataturk) katika kuukana na kukiri uongozi na sheria za dini ya Kiislamu kuwa ndiyo mwongozo mtakatifu wa kutawala Taifa. Hapo ndipo Saudi Arabia, ilipotia saini mkataba na kujiunga na Jumuiya ya Umoja wa Mataifa. Hivyo basi, Saudi Arabia, ikiwa ni kiini na chimbuko la Uislamu, ikakumbatia mfumo mpya Dajjal wa Taifa la kidunia ndani ya mfumo huo wa Kimataifa. Tendo hilo likawa limekamilisha kuvunjwa kwa *Dar al-Islam* ambayo ilianzishwa na Mtume Muhammad (*rehma na amani za Allah juu yake*).

Wakati *Hejaz* ilipokuwa *Dar al-Islam* kila Muislamu alikuwa na haki ya kuingia katika eneo hilo, na hakuhitaji viza. Kulikuwa hakuna kitu chochote kinachoitwa uhuru wa Saudia. Kulikuwa hakuna kitu kinachoitwa uraia wa Saudia. Haki ya kuingia kwenye sehemu yoyote ya *Dar al-Islam* ni moja miongoni mwa haki kadhaa ambazo Waislamu walikuwa nazo, ikiwemo haki ya kuishi ndania ya *Dar al-Islam,* hawakuhitaji kibali cha kuishi humo, haki ya kutafuta rizki na maisha katika sehemu yoyote ya *Dar al-Islam,* hawakuhitaji kibali cha kazi n.k.  Kuzaliwa kwa Taifa la kidunia la Saudi Arabia katikati ya kiini cha chimbuko la Uislamu na kubadilishwa kwa *Khilafah* ya Ottomani kuwa Taifa la Uturuki la kidunia kulikofanywa na Mustafa Kamal kumepelekea si tu kwa Waislamu kukataliwa na kunyimwa haki hizo, bali hatimaye kuondolewa kabisa haki hizi zote ambazo Waislamu walikuwa nazo.

Kuvunjwa kwa Ukhalifa na kuzaliwa Mataifa ya Kiislamu ambayo yaliiga mfumo wa kidunia wa Mataifa ya ki-magharibini ilikuwa ni matukio yaliyobadilisha sura ya dunia ya Kiislamu, jambo ambalo halikuwahi kutokea katika historia nzima ya Uislamu. *Dar al-Islam* ambayo ilianzishwa na Mtume mwenyewe, leo hii imetoweka kabisa, na haipo hata Makka na Madina.Ukweli ni kuwa dunia ya Kiislamu hivi sasa imerejea, ukiangalia kwa mtazamo wa kiujumla wa kuwapo kwa *Ummah,* kwenye hali ya Uislamu wa *kabla ya hijri*. Dunia ya Kiislamu, kama vile ilivyokuwa kwa sehemu zilizobaki za dunia isiyokuwa ya Kikristo ya bara la Ulaya, leo hii imefungamanishwa katika mfumo mpya wa kidunia ya kisasa na sera za kitaifa za kisiasa zilizojikita kwenye *Shirk.* Kitu ambacho ni kinyume kabisa na mantiki ya kuwapo kwa *Dar-al-Islam*.

Utamaduni wa Kiislamu unaonekana sasa kuingia katika hatua yake ya kihistoria ya baada ya Ukhalifa. Na kama ilivyokuwa Makka miaka elfu moja na mia nne iliyopita, vile

vile leo hii, jumuiya ya Kiislamu inatawaliwa na kuwa chini ya jamii inayokumbatia kila kitu, kila nchi na kila jambo ya ki-*jahiliyah* ambayo inatawala dunia. *Jahiliyah* hiyo, si wengine bali ni jamii ya utamaduni wa kisasa wa *Dajjal* wa baada-ya-Ukristo ya kimagharibi yenye sera zisizomtambua Mungu. Kama alivyo muasisi na mbunifu wake, Dajjal, Mtume wa uongo, huu ni utamaduni ambao (kama mithili) una neno *Kafir* limeandikwa kwenye paji la uso wake kati ya macho mawili.

Hebu sasa tujikumbushe jinsi gani dunia ya Kiislamu ilivyozipokea taarifa za tangazo la Bunge Kuu la Taifa la Uturuki kuwa Khilafah imevunjwa na Mustafa Kamal amekamilisha kubadili Khilafah na mahali pake kuzindua Jamhuri ya Uturuki.

Chuo Kikuu cha Al-Azhar kilitoa tamko la kulaani kitendo cha Waturuku na kukiita kuwa ni *Bid'ah* (ikim. tendo la kuzusha / kubuniwa, ambalo siyo asilia kwenye mafunzo *Sunnah* na maamrisho ya *Qur'ani*) na kusisitiza kuwa Khilafah ni sehemu muhimu ya Uislamu.

Tamko liliambatanishwa na kusisitizwa na nukuu kutoka kwenye Hadithi ya Mtume (*rehma na amani ju yake*) inayohusu umuhimu wa mpangilio wa *Bai'ah*, ikim., kiapo cha utiifu kinachotolewa na watu / waumini ambacho kinathibitisha na kinapelekea kuchaguliwa / kuteuliwa kwa kiongozi wa *Ummah* anayechukuwa nafasi ya uongozi:

"…Yeyote ambaye atatoa au kuondoa mkono wake kutoka kwenye utiifu (ikim.; toka kwa *Amir* ambaye ameteuliwa kwa haki) atakutana na Allah siku ya Qiyama akiwa hana Ushahidi wowote (wa imani); na yeyote atakayekutwa na umauti bila ya *Bai'ah*, hakika atakuwa amekufa kifo cha *Jahiliyah* (ambayo pia inaweza kumaanisha kifo katika zama zilizoshuhudia kurudi kwenye *Jahiliyah* ya *kabla ya Hijri*.)"

(Sahih Muslim)

Tamko liliishia kwa kutoa wito wa kufanyika kwa Mkutano wa Kimataifa wa *Khilafah* ya Kiislamu uliofanyika Kairo ambao ulitoa majibu mahususi kufuatia uamuzi wa Baraza la Juu la Bunge la Uturuki, mnamo mwezi wa Tatu, mwaka 1924, wa kuvunja Utawala wa *Khalifa*.

Mkutano wenyewe ambao ulifanyika in 1926, ulipisha azimio ambalo lilijumuisha usemi huu wa Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) na kuthibitisha umuhimu wa kuwapo kwa taasisi ya Khalifa, na hivyo basi, Mfumo wa Kimaisha wa Jumuiya wa Kiislamu, kwa ajili ya dunia ya Kiislamu.

Changamoto iliyojitokeza leo hii mbele ya *Ummah* ni kuirudisha upya Dar al-Islam (Mfumo wa Kimaisha wa Jumuiya ya Kiislamu) na kitengo cha *Khilafah*. Bila kujali kuwa utafiti wetu wa Eskatolojia ya Kiislamu unaonyesha kuwa Khilafah haiwezi kurudishwa mpaka atakapojitokeza Imam al-Mahdi, bado wajibu wa Waislamu unabaki pale pale katika kujikita kwenye jitihada hizo. Ili *Ummah* huu uweze kufanikisha lengo hilo la kurudisha tena

nguvu na miliki ya Uislamu juu ya Taifa katika dunia ya Kiislamu, ni muhimu kwa Waislamu kujua historia ya kuanguka kwa Ukhalifa na ni kitu gani kilijitokeza kuchukua nafasi yake, kwenye kiini na chimbuko la dini ya Kiislamu, ikiwa ni Taifa la Wahhabi wa Saudi lenye mwelekeo wa kidunia. Pia ni muhimu zaidi kwa Waislamu kuelewa mchango mkubwa na wa kisaliti ambao Ufalme wa Ottomani ulichangia kwenye kuanguka huko ikiwa tunatarajia kushuhudia jitihada zinazoelekezwa kwenye kuufufua mfumo mzima wa Khilafah. Kitabu hiki kina lengo la kuchangia jitihada hizo kwa kuielimisha jamii.

## *Kuanzia kwenye kuvunjwa kwa Khilafah hadi kuvunjwa kwa Hajj*

Somo hili lina umuhimu wa ziada wa kimkakati kwa kuwa adui aliyeuteketeza *Khilafah* hivi sasa ana lengo jipya likiwa ni ibada ya *Hajj*. Ibada hii ya *Hajj* imekuwa ikifanyika bila kusita tangu ilipoanzishwa na Mtume Abraham (*rehma na amani juu yake*) miaka elfu kadhaa iliyopita. *Hajj* iliendelea kufanywa hata wakati ambapo ghuba ya Uarabuni ilikuwa imekamatwa na hulka za kuabudu masanamu. Maadui wa Uislamu hivi sasa wana lengo moja wanalolipa kiupa-umbele cha hali ya juu la kuhakikisha kuwa ibada hiyo inasitishwa.

Abu Said al-Khudri alinukuu Hadithi ya Mtume Muhammad (rehma na amani juu yake) ambamo, yeye, Mtume amesema:

> "Watu wataendelea kufanya ibada ya Hijja na Umrah kwenye Ka'aba hata baada ya kujitokeza kwa Ya'juj na Ma'juj (Gog na Magog)." Shu'ba alinukuu ziada kuwa:
>
> "Saa ya mwisho haitotimia hadi ibada ya Hajj kwenye Ka'aba itakapoachwa."
>
> (Sahih Bukhari)

Uchunguzi wetu wa suala hili umeashiria kuwapo kwa dalili kuwa lengo la kusimamisha ibada ya *Hijja* hivi sasa imo katika uwezo wa maadui wa Uislamu. Kinachotakiwa kufanyika ili lengo hilo litimizwe ni aidha kwa Israeli kuanzisha vita za kivamizi dhidi ya Waarabu na Waislamu au kuvunja *Msikiti wa al-Aqsa* tu. Taifa la Kiyahudi la Israeli linaweza kufanya hilo wakati wowote. Ni kiasi cha wao kujichagulia wakati muafaka. Utawala uliopo wa Saudia umeisaliti dunia ya Waislamu kiasi kufikia kuwa na ushirikiano wa kimkakati na Wazayonisti pamoja na Taifa la Israeli. Vita mpya za kivamizi za Wazayonisti au uvunjaji wa *Msikiti wa al-Aqsa* utaibua wingu la upinzani mkubwa ndani na nje ya Saudia dhidi ya utawala wa taifa hilo. Hawatoweza kudhibiti hasira za Waislamu zitakazojitokeza na kuonyeshwa wazi wakati wa *Hajj*. Na watakapoonekana kuwa hawawezi kudhibiti *Hijja*, ndipo upinzani wa ndani wa Saudi Arabia utaitumia ibada ya *Hajj* kuudhoofisha utawala wa Saudia. Haya ni mojawapo ya mazingira ambayo yanaweza

kujitokeza na kupelekea kwa watawala wa Saudia kusimamisha *Hajj* ili kulinda utawala wao na maslahi yao.

Endapo dunia ya Kiislamu itapoteza ibada ya *Hajj*, baada ya kupoteza utawala wa *Khalifa*, hicho kitakuwa kipigo kingine kikubwa na kitaendelea kurudisha nyuma maendeleo ya Waislamu kuelekea kwenye *Jahiliyah* ya zama za *kabla-ya-Hijri* za Makka. Ni *Imam* mwenye nguvu na jasiri kupita kiasi pekee ndiye atakayeweza kuhimili mtihani huo! Je, tunaweza kufanya nini juu ya hayo? Hatua ya mwanzo kabisa ambayo inabidi ichukuliwe katika kuweka mkakakati wa kukabiliana na hali iliyopo ni ulazima wa kuchunguza kwa makini, kufuatilia na kudodosoa historia ya wakati ule ambamo *Khilafah* ilivunjwa na *Dar al-Islam* vyote viwili kupotezwa. Hiki hasa ndicho tunachojaribu kukifanya japo kwa uchache kwenye kitabu hiki.

# Sura ya Kwanza

## *Diplomasia ya Kiingereza na mashambulizi dhidi ya Khilafah*

> "Ili utamaduni za kimagharibi uweze hatimaye kufanikiwa kuushinda na kuudhibiti Uislamu, na ili uweze kuijumuisha dunia yote ya Kiislamu kwenye mfumo mpya wa kimataifa wenye msimamo na mwelekeo wa kidunia ambao umebuniwa na kuanzishwa na mataifa ya Magharibi, lengo la mkakati linahitaji *Hejaz* iwe chini ya himaya ya wakala wa utamaduni wa ki-Magharibi wa mshikamano wa Kiyahudi-Kikristo ili mabaki ya Taifa la *Khilafah* la Kiislamu ambalo lilianzishwa na kuendelea kuwapo Konstantinopol kwa karne kadhaa, liweze kudhoofishwa na hatimaye kuondolewa kwenye uso wa dunia. Kudhibiti *Hejaz* kunapaswa kuwe kwa kutumia wakala, badala ya udhibiti kwa ukoloni wa kimagharibi wa moja kwa moja kwani *Dajjal* alishajua kuwa Waislamu watakuja juu na kuwa kitu kimoja kupinga hilo na kujaribu kuikomboa Makka na Madina kutoka kwenye himaya ya *Kuffar*. Lakini udhibiti wa himaya chini ya wakala ambao ni sawa na udhibiti wa himaya hiyo moja kwa moja – na Mtume aliyebarikiwa alishapewa onyo kuwa *Dajjal* atafanikiwa kuunda na kushika madaraka yake dhidi ya *Makka* na *Hajj* katika zama za *Akhir al-Zaman*. Mwisho wa yote, je, Mtume (rehma na amani juu yake) hakusema kuwa alioteshwa kuwa amemuona *Dajjal* akifanya ibada ya *Tawaf* kuizunguka Ka'aba?"

Muda wote ambamo Taifa la *Khilafah* litaendelea kuwapo, wakati huo wote litaendelea kuwa ni tishio kwa mataifa na utamaduni wa ki-Magharibi, likiwa kama kiungo na alama muhimu yenye nguvu inayoegemeza msimamo wake kwenye mfumo wa Kijamii wa maisha wa Kiislamu au *Pax Islamica*, na chombo muhimu ambacho wakati wowote kinaweza kuhamasishwa na kuwa jeshi kubwa linaloweza kupigania yale yanayowahusu Waislamu na malengo yao. Daima palikuwa na kiungo baina ya "nguvu" na Taifa la *Khilafah* katika Uislamu!

Allah, mwingi wa nguvu asiye na mwenza, ametuletea dini ya Kiislamu pamoja na Mtume Muhammad (rehma na amani juu yake) ili iweze kuhimilisha ubora wake juu ya wapinzani wote. Hii inahitaji kuwepo kwa kukubalika na usikivu wa *Umma* wa Kiislamu, juu ya ubora huo katika maisha yao yote ya binafsi na ya kijamii.

Kuwapo kwa madaraka na mamlaka ya Khalifa kuliuwezesha Uislamu kuwa na alama ya ubora wa nguvu katika maisha ya kijamii. Kutokuwapo kwa mamlaka hayo, dunia ya Kiislamu haiwezi kuwa na nguvu hizo. Palikuwapo, hata hivyo, kiunganisho muhimu baina ya mamlaka ya Khalifa na uwezo wake wa kudhibiti na kusimamia *Haramain*, ikimaanisha maeneo matakatifu katika miji ya *Hejaz* ya Makka na Madina. *Khalifah* alilazimika kuwa na

mamlaka na kusimamia Hajj ambayo ni moja ya nguzo tano za Uislamu, na kwa kuwa *Hajj* inafanyika *Hejaz*, mantiki inapelekea kuwa Khalifah anapaswa pia kuwa na mamlaka juu ya *Hejaz*. Yeyote atakayefanikiwa kuvunja kiunganisho hicho, angeweza kusababisha kudhoofika kwa Ukhalifa na, hadi mwishowe, kupelekea dunia ya Kiislamu kuwa haina nguvu tena!

Katika miaka yote 1400 ya historia ya Umma wa Mtume Muhammad (rehma na amani juu yake), hakuna mtu hata mmoja ambaye alifaulu kuteuliwa kuwa Khalifa, na kupata uhalali wa uteule wake kupitia *Baiy'ah* ikiwa ni ahadi ya kutii na kufuata amri na utawala wake juu ya Waislamu, bila ya mtu huyo kuwa aidha na nguvu za moja kwa moja za kudhibiti au kuwa na mamlaka ya kudhibiti *Hejaz* kwa ujumla na hususan *Haramain.* Historia pia ina ushahidi ambao unaoweka wazi kiungo kisichotenganika kwenye fahamu na hulka za kisiasa na kidini za *Ummah* baina ya Mamlaka ya *Khalifah*, na utawala juu ya *Haramain*, kwa upande mmoja na mamlaka yake dhidi ya *Hejaz* na *Haramain*, kwa upande wa pili.

Kiunganisho hicho muhimu ambacho hakijawahi kutenganishwa, kilikuwa pia na misingi katika mfumo wa *Shariah* wa Kiislamu kwani tendo la *Hajj* ni moja ya nguzo muhimu ya kutekelezwa kwa kila mmoja anayejishirikisha kwenye *Umma*, na *Hajj* linahitaji kufunga safari kwenda *Hejaz*. Hakuna mtu yeyote ambaye angeweza kutambulika kama kiongozi wa ngazi ya juu kabisa wa Waislamu ambaye asingekuwa na uwezo na mamlaka ya kudhibiti na kusimamia kitendo cha kutayarisha na kusimamia *Hajj*. Na hii, inajumuisha, bila ya shaka yoyote, uhuru na usalama wa mahujaji, hivyo ilihitaji uwezo na nguvu za kiutawala juu ya *Hejaz.* Kutokana na hali hiyo, hata pale ambapo makao makuu ya *Khilafah* yalipokuwa yanahamishwa kutoka Hejaz kwenda Kufa (Iraq), Damascus, Baghdad, Kairo na hata Istanbul, Makhalifa (*Khulafa*) wakati wote walichukua tahadhari na uangalifu wa hali ya juu kuhakikisha kuwa wanaendelea kuwa na mamlaka na nguvu za kudhibiti *Hejaz.*

Hatua kubwa kabisa ya mwanzo iliyochukuliwa katika mkakati wa kuuangusha mfumo wa *Khilafah* ilikuwa ni kuanzisha Taifa la *Khilafah* ambalo liko nje ya dunia ya Kiarabu. Ya pili, ambayo ilikuwa hatua nyepesi kuliko ya mwanzo, ilikuwa ni kukata na kusitisha mamlaka ya hilo Taifa la *Khilafah* juu ya *Haramain* na *Hajj* na hivyo basi kulipa pigo la nguvu lililouvua uhalali wa kuwapo kwake.

Waturuki wa Ottomani walichaguliwa, kwa kujua au kutokujua, kuwa wenyeji wa Taifa hilo la *Khilafah* ambalo lingekuwa, kwa mara ya kwanza kwenye historia ya Uislamu, nje ya dunia ya Kiarabu. Kwa kweli Wazayonisti waliua 'ndege wawili kwa jiwe moja' pale ambapo Taifa hilo la Khilafah lisilokuwa la Kiarabu lilipoanzishwa kwenye mji mkuu wa Konstantinopol. Ushirikiano wa Wazayonisti wa Kiyahudi-Kikristo ulibaki ndani ya kundi la Wakristo wa Ulaya ya magharibi na haukujumuisha wale Wakristo ambao walikuwa wakiitwa kuwa ni *Rum* ambao wanatamkwa kwenye *Qur'an* kuwa na upendo na hisia chanya dhidi ya Waislamu. Ukweli ni kuwa Surah nzima ya *Qur'an* imepewa jina la Wakristo hao, ikim.; *Surah al-Rum*. Konstantinopol ulikuwa ni mji mkuu wa *Rum.*

Waturuki wa ki-Ottomani walikuwa na mamlaka juu ya *Haramain* na *Hajj* mfululizo kwa karne kadhaa hali iliyoendelea hadi Wazayonisti walipofanikiwa kwenye Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia kusitisha mamlaka hayo na hivyo basi kuwapa pigo kubwa liliowavua uhalali wa *Khilafah* ya ki-Ottomani. Hilo lilipelekea si tu kutoweka kwa *Khilafah* ya ki-Ottomani, bali pia kutoweka kabisa kwa Taifa la *Khilafah*.

Kilichobaki kufanyika katika mpango wa Wazayonisti wa kulivunja Taifa la *Khilafah* ya Kiislamu ilikuwa ni kuhakikisha kuwa hapatokei tena Taifa *Khilafah* la Kiislamu kuchukua nafasi ya Taifa la *Khilafah* la wa-Ottomani. Ushirika wa Wahhabi wa Saudia ulijitokeza katika historia na kulibeba hususan jukumu hilo kwa niaba ya Wazayonisti. Hapana atakayejitokeza na kufanikiwa kudai kuundwa kwa *Khilafah* ilhali Wahhabi wa Saudia watendelea kuwa na mamlaka dhidi ya *Haramain* na *Hajj*.

Dajjal Mtume wa uongo pamoja na ushirika wa Wazayonisti walikuwa makini sana kuhakikisha kuwa wanachunguza na kufahamu kiunganisho baina ya *Ukhalifa,* nguvu za Uislamu katika uwanja wa dunia nzima, na mamlaka ya kudhibiti *Haramain,* kisha walipanga mkakakti wao wa kishetani kuudhoofisha Uislamu kuwa hauna nguvu, na kuuacha umejibana kutimiza tu mahitaji ya kiimani ya mtu binafsi mmoja mmoja, bila kuwa tena na uwezo wa kuathiri jamii nzima kwa ujumla. Kwa maneno mengine, walipanga mkakati wao kuufanya Uislamu ufungamane na mfumo wa kidunia na kuwarudisha nyuma Waislamu ili wafuate mfumo wa maisha wa Kiulaya usiomtambua Mungu.

Ili jumuiya ya utamaduni wa ki-Magharibi iweze kufanikiwa katika kuushinda na kuudhibiti Uislamu, na ili iweze kuufungamanisha ulimwengu wa *Kiislamu* katika klabu mpya ya mataifa yenye msimamo na mfumo wa kidunia iliyouanzisha, mkakati ungehitaji kuifanya *Hejaz* nayo iwe na athari za ki-Magharibi na kutawaliwa na wakala wa utamaduni wa Kikristo-Kiyahudi. Mamlaka yangelazimika kuwa chini ya wakala badala ya utawala wa moja kwa moja wa kikoloni wa ki-Magharibi juu ya *Hejaz*, kwani *Dajjal* alijua kuwa Waislamu wangekuja juu na kujiunga kuwa kitu kimoja katika kupigania kuikomboa Makkah na Madina kutoka kwenye mamlaka ya *Kuffar*. Lakini mamlaka kupitia wakala ni sawa kabisa na mamlaka ya moja kwa moja- na utabiri wa Mtume uliashiria kuwa yeye (*Dajjal*) atafanikiwa kushika mamlaka juu ya Makkah na Hajj katika *Akhir al-Zaman*. Mwisho wa yote, Mtume (rehma na amani juu yake) hakusema kuwa alitokewa na maono ambamo alimuona *Dajjal* akifanya ibada ya *Tawaf* kuizunguka *Ka'aba?*

Waingereza, walipogundua umuhimu wa *Hejaz* na *Haramain* kama kiungo muhimu katika kujenga nguvu, kuhalalisha na hata kuweka misingi ya kuokoa uhai wa *Khilafah* wa Ottoman, waliongeza jitihada zao wakati wa Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia ili kuiondoa *Hejaz* kutoka katika himaya ya Khalifa wa Ottoman. Hii iliwezekana pale ambapo *Sharif* Husain, ambaye alikuwa ni Sharif wa Makka aliyeteuliwa na utawala wa Khalifa wa Ottoman, ambaye ni baba wa babu wa aliyekuwa mfalme Husain wa Jordan (ambaye naye alirithiwa na mwanawe Abdullah), alishawishiwa na Waingereza kumkana Khalifa wa

Ottoman na badala yake aliwakubalia kujiteua yeye mwenyewe kuwa na mamlaka juu ya *Hejaz* chini ya uangalizi, kinga na ushirikiano na Waingereza.

Hadi mwaka 1916, katikati ya Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia, Khalifa wa Ottoman alikwishapoteza mamlaka na uwezo wa kudhibiti Makka na Jeddah, hiyo miji ikiwa ni sehemu ya *Hejaz*. Mamlaka yake kwa mji wa Madina yaliweza kudumu kwa kipindi chote cha vita hiyo na yalikoma mwishoni mwa mwaka 1919 wakati ambapo baadhi ya askari wa ki-Ottoman waliposhauriwa kumkana kiongozi wao shujaa, Fakhri Pasha[1]**.** Baada ya *Khalifa* wa Ottoman kupoteza mamlaka yake juu ya *Hejaz*, nguvu za *Khalifa* zilikuwa zimepungua kwa kiasi kikubwa sana na utawala huo uliokuwa Konstantinopol uliweza kujikokota kwa shida kwa miaka kadhaa na hatimaye ulianguka na kutoweka moja kwa moja. Huu kwa kweli ulikuwa ni ushindi mkubwa kwa diplomasia ya Kiingereza. Kudhoofishwa kwa Ukhalifa kuliathiri mfumo mzima wa Ufalme wa Kiislamu wa Ottoman.

Nao ulianguka na kutoweka. Mnano mwaka 1919, pale majeshi ya Kiingereza, chini ya uongozi wa Jenerali Allenby, yalipouteka mji wa Jerusalem. Ni muhimu kuelezea kuwa Jenerali Allenby, alipokuwa anaingia katika Mji huo Mtakatifu, alitangaza kuwa "*hatimaye sasa kampeni za krusedi zimekwisha*". Ikiwa kama palikuwa na wasiwasi au shaka yoyote juu ya ukweli kuwa hatari kubwa kwa Uislamu ilikuwa inaletwa na kusababishwa na diplomasia ya Waingereza katika Ghuba ya Kiarabu, basi maneno hayo ya Allenby yanapashwa kuuondoa na kuufuta kabisa wasiwasi huo!

Alichokuwa akimaanisha Allenby ni kuwa Uislamu sasa umebaki kama vile mithili ya chui asiyekuwa na meno wala makucha. Hatma yake (Uislamu) ni kubaki daima bila ya nguvu wala uwezo, na hivyo kutoweza kujibu mashambulizi baada ya kunyang'anywa na kupoteza Jerusalem kama vile ambavyo Salahuddin Ayyubi (Saladin) alivyoweza kujibu mashambulizi wakati Jerusalem ilipochukuliwa na wapiganaji wa kampeni za krusedi.

Waarabu walikuwa miongoni mwa wapiganaji wa Allenby walioinyang'anya Jerusalem kutoka kwenye mikono na utawala wa Khalifa wa Ottoman. Waarabu hao walikuwa sasa wanasubiri kushambulia mzoga ulioachwa na Waingereza baada ya ushindi wao hapo Istanbul. Walitamani utawala wao wenyewe wa ndani juu ya *Hejaz*, chini ya Khalifah mwenye asili ya kiarabu, lakini ilikuwa muhimu kusubiri ili kuona kama Khalifa wa Ottoman angeweza kukusanya nguvu za kutosha ili kuweza kujaribu kurudisha madaraka yake katika kudhibiti *Hejaz*.

[1]Elie Kedourie, katika sura yenye kichwa cha habari "Kuanguka kwa mji wa Madina – Januari 1919" (Uislamu katika Dunia ya Kisasa, Holt Rinehart na Winston, NY. 1980 ukurasa wa 277 – 296) anajenga picha halisi kwa maelezo na uchambuzi mahiri wa jinsi kamanda wa jeshi la ki-Ottomani, Fakhri Pasha, alivyokuwa akipigana kishujaa kuulinda mji wa Madina hadi mwezi januari 1919 pale aliposalitiwa na baadhi ya wanajeshi wake.

Hadi ilipofika tarehe 3 ya Mwezi wa Tatu mnamo mwaka 1924, Ukhalifa wa Ottoman ulipofutwa, ikawa wazi kuwa hakuna hatari yoyote iliyokuwa ikiwakabili kutoka kwa Ufalme huo. Muda huo huo ndipo wasaliti walioshirikiana na Waingereza walipoanza kupigania mzoga ulioachwa baada ya wao kuusaliti utawala wa Khalifa wa Ottoman.

Mnamo tarehe 7, Mwezi wa Tatu, 1924, *Sharif* al-Husein akawahi na kujitangaza yeye mwenyewe kuwa yeye ni Khalifa. Sifa kubwa na muhimu kuliko zote alizozitaja ni kuwa yeye ni mwenye mamlaka na madaraka juu ya *Hejaz*. Pia alijisifu kuwa yeye ni *Hashimite*, ikimaanisha kuwa anatoka katika mlolongo wa uzawa wa kabila lile lile la *Banu Hashim*, ambalo ni moja ya kabila la ki-Quraish ambalo ndilo kabila la Mtume Muhammad (rehma na amani juu yake). Kwa hakika hili lilitia uzito sana katika hoja zake miongoni mwa wasomi (*Ulama*) kiasi kwamba *Kadhi Mkuu* wa Transjordan mara moja alikubali hoja hizo na kupitisha na kumtambua Husain kama Khalifa.

Huo wasifa wake mwingine, ambao ulikuwa unatiliwa mashaka kuwa na dosari miongoni mwa jumuiya za Waislamu, lakini wasifa ambao ulichukua na kupewa nafasi na uzito mkubwa kwenye mustakabali wa nguvu-na-siasa za wakati ule katika Ghuba ya Arabia, ulihusishwa na ukweli kuwa *Sharif* alikuwa ni rafiki na mshirika wa Uingereza, taifa ambalo wakati huo lilikuwa na nguvu za dola kubwa kuliko taifa lolote duniani (*super power*) na alikuwa amepewa kiasi kikubwa cha pesa, ikiwemo pia msaada wa kidiplomasia na kijeshi baada ya kufuzu kuupinga na kuukana uongozi wa Khalifa wa Ottoman na madaraka yake juu ya *Hejaz*.

Katika kuchukua madaraka na kujitaja yeye mwenyewe kuwa ni Khalifa *Sharif* Husain alifanya kosa kubwa mno lisilosameheka la kutokuomba kibali cha kujitangaza kuwa Khalifa kutoka kwa Waingereza ili kufanya hivyo. Hicho ndicho kiini cha, na hadhi inayokuwapo pale pote penye mawiano aina ya nchi-Mteja, uhusiano ambamo uhuru wa nchi-Mteja unaathirika kwa kubanwa. *Sharif* Husain akawa amevunja kanuni ya kimsingi ya uhusiano uliopo wa nchi-Mteja. Je, Waingereza wangechukua hatua gani?

Diplomasia ya Waingereza katika Ghuba ya Arabia (*Jaziratul Arab*) ilikuwa ikiendeshwa katika mielekeo tofauti kadhaa lakini yote ilikuwa ikijumuishwa. Mwanzoni palikuwa, kabla ya yote, na lengo la kuyaondoa madaraka na udhibiti wa Khalifa aliyekuwa Konstantinopol wa maeneo ya *Haramain*. Hili lilikuwa na lengo la kudhoofisha utawala wake, uhalali wa kuwapo kwa Khalifa, na hivyo kudhoofisha nguvu na upeo wa uwezo wake wa kudhibiti dunia ya Kiislamu, na mwishowe kuwezesha kuushinda utawala na Ufalme wa Ottoman kwenye Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia. Pili, Waingereza walihitaji kuwa na mtawala aliye rafiki na mshirika wao (na ndivyo ulivyokuwa utawala wa wa-Ottomani takriban kwa kipindi chote cha utawala huo) awe ndiyo mtawala mwenye madaraka juu ya *Hejaz* ili iwawezeshe kuwa na uwezo mkubwa zaidi na nafasi ya kusimamia na kuongoza matukio na siasa za Ghuba ya Arabia yaende vile wanavyotaka wao kwa maslahi yao. Mwishowe, siasa za Ghuba na kuanguka kwa utawala wa wa-Ottoman kuliungana na mkakati wa Waingereza wakishirikiana na Wazayonisti katika jitihada za kishetani za kuikomboa

Palestina na kuliwezesha Taifa la Kiyahudi kuibuka. Mielekeo hiyo ya diplomasia ya Kiingereza hatimaye iliwekwa wazi kwa kufikiwa Mkataba wa kidhalimu wa Sykes-Picot wa mwaka 1916 na Azimio la Balfour la mwaka 1917.

Taifa lililokuwa na nguvu za dola kuliko mataifa yote kwa wakati huo (*super power – Taifa Tawala*) na wale waliojulikana kama '*taifa teule*' wakawa wamefungamana kwa mkataba ambao ungesababisha mabadiliko makubwa kwao kama wahusika wakuu na athari zake kuifikia hata jamii yote ya dunia nzima ya binaadamu.

Lengo la diplomasia hiyo ilikuwa ni kuuvunja mfumo mzima wa Maadili na Mwenendo wa Jamii wa Kiislamu na hivyo kuvunja nguvu za dini ya Kiislamu isiweze kuzuia harakati za Wazayonisti watimize lengo lao. Vyombo shirikishi vya Kiislamu katika kusimamia mfumo huo wa Kiislamu vikiwemo *Ahl al-Dhimmah* na *al-Jizyah*[2] tayari vilikwishakuwa vimefutwa ndani ya Utawala wa Ufalme wa Ottomani mnamo mwaka 1855 ikiwa ni matokeo ya shinikizo la wazungu ki-Zayonisti wa Ulaya. Ikiwa mamlaka ya *Khalifah* yataendelea kuwapo, hata kwa kusuasua, basi bado pangekuwa na uwezekano kuwa mfumo huo wa Maadili na Mwenendo wa Kiislamu ungeweza kuibuliwa upya.

Hivyo mashambulizi ya kuutokomeza Ukhalifa yalikuwa ni muhimu sana ikiwa jumuiya ya ushirikiano wa wazungu waUlaya-Wayahudi ungetaka kutimiza lengo lao.

Pia ilikuwa wazi kwa Waingereza na Wazayonisti kuwa Makazi ya Taifa la Wayahudi, ikimaanisha Taifa la Wayahudi la Israel, haliwezi kuundwa ndani ya Palestina yenye itikadi na msimamo wenye kufuata dini ya Kiislamu. Taifa hilo la Wayahudi lisingeweza kudumu kwa muda mrefu kwani dunia ya Kiislamu na *Khalifah* wangeweza kukusanya nguvu za rasilimali mbalimbali, ikiwemo juhudi za mshikamano wa kidini na bila kusahau nguvu za kijeshi kupinga kuwapo kwa taifa hilo. Hivyo kumiliki *Hejaz*, ambako kulikuwa muhimu sana kwenye siasa za ghuba, kulikuwa ni jambo mojawapo ambalo diplomasia ya Kiingereza ilielekeza nguvu zake nyingi na kuipa kiupambele cha hali ya juu kabisa.

Hata hivyo madai ya *Ukhalifa* ya Sharif al-Husain, akiwa ni *Hashimite*, hayakuwa na muelekeo mzuri na salama kwa malengo na makusudio yalipangwa na diplomasiya ya Kiingereza kwa kuwa wakati wote pangekuwa na uwezekano wa kuyarudia madai ya kuwapo kwa *Khalifah*. Sharif al Husain angeweza kuuhamasisha umma wa Kiislamu kufikia kiwango cha kutaka kuwapo upya kwa Mfumo wa Maisha wa Jumuiya ya Kiislamu na *Pax Islamica*

---

[2]*Ahl al-Dhimmah* – ni watu wasiokuwa Waislamu ambao wanakuwa chini ya uangalizi wa Waislamu na wanaruhusiwa kuishi ndani ya *Dar al-Islam*. *Jizyah* ni kodi ya adhabu ambayo imeamrishwa ndani ya *Qur'an* dhidi ya watu ambao wameshindwa vita ya Jihad na ambao wangependa kuendelea kuishi kwenye ardhi yao waliyokuwa wakiishi kabla ya kutekwa. Malipo ya kodi hii yana lengo la kuonyesha utii wao dhidi ya utawala wa Kiislamu katika eneo hilo.

katika sehemu muhimu ambayo ni chimbuko la Uislamu yenye sifa za pekee katika jumuiya ya Kiislamu, na hivyo kuwa ni tishio kwa athari zilizokusudiwa na utawala wa Kiingereza katika mpango wake wa kutawala na kumudu sehemu kubwa za *Dar al-Islam*. Msisimko mpya wa dunia ya Kiislamu pia ungepelekea kushindwa kwa jitihada za Wayahudi kudhibiti Palestina ikiwemo udhibiti wa mji wa Jerusalem. Taifa la Israeli halitoweza kuundwa.

Hivyo basi, Uingereza ilitoa idhini na kumbariki mteja mwingine wa Waingereza katika ghuba, Abd al-Aziz Ibn Saud, kumpinga Husain na kumnyang'anya utawala wa *Hejaz.* Huu ulikuwa ni uthibitisho wa kufikiwa kwa kilele cha ustadi wa sanaa za usaliti na unafiki. Mteja mmoja alitumika kuhakikisha kuwa anamuondoa mteja mwingine. Mwisho kama huo, sasa hivi ukawa unawasubiri Husain na wa-Ottomani. Somo liko wazi, nalo ni kuwa *Dajjal* anawatumia wateja hadi inapofikia wakati ambapo hawahitaji tena, ndipo anapowatupilia mbali na kuweka mteja mpya kwenye nafasi yake (Hii ni sawa na upako wa maraisi wa Amerika, bila kujali kama anatokea chama cha Democrat au cha Republican – ambao japo wanapokezana madaraka baada ya chaguzi, wote wanamtumikia *Dajjal* kwa utiifu mkubwa. Na yeyote anayethubutu kujitoa nje ya mstari wa utiifu huo, anauawa na Shirika la Kijasusi la Israeli- Mossad).

Uingereza iliustawisha urafiki na muungano na Ibn Saud wakati wa vita na, kama kawaida, ilitumia diplomasiya ya kipesa (ikimaanisha, rushwa). Ibn Saud alikuwa akipewa jumla ya paundi za Kiingereza 5000 (elfu tano) kila mwezi kutoka Wizara ya Fedha ya Uingereza ikiwa kama malipo ya kukubali kwake kutojihusisha kwa namna yoyote ile; ikiwa aidha kwa kukubali au kupinga kuasi kwa Husain dhidi ya *Khalifah*, kulazimishwa kwa utawala wa Hashimite juu ya *Hejaz*, ikiwemo jitihada za kidiplomasiya na za kijeshi za Waingereza katika Ghuba zilizokuwa znaelekezwa dhidi ya Utawala wa Kiislamu wa Ottomani. Ukweli ni kuwa alikuwa mteja wa Uingereza. Naye, Ibn Saud, aliutetea utovu huu wa hali ya juu kabisa wa amri ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake kwa kujieleza kuwa alichokuwa akipokea ni *Jizyah*[3]. (Qur'an 5:51)

Hata hivyo diplomasiya ya Kiingereza dhidi ya Ibn Saud ilikuwa na malengo yenye masafa marefu na mbinu zilizo muhimu zaidi ya kupata kutokufungamana kwake na upande wowote katika vita, ikiwamo jitihada za kumg'oa mtovu *Sharif* Husain. Ibn Saud alikuwa na uwezo mkubwa zaidi wa ziada ambao sasa Uingereza ilijipanga kuanza kuunyonya, baada ya Sharif Husain kuweka wazi madai ya kuchukua *Ukhalifa*.

Nguvu za Saudi katika *Najd*, zilizojitokeza upya baada ya kutekwa kwa *Riyadh* mnamo mwaka 1902, zilikuwa ni matokeo ya muungano wa zamani baina ya chifu wa kikabila na kiongozi wa kidini mwenye msimamo na ushupavu mkali wa kidini wa madhehebu ya *ki-Wahhabi*, ambao ungeweza kuitwa kuwa ni Waislamu Waprotestanti. Muungano huu ulihakikisha kuwa wakati wote wazawa wa chifu wa kabila watakuwa na nguvu na mamlaka ya kiutawala wa kisiasa katika eneo linalotawaliwa na muungano huo, masuala yanayohusiana na dini yatakuwa chini ya utawala na uamuzi wa wazawa wa kiongozi wa kidini. Kuwapo kwa hali hiyo, kulipelekea kuwa Wasaudia wa *Najd* walijikuta

wakiwa chini ya shinikizo lililotokana na *Wahhabi* kutaka kulazimisha kukubalika kwa mtazamo wao wa kidini kuwa ndio mtazamo wa imani ya kweli katika maeneo ya chimbuko la Uislamu ya *Hejaz*.

Waingereza, kwa furaha na shangwe, walitoa idhini kwa Ibn Saud mteja wao wa kwanza, kupeleka majeshi yake dhidi ya *Sharif* Husain, mteja wao wa pili, siku nne tu baada ya *Hashemite* kudai kuuchukua Utawala na kujitangaza kuwa yeye ni *Khalifah*. Ibn Saud alikuwa na pupa katika kutaka kumkabili Husain kwa kuwa, japo itaonekana kuwa haiyumkiniki, bali ni kuwa uwezo wa Wayahudi kudhibiti Jerusalem na pia uwezo wa *Wahhabi* kudhibiti *Hejaz*, kote kulikuwa kunakabiliwa na tishio lile lile, lililo sawa na la aina moja. *Yote hayo yasingewezekana kufanikiwa na pia yasingeweza kuendelea kudumu, kama Umma wa Kiislamu ungekuwa na Khalifah*.

Katika kumuunga mkono Ibn Saud, Waingereza sasa wameweza kuhakikisha kuwa kwa kadiri ambavyo *Wahhabi* wa Saudia wangekuwa watawala wa *Hejaz*, *Ukhalifa* hautoweza kurudishwa. Waingereza pia walichukulia pima ya kiakili kuwa kutokuwapo kwa *Ukhalifa*, Mfumo wa Jumuiya wa Kiislamu hautoweza kuokoka na kudumu na hivyo Umma wa Kiislamu utadhoofika kiasi cha kutoweza tena kuhamasika na kujumuika kupinga kuzaliwa kwa Taifa la Israeli. Waingereza pia walijua kuwa *Wahhabi* wenyewe, pia wasingeweza kudai kuwa *Makhalifa* kwa kuwa *Khalifa* wa *ki-Wahhabi* siku zote asingekubalika kwa wengi miongoni mwa Jumuiya ya Waislamu duniani kote.

Hivyo basi, kwa kutomuunga mkono Husain na hapo hapo kwa kumuunga mkono Ibn Saud, Uingereza ilikuwa ikifuatilia na kutimiza malengo yake ya daima ya kushambulia Mfumo wa Jumuiya ya Kiislamu.

Baada ya miezi michache Ibn Saud aliweza kuiteka Makkah, na Husain alikimbilia Jeddah. Waingereza hatimaye waliingilia kati na kumtoa kutoka katika eneo la Ghuba kwa kumpa pendekezo la maisha ya kifahari uhamishoni nchini Cyprus. Punde tu, baada ya hapo, Madina na Jeddah zote zikawa chini ya utawala wa *Wahhabi* wa Saudia.

Zaidi ya karne moja kabla, hata hivyo, muungano wa Wahhabi wa Saudia ulifanikiwa kuyashinda majeshi ya ulinzi ya Taif na Makkah na palitokea umwagaji wa damu wa kiwango cha kutisha. *Wahhabi*, katika msukumo wao wa msimamo wa siasa zenye mtazamo mkali, waliwachukulia Waislamu waishio katika eneo la *Hejaz* kuwa ni *Mushriqoon*

---

[3] "Enyi mlio amini (hii Qur'ani)! Msiwafanye (wale) Mayahudi na (wale) Wakristo kuwa ni marafiki zenu na washirika wenu (wale) ambao ni marafiki na washirika wao kwa wao (baina yao – msiingie kwenye urafiki na ushirika na ushirika wa Wazayonisti wa Kiyahudi-Kikristo). Na miongoni mwenu mwenye kufanya urafiki nao, basi huyo ni katika wao (umeupoteza Uislamu wako). Hakika Mwenyezi Mungu hawaongoi watu wenye kudhulumu." (Qur'ani, al-Maidah, 5:51)

[4] Toynbee Ed., Mtazamo wa kiuchunguzi wa Matukio ya Kimataifa, 1925

(ikimaanisha, watu wenye kosa la kufanya na kutenda kufuru) na, hivyo basi kudiriki kufikia uamuzi wa kuhalalisha mauaji yao kwa kiwango ambacho hakijawahi kutokea kabla katika historia ya Uislamu. Hivi tunavyoandika haya, wapiganaji wa Dajjal wameibuka tena Libya na wanafanya hayo hayo na pia wanarudia yote hayo huko Syria. Itikadi ile ile ya kidini inatumiwa kwa kuua watu wasiokuwa na hatia ndani ya Libya na Syria katika jitihada zao ka kuzipigania nchi hizo na kumkabidhi Dajjal. Inaonyesha Pakistani na Algeria zinasubiri kukumbwa na hali kama hiyo.

Wakati wa umwagaji damu huo wa kutisha uliofanywa na Wahhabi, *Khalifah*, wakati huo akiwa katika makao yake makuu katika mji wa Konstantinopol, Uturuki, alimtaka Mamluke Khedive wa Egipt, Muhammad Ali, kutuma jeshi kwenda *Hejaz* chini ya uongozi wa mwanawe Ismail. Wapiganaji wa *Dajjal* wa *Wahhabi wa Saudia* walisambaratishwa na kuondolewa kutoka *Hejaz* na kukimbilia jangwani. Karne moja baadaye, pamoja na hayo, pakawa hakuna *Khalifah* na jamii zote za Kiislamu zilizokuwa na nguvu na uwezo zilikuwa chini ya utawala wa kikoloni wa jumuiya za kimagharibi. Zaidi, Ibn Saud alijihakikishia ulinzi wa kirafiki wa Uingereza, wakati huo ikiwa ni dola isiyokuwa na mpinzani duniani, *super power*. Hali hiyo ilipelekea kutokuwapo kwa uwezekano wa aina yoyote ile wa kuweza kuyaondoa majeshi ya *Wahhabi wa Saudia* kutoka *Haramain* na *Hejaz*.

Japokuwa *Hejaz* ilikuwa tayari chini ya utawala wa Ibn Saud, lakini bado alikutwa na matatizo na misukosuko mwanzoni mwa utawala wake mnamo mwka 1924. Ilimbidi atayarishe mbinu maalum ambazo zingehakikisha kuwa hayatokei tena majanga kama yale yaliyoutokea utawala wa *Hejaz* wa awali wa *Wahhabi*. Inaonekana kuwa kwanza alifikiria sera za kuwajumuisha Waislamu wa madhehebu zisizokuwa za *ki-Wahhabi* na kutumia utawala wake wa *Hejaz* kupigania umoja wa *Ummah*. Hivyo muda mfupi tu baada ya kutwaa madaraka ya kutawala Makkah na kupokea kutoka kwa wakazi wake kutambulika kwake kuwa yeye ni *Sultani* wa *Hejaz*, alitoa tamko kwa jumuiya ya Waislamu wote wa dunia nzima, ndani yake akiwakilisha ujumbe kuwa *Hejaz*, pamoja na *Haramain* yake, ni mali ya jumuiya ya Waislamu wote duniani na kuwa yeye, Ibn Saud, ana madaraka juu ya Hejaz akiwa tu kama muwakilishi, na kwa niaba ya jumuiya yote ya Waislamu wote duniani[4]. Aliendelea kutamka kuwa anaukaribisha ulimwengu wote wa Waislamu kutuma wawakilishi wao kwenda Makkah ili, kwa mujibu wa maadili ya *Shura* (majadiliano) na *Ijma* (muafaka), wawakilishi wa kiutawala ulio wa haki na usawa, wenye ufanisi bora wangeweza kupatikana na kuweza kuwa na mamlaka juu ya *Hejaz*.

Tangazo hili muhimu lilikuwa thabiti na lilifuata na kutimiza misingi yote ya mahitaji ya Mfumo wa Jumuiya ya Kiislamu. *Hejaz* bado ilikuwa *Dar al-Islam* ambayo ilikuwa imejengwa na Mtume Muhammad (rehma na amani juu yake). Na hadi hapo bado hapakuwa na dalili yoyote kuwa Taifa la Saudia lingetangaza madai ya kumiliki "eneo huru" la *Hejaz*. Haki za Waislamu ndani ya eneo la *Dar al-Islam* zilikuwa zikitambuliwa na kuheshimiwa wazi bila kuficha wala kubagua baina ya Waislamu wote.

Lakini kwa bahati mbaya matamshi hayo ya hali ya *Hejaz*, yaliyotilia maanani na kuujali umoja katika *Ummah* wa Waislamu duniani kote haukuambatana kamwe na vitendo halisi vya Wahhabi wa Saudi vilivyoelekezwa kwa *Hejaz*.

Kwa ufupi kilichotokea ni '*siasa za kujifaidisha'* na zilielekezwa katika kuwalinda Wahhabi wa Saudi haswa baada ya kujitokeza mkakati maalum uliosimamiwa na Chuo Kikuu cha *Al-Azhar* cha Kairo mara tu baada ya kuangushwKhalifa wa Ottomani.

Ni kweli kabisa kuwa mkakati huo ulikuwa unahatarisha mamlaka ya Ibn Saud na utawala wa *Wahhabi wa Saudia* kusimamia *Hejaz*. Zaidi, mkakati huo ulikuwa unachachua

mchuzi wa ushindi uliokwishapikwa na Waingereza na Wayazayonisti. *Al-Azhar* ilipendekeza kuitishwa mjini Kairo kwa Kongamano la Kiislamu la Kimataifa la Ukhalifa (*Mu'tamar al-Khilafah*) ambamo miongoni mwao, pangefanywa jitihada za kuchagua Khalifa mpya mtawala wa *Ummah* wa Kiislamu wa dunia nzima.

Laiti kama *Wahhabi* wangekuwa wana nia njema isiyo na dosari ya kuupigania Uislamu, basi wangeukaribisha na kuupokea kwa mikono miwili mwito huu wa *Al-Azhar* uliolenga kutimiza tendo muhimu linaloenda sambamba na matakwa ya *Shariah*, ikimaanisha kuteuliwa kwa Khalifa mahsusi atakayekubalika na kutambulika na *Ummah* wote wa Waislamu kote duniani. Ikumbukwe kuwa Wahhabi kwa kipindi kirefu kilichotangulia hapo walidai kuwa *Ukhalifa* baada ya *Rashiduun* haukuwa halali kwa kuwa, miongoni mwao, *Ukhalifa* haukusimamishwa na kujengwa kufuatana na kanuni na misingi ya *Shariah*. Ikiwa *Ukhalifa* usiokuwa rasmi umeshatoweka, na Chuo kinachoongoza cha elimu za Kiislamu kinaitisha kongamano ili kujadili suala la *Ukhalifa* kukiwa na lengo la kufanya uchaguzi wa *Khalifah* mpya, *Wahhabi* walipaswa si tu waukubali mwaliko, bali pia walipaswa watoe kila aina ya ushirikiano unaowezekana na walipaswa kuwapo kwenye kongamano hilo na kuhakikisha kuwa *Khalifa* anachaguliwa kwa kufuatwa misingi ya *Shariah* kama walivyokuwa wakidai.

Lakini *Wahhabi* hawakuwa na nia njema ya kupigania Uislamu. Msimamo wao ulikuwa ni ule wenye kuonyesha kuchagua nini kinawafaa kwenye masuala ya kidini, kujali kufaidika binafsi, kujipendekeza na kutokuwa na muono wa mbali. *Kwa kweli Ushahidi wa hili uko wazi kabisa kwani kwa takriban miaka 100 tangu kuangushwa kwa Khilafah ya Ottomani mwaka 1924 na kuwapo kwa mamlaka ya Wahhabi juu ya Makkah mnamo mwaka huo huo, Wahhabi / Wa-Salafi hawajafanya jitihada zozote kuurudisha utawala wa Khilafah wa Kiislamu katika Hejaz.* Mwandishi huyu anahofu kuwa muda pekee watakaofanya hivyo, itakuwa pale ambapo *Dajjal* atakapohitaji kibaraka wa ufufuaji wa Khilafah ya Kiislamu au madai ya kurudisha Khilafah ili Wazayonisti waweze kuichukua fursa hiyo kama *causus bellum* kuhalalisha vita kubwa watakazozianzisha dhidi ya Waarabu.

[4] Toynbee Ed., Mtazamo wa kiuchunguzi wa Matukio ya Kimataifa, 1925

*Wahhabi* walijua fika kuwa Waislamu wasingekubali kumchagua *Khalifa* kutoka kwenye madhehebu yao ya ki-*Wahhabi*, na hivyo basi, wakaona ni afadhali wakatae kata kata kuwapo kwa chombo muhimu sana, ambacho ndicho chenye umuhimu wa mwanzo katika Mfumo mzima wa Jumuiya ya Kiislamu. Walikusanya na kutumia nguvu zao zote za hali na mali kuhakikisha kuwa Kongamano la *Khilafah* la Kairo halifanikiwi. Miongoni mwa mikakati yao ilikuwa kutayarisha kongamano pinzani mjini Makkah wakati wa ibada ya *Hajj* mnamo mwaka 1926. Hii ilimaanisha kuwa kongamano la Makkah lingefanyika mwezi mmoja tu baada ya lile la Kairo, hivyo kupelekea kuwapo kwa ugumu kwa washiriki kuweza kuhudhuria makongamano yote mawili. Kwa kuwa Kongamano la Makkah lilipangwa kufanyika wakati wa ibada ya *Hajj*, na kwa kuwa lilipata kuungwa mkono kwa hali na mali na Waingereza, lilikuwa limejiwekea nafasi nzuri ya kuweza kufanikiwa ukilinganisha na lile la Kairo.

Pili, *Wahhabi* waliliondoa kabisa kutoka kwenye ajenda ya Kongamano la Makkah suala na mjadala wowote unaohusiana na *Ukhalifa*. Jaribio hili lililo wazi la kuliwekea upinzani Kongamano la Kairo na kuufuta mjadala juu ya, na uchaguzi wa *Khalifah* liliuweka wazi ushahidi wa nia batili na wadhifa dhaifu wa *Wahhabi* kujidai kuwa ni mabingwa, wafuatiliaji na watekelezaji wa *Shariah* na Uislamu.

Majibu ya jumuiya ya Kiislamu dhidi ya upinzani huu, ikimaanisha Kongamano la Kairo la Mwezi wa Tano / Sita mwaka 1926 na Kongamano la Kimataifa la Kiislamu la Makkah la Mwezi wa Saba 1926, ni somo linalohitaji uchunguzi zaidi na wa kina. Ni kiasi gani kwa mfano, diplomasiya ya Kiingereza ilijikita na kuhakikisha kuwa, kwa mfano, kwanini ujumbe wa Jumuiya muhimu ya Kiislamu ya India ambayo ilikuwa ikiuunga mkono kwa jitihada zote *Ukhalifa wa Ottomani*, ambayo ilianziasha Shirikisho la Kugombea Kuufufua *Ukhalifa* lililokuwa na nguvu kubwa za kijamii, halikuhudhuria kwenye Kongamano la Kairo na, badala yake likahudhuria Kongamano la Makkah, ambako ajenda ya *Ukhalifa* haikuwamo kabisa kwenye mpangilio wa majadiliano? Uchunguzi mdogo sana umefanywa kwenye somo hili.

Kilichokuwa wazi, pamoja na yote, ni kuwa katika upinzani wa Makongamano uliojitokeza, Kongamano la Makkah lilipata ushindi wa kimbinu dhidi ya Kongamano la Kairo, ushindi ambao ulipelekea kuwapo kwa hali ambayo iliathiri kudumu kwa *Ukhalifa* na kuwapo na kufuatwa kwa kwa misingi mahsusi na halali ya Mfumo wa Jumuiya ya Kiislamu (ikimaanisha, *Dar al-Islam*). Wale ambao walitayarisha Kongamano la Kairo walikuwa na lengo la kutaka kuoanisha misingi ya Mfumo huo wa Kiislamu kwa kuwapo kwa chombo muhimu cha utaratibu mzima wa utawala wa kisiasa wa Kiislamu. Lakini hawakuweza kujenga hoja iliyokuwa wazi na nyepesi ya Mfumo wa Jumuiya ya Kiislamu (ikimaanisha, *Dar al-Islam*) ikiwemo Mfumo wa Kiislamu wa Utaratibu wa Uhusiano wa Kimataifa iliyoweza kukubalika na kuuhamasisha *Ummah* wa Kiislamu uliokwisha kata tamaa.

Wale waliotayarisha Kongamano la Makkah kwa upande wa pili, hawakutaka, kwa sababu zao za kibinafsi, kubaki waadilifu kufuata misingi ya Mfumo wa Jumuiya ya

Kiislamu ikiwamo kuwa na Khalifa (ikimaanisha, *Dar al-Islam*) n.k. Badala yake waliamua kuchagua kufuata mfumo wenza wa kisasa wa kisiasa wa utamaduni wa mataifa ya kimagharibi ambao ulikwishajipenyeza na kuingia kwenye utawala wa *Khalifah wa Ottomani*, huu ukiwa ni mfumo wa Serikali za kitaifa. Walifanya hivyo kwa kuwa hiyo ndiyo ilikuwa namna pekee ambayo ingewawezesha Wahhabi wa Saudi kuendeleza jitihada za kuweza kutambulika kama watawala halali wa *Hejaz* na hivyo kujihakikishia kudumu kwa Taifa la Saudia. Walifanya jitihada kubwa katika kuficha mbinu zao na kutenda vitendo vya wazi vilivyokuwa na lengo la kuighilibu Jumuiya ya Waislamu. Ushindi wao katika mchezo huu ulidhihirika wazi kwa namna, malengo na mwenendo wa Kongamano la Makkah.

Ushindi huu wa kimbinu wa Kongamano la Makkah dhidi ya Kongamano la Kairo lilikuwa na athari kubwa sana katika kupelekea kufungua njia kwa jumuiya zilizobaki za Kiislamu, ikiwamo nchi zilizo kwenye chimbuko asili la Uislamu, hatimaye kufuata mfano wa Mustafa Kamal na mfumo wake mpya wa Taifa la Uturuki lenye kufuata mfumo wa kidunia. Historia ya Ulimwengu wa Kiislamu kuanzia mwaka 1924 imekuwa ikishuhudia, kwa upande mmoja, mabaya ambayo yamekuwa wakati wote yakichomekezwa kwenye mwili wa *Ummah* kupitia mfumo huu wa kigeni wa utawala wa kisiasa na, kwa upande wa pili, jitihada za kijinga, zilizojaa dalili za kuchanganyikiwa kifikra, zinazokosa uchambuzi wa kina wa matatizo yaliyopo zinazowakilishwa na wasomi wa kisasa wa Kiislamu katika majaribio ya kuunda upya Mfumo wa Jumuiya ya Kiislamu ndani ya misingi na mifumo ya Serikali za kitaifa ambazo zimejikita kwenye mfumo wa kidunia usiomtambua Mwenyezi Mung una kuwasilisha kuwa ni mfumo mbadala wa *Khilafah* ya Kiislamu.

Kilichojitokeza kutokana na jitihada hizo ni lengo la ‘kujenga Uislamu’ na kuunda ‘Taifa la Kiislamu’ ndani ya mfumo wa Serikali za kitaifa. Hata hivyo, jitihada hizi zote hazikuweza, na bado haziwezi, kuzaa matunda kwa kuwa, malengo hayo hayawezi kutimia bila ya kwanza kuvunja na kuondoa baadhi ya sehemu muhimu za mfumo huo wa kidunia wa Serikali za kitaifa, sehemu ambazo ni muhimu kwa kuuwezesha mfumo huo wa kidunia wa Serikali za kitaifa kuweza kuwapo na kudumu kama chombo kamili.

Dr Muhammad Iqbal na *Maulana* Abul Ala Maududi (rahimahumullah) wakiwa India, wakiwamo wanazuoni na wanaharakati kama vile Hassan al-Banna wa Egypt, wote walijiingiza kwenye *Ijtihad* (ikim., jitihada binafsi za kutafakari kwa kina) kwa lengo la kujenga upya Mfumo wa Jumuiya ya Kiislamu katika enzi hizi za baada ya kutoweka kwa *Khalifah* wa Kiislamu. Jitihada zao zilizaa wazo jipya na pendekezo la ‘*Taifa la Kiislamu’*. Hata hivyo, kwa bahati mbaya, jitihada za kujenga *Taifa la Kiislamu* kumepelekea mfumo halali na halisi wa Mfumo wa Jumuiya ya Kiislamu, na utaratibu wake wa mfumo wa kisiasa wa *Ummah* (*Pax Islamica* na *Dar al-Islam*) kurudishwa nyuma hadi kufikia hali ya kutoweka na kutoonekana kabisa. Matokeo ya hayo ni kuwa fikra za kisiasa katika Jumuiya za Kiislamu zilielekezwa kule ambako hazikupaswa kuelekea, tendo ambalo linaleta athari mbaya kwa *Ummah*, na matatizo na utatanishi mkubwa uliojitokeza umekiri katika kila hali, kila mahali, hali ambayo inadhihirika na kuukabilia *Ummah* hadi hii leo, ambako waislamu

wanajisajili kama vyama vya kisiasa na kujiingiza kwenye kupigania uongozi kupitia mfumo wa chaguzi za kisiasa katika serikali za mataifa yenye mfumo wa kisasa wa kidunia ambao misingi yake ni ile ya kutomtambua Mwenyezi Mungu. Ushahidi unaonyesha wazi kuwa muda pekee ambao wataweza kupata ushindi na kushika madaraka kwenye taifa la aina hiyo, ni pale tu ambapo watakubali kuwa wateja wa Wazayonisti.

Wakati Wazayonisti, kwa mfano, walipoamua kuwa Libya na Syria zinahitaji kufanyiwa mabadiliko ya viongozi watawala wake kwa kuwa hao walionyeshwa kuwa ni 'madikteta wanaomwaga damu' za raia wao kwa kuwaua baada ya raia hao kuinuka na kuzipinga 'serikali zao za kigandamizi', wateja wa Wazayonisti, ambao walifanikiwa kushika madaraka kwa chaguzi zilizokuwa kwenye mfumo wa Kiislamu, walilazimika kuunga mkono wito huo wa Wazayonisti wenye lebno la kubadilisha utawala.

۞۞۞

# Sura ya Pili

## *Kuanguka kwa Khilafah ya Ottomani na Kuinuka kwa Serikali ya Kitaifa ya Wahhabi wa Saudia inayojengwa kwa Msimamo wa Sera za Kidunia*

"Miongoni mwa malengo makuu ya kisiasa na kijeshi ya Uingereza katika vita, ilikuwa siyo tu kuuangusha Uislamu na kuuondolea nguvu za kiutawala duniani, kuiteka Jerusalem, kuundwa kwa makazi rasmi ya Wayahudi ndani ya Palestina ambapo daima ingepatikana fursa ya kuchafua jumuiya ya Kiislamu ya Mashariki ya Kati kwa niaba ya mataifa ya magharibi. Viongozi wa Wayahudi wa ki-Zayonisti walikuwa pia na lengo la ziada. Walitaka kuunda Taifa la Israeli katika Ardhi Takatifu iliyokombolewa ambalo lingetambulishwa kwa Wayahudi asilia wasiokuwa wazungu kuwa hilo ni Taifa Takatifu la Israeli lililorudishwa upya baada ya kuanzishwa na David (Nabii Daud – rehma na amani juu yake) na Solomon (nabii Suleyman – rehma na amani juu yake). Lengo lao kuu kabisa lilikuwa ni kwa Israeli kuwa Taifa Tawala la dunia na hivyo basi kumpa fursa Dajjal kuweka madai yatakayoeleweka na kukubalika kuwa yeye ni Masihi wa kweli"

## *Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia na Kusitishwa kwa Khilafah ya wa-Ottomani*

Kwa mtazamo wa Jumuiya ya Kiislamu, Vita Kuu ya Kwanza ya dunia ilikuwa ni zaidi ya vita vilivyopiganwa na wakazi wa bara la Ulaya tu. Vita hiyo ilikuwa, ikiangaliwa kwa dira ya kina, ni vita iliyoleta misukosuko mikubwa, na mabadiliko ya kimsingi ndani ya Jumuiya za Kiislamu ambayo hayakuwahi kutokea katika historia yote ya kuwapo kwa waislamu mnamo miaka elfu moja na mia tatu (1300) ya kuwapo kwao.

Kwanza, Mwakilishi wa Waislamu aliyekuwa na nguvu kubwa za dola, akiwa kama mwakilishi na makao makuu ya *Ukhalifa* na utawala wa Ufalme wa Ottomani, aliingia kwenye vita hiyo kwa upande wa Wawakilishi wa Kati (Central Powers). Wakati uamuzi huu bado ukiwa unatingwa na ukungu wa mabishano tangu zama hizo, hadi dakika za mwisho, Uongozi wa Ottomani haukuwa umeamua aidha kujiingiza kwenye vita au kutoshiriki, na hata kama kujiingiza, ni upande upi waungane nao, palikuwa na sababu za kimsingi za kudhani kuwa palikuwapo na uwezekano wa njama zilizosukwa baina ya Wazayonisti wa kiingereza na kifaransa zilizopelekea Ufalme wa Ottomani kuungana na Wajerumani badala

ya kuungana na washirika wao wa kawaida – Waingereza na Wafaransa. Hivyo suala zima la ushiriki wa wa-Ottomani kwenye vita hiyo bado lina utata.

Ushirikiano wa Waingereza na Wafaransa na Urusi ambao ulikubaliwa baina yao na kupitishwa mwaka 1907 ndiyo ulioweka mazingira yaliyopigilia msumari wa mwisho kwenye jeneza la Ufalme wa Ottomani. Kwa hakika, hiyo ndiyo sababu iliyowafanya Wafaransa na Waingereza waikumbatie Urusi. Kumbatio hilo lilipigiwa mstari mkubwa kwa makubaliano ya siri kuwa ushirikiano huo utakapovuna tunda lililokusudiwa, Urusi itakabidhiwa Konstantinopol. Kwa kutumia ghilba kubwa, ikiwa ni moja ya tabia maarufu ya Waingereza na Wamarekani, walipanga kuwa muda huo huo, mpango wa kuupindua utawala wa Kirusi (ikim., kufanya Mapinduzi ya ki-Bolsheviki ya mwaka 1917 yafanyike) kwani mapinduzi hayo yangeinyima Urusi kile walichoahidiwa, mji wa Konstantinopol.

Kiongozi wa ki-Ottomani katika kipindi hicho cha vita, Mehmed Talaat Pasha alizungumza kwa uhakika na kujiamini kwenye kumbukumbu zake kuhusiana na utata ulioukumba Ufalme wa Ottomani (zilizochapishwa baada ya kifo chake). Ni maandishi yaliyo wazi kabisa ambayo yanampa msomaji picha halisi ya mkakati uliopangwa na Wazayonisti kutengeneza mazingira ambayo yalipelekea kuibuka kwa Vita Kuu ya Kwanza ya dunia, ambamo yeye mwenyewe, akiwa mshirika wa Kamati ya Umoja na Maendeleo ya Freemason, kushiriki kwake hakumjengei sifa nzuri. (Tazama kiambatanisho nambari 1)

Miongoni mwa malengo makuu ya kisiasa na kivita ya Uingereza katika vita kuu ya Kwanza ya Dunia ilikuwa ni pamoja na kuuvunja Uislamu kama chombo chenye nguvu duniani, kuiteka Jerusalem, na kuundwa kwa makazi ya Wayahudi ndani ya Palestina na kasha kuitumia hiyo kama chombo ambacho daima kingekuwa na lengo la kusambaratisha na kusimamia kama polisi ulimwengu wa Waislamu wa Mashariki ya Kati kwa niaba ya nchi za Magharibi. Viongozi wa Wayahudi-Wazayonistinda walikuwa na lengo la ziada. Walikuwa na lengo la kuunda Taifa la Isaeli ndani ya Ardhi Takatifu ambalo lingewakilishwa kwa Wayahudi aslilia wasiokuwa wazungu kuwa hili ni Taifa lililorudishwa likiwakilisha Taifa Takatifu la Israeli ambalo lilianzishwa na David (Nabii Daud -rehma na amani juu yake) na Solomon (nabii Suleyman – rehma na amani juu yake). Lengo lao kuu ilikuwa ni kuhakikisha kuwa Taifa la Israeli linakuwa Taifa Tawala duniani na hivyo basi kumruhusu Dajjal kuweka madai kuwa yeye ni Masihi wa kweli.

Kuingia kwa Ufalme wa Kiislamu wa Ottomani kwenye Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia kwa upande wa Ujerumani kulikuwa ni hatua muhimu sana ya kwanza katika utekelezaji wa malengo ya Wazayonisti. Walikwishafanya majaribio kadhaa ya kutaka kuwa na makubaliano na Khalifah wa ki-Ottomani ya kupewa mamlaka na utawala juu ya Jerusalem kabla ya hapo ambayo yote hayakufanikiwa. Ilifikia hadi kutaka kutoa pesa na kuununua mji mtakatifu wa Jerusalem. Uingereza ilikuwa inaunga mkono jitihada hizi za Wazayonisti wa Kiyahudi. Wa-Ottomani waliendelea kukataa maombi hayo, na matokeo yake, ikawabidi waichukue Jerusalem kwa kutumia mtutu wa bunduki. Pili, ili kutowapa wa-Ottomani nafasi ya kujikusanya upya na kuungana na Waislamu wengine kuuchukua tena mji

wa Jerusalem, walilazimika kuvunja Ufalme wa ki-Ottomani na kuiweka nchi ya Uturuki chini ya utawala ambao ungefuta mahusiano yote ya Kiislamu ya Waturuki na Jerusalem.

Ufalme wa Ottomani kama ulivyotarajiwa ulijaribu kuushawishi *Ummah* wa Kiislamu kujiunga kwenye jitihada zake katika vita hiyo kutoka kwenye nchi zote za Kiislamu dunia nzima. Katika jitihada hizo, mnamo mwezi wa Kumi na Moja (Novemba) tarehe 23 mwaka 1914, *Shaikh al Islam* wa Utawala wa Ottomani alitoa rasmi tamko la Fatwa na azimio la jihadi na kuwaamuru Waislamu wote kupigana dhidi ya Mataifa Washirika (Allied Nations) (Matamshi ya Fatwa yanapatikana katika kiambatanisho nambari 2). Diplomasia ya Kiingereza, hata hivyo, ilifanikiwa kutumia hila ‘mchipuko wa kwanza wa kiarabu’ na kuyashawishi mataifa ya Ghuba kwa kuupendekeza Utaifa wao kama zana ya kupinga wito huo wa Fatwa na hivyo kuhakikisha kuwapo kwa misingi imara ya kudidimiza nguvu na jitihada umoja na udugu wa Waislamu wote. Hali hiyo ilipelekea kwa Waarabu kupinga msimamo na wito wa watawala wa Ottomani na badala yake, ‘kama tutakavyoona kwenye mchipuko wa pili wa Kiarabu’ takriban miaka mia moja baadaye, walilitumia pendekezo la Waingereza la kupewa msaada utakaohakikisha kuwa wanapata uhuru wao kila mmoja kama taifa huria, huku wakibakia na kuashiria kuwa dunia ya Kiarabu kuendelea kuwa rahisi kudanganywa na kuwapa ushindi wa ila wa Wazayonisti.

Katika muda usiotimia miaka miwili, mara baada ya kuanza kwa vita hiyo, Sharif al-Husain, aliyejitangaza kuwa ni ‘Mfalme wa Waarabu’, akiwa kama rafiki wa dhati wa Uingereza, ambaye ni baba wa babu wa Mfalme Husain wa Jodani, alikuwa ameshafanikiwa kuasi Utawala wa Ottomani na alivishwa taji kama Mfalme wa *Hejaz*, ambalo ni shina na chimbuko la Uislamu. Kutokana na kutoweka kwa mji wa Makkah na hatimaye mji wa Madina kutoka kwenye mikono na usimamizi wa Ufalme wa Ottomani, tamko la Fatwa la Ufalme wa Ottomani lililoelekezwa kwa Waislamu wa dunia nzima lilipata pigo kubwa sana na kupungukiwa na thamani yake, jambo lililoleta athari ambazo hazikuwa na suluhishi.

Waingereza walijiongezea ushindi wao ndani ya Hejaz pia kwa kuwateua na kuwaweka watoto wa Husain kama Wafalme wa Iraq na Transjodani. Hadi mwaka 1919, Jenerali wa Kiingereza, Allenby, akiwa na wapiganaji wa Kiarabu miongoni mwa wapiganaji wake watiifu, aliingia kwa ushindi Jerusalem na kutangaza rasmi kuwa vita vya krusedi sasa hatimaye vimefikia kikomo. Palestina iliwekwa chini ya mamlaka ya Waingereza (mamlaka yaliyowekwa na kuthibitishwa na Ligi ya Mataifa (League of Nations) hadi mwaka 1948 ambamo Uingereza ilijitoa na Wazayonisti wa Kiyahudi walitangaza kuanzishwa kwa Taifa la Israeli.

‘Mchipuko wa pili wa Kiarabu’ ambao bado unaendelea wakati maneno haya yakiandikwa, unalenga kuendeleza mafanikio yaliyokwishapatikana na kujumuisha Zaidi kutoweka kwa silaha za nyuklia za Taifa la Pakistani, na hivyo basi kupelekea kuibuka kwa Taifa la Israeli kama *Taifa Tawala* duniani.

Ufalme wa Kiislamu wa ki-Ottomani ulishindwa katika vita kwa kuangamizwa kwa kiasi na athari kubwa. Mataifa Washiriki walijumuisha nguvu zao kwa pamoja ikiwemo nguvu za silaha za kisaikolojia ambazo zilikuwa na athari kubwa sana kwa Uislamu. Waingereza na Wafaransa walifanikiwa kuhakikisha kuwa wanaungwa mkono na majeshi ya Kiislamu yenye wapiganaji waislamu (kwa kutumia hila, bila kujali uhalali) kuanzia India, eneo la Maghrebu na sehemu nyinginezo kiasi hali kufikia kuwa Waislamu Waarabu na hata pia Waislamu wasiokuwa Waarabu wakawa wanapigana kwa upande wao kuwapiga ndugu zao Waislamu wa Kituruki. Matokeo yakawa kuwa Ufalme wa Kiislamu wa Ottomani haukushindwa tu vita peke yake, bali pia misingi ya jumla ya Kiislamu ya kukubalika kwake ikawa imevunjika na kutoweka.

Baada ya kushindwa huko kwa wa-Ottomani mnamo vita Kuu ya Kwanza ya Dunia, majeshi ya kitaifa ya Kituruki, yakiongozwa na Mustafa Kamal, akiwa na msimamo wa sera za kidunia, yalijikita kupigana kile kilichoitwa kuwa ni "vita baada ya vita" kwa ustadi mkubwa, uhodari wa hali ya juu na msisimko kiasi kwamba mataifa makubwa ya bara la Ulaya yaliyokuwa yameshachoshwa baada ya kupigana vita kwa miaka kadhaa, hawakuingilia tena kati kwenye vita hiyo kwa kuhofu kutoenda kinyume na matakwa na utashi wa wananchi wao uliojitokeza kwenye vipimo vya maoni kwenye nchi zao, hivyo kupelekea Uturuki kuishinda Ugiriki (iliyoshika imani ya asilia ya Kikristo – ikim., *Rum* inayotajwa katika Qur'ani) kwa kuipa kipigo kikubwa na kujipatia uhuru wao. Makubaliano ya Lausanne, yaliyotiwa saini mwaka 1924, yaliyatambua maeneo yote ambayo Waturuki waliyapata baada ya mapigano hayo na hivyo kuweza kutambulika kimataifa. Upako wa Mustafa Kamal, shujaa mpya wa Uturuki ya kisasa yenye msimamo wa kidunia, ukawa umekamilika. Ushindi wa *Dajjal* ukawa kamilifu na wa kupendezesha mno!

## *Wazalendo (Nationalists) wa Kituruki na Khilafah*

Vikundi vya wazalendo wa kituruki vilikuwa vikipingana na *Khalifah-Sultani* kwa zaidi ya miaka hamsini, upinzani wao ukiwa na lengo la kusitisha mamlaka yake kwa kutumia katiba ikiwa na lengo la kuuondoa utawala wake ambao waliuona kuwa ni wa udikteta wa kidini. Vikundi hivyo vya kizalendo vywa Kituruki vilikuwa na msimamo wa kisiasa ambao aghlabu ulikuwa wa kidunia na walivutiwa kwa kiasi kikubwa na kile walichokiona kuwa ni dalili dhahiri za ubora wa utamaduni wa Kimagharibi ukilinganishwa na Ukhalifa wa Ottomani na Ufalme wa Kiislamu.

Baada ya kuondolewa kwa miji ya Makkah na Madina, na hatimaye baada ya ndugu zao wa Kiislamu kupigana kwa upande wa maadui zao katika vita Kuu ya Dunia, walijikuta hawana tena hamasa ya kujiambatanisha na dunia ya Kiislamu. Bila kusita walipitisha uamuzi wa kubadili msimamo na mtazamo wao wa kisiasa kutoka kwenye mfumo wa zamani wa *Dar al-islam*, au Mfumo wa Maadili wa Jumuiya ya Kiislamu, kuelekea kwenye mfumo

wa kimagharibi wa nchi na serikali za Kitaifa zenye sera za kidunia, na hivyo kuanzishwa kwa Taifa la Uturuki.

Katika kufanya mabadiliko kama hayo, ilibidi, na daima bado itaendelea kuwa haina budi, kulazimika kuwapo kwa kutenganishwa kwa ‘kanisa’ kutoka kwenye ‘serikali’ kwani huu ndiyo hasa msingi wa mfumo wa kimagharibi[5]. Utenganishaji huo ni muhimu kufanyika ili kujenga taifa la kidunia.

Bunge Kuu jipya la Uturuki, likiwa limejikita kwenye misingi ya mfumo mpya lilianzisha na kupitisha uteuzi wa Abdul Majid kama *Khalifah* mnamo mwaka 1922, kuwa kama kiongozi wa ‘Kanisa’ la Kiislamu. Ukhalifa wake, hata hivyo, ulinyonyolewa na kunyang’anywa nguvu na mamlaka ya aina zote.

Nguvu hizo, na madaraka yote yalihamishiwa kwenye Taifa / Serikali. Ilikuwa pia ni jambo lisiloweza kuzuilika kuwa mfumo huu mpya nao usingeweza kudumu nchini Uturuki, ukitilia maanani hali halisi ya Uislamu nchini Uturuki.

Haikuwezekana, na bado haiwezekani, kuutendea Uislamu kile ambacho Wazungu wa bara la Ulaya wameutendea Ukristo baada ya kuvunja Ufalme Mtakatifu wa Kirumi. Khalifa hakuwa, na hakuweza kuwa, sawa na Papa[6]. Pasingeweza kuwapo kwa sera za kisiasa za kidunia ndani ya mfumo wa Kiislamu kwa kuwa Uislamu ulikuwa hautambui utenganishaji wa Kanisa kutoka kwenye Nchi / Taifa / Serikali. Kwa hakika, hakukuwa na kitu chochote ambacho kingeweza kukubalika na Waturuki ambacho kingejulikana kama ‘kanisa’ la Kiislamu.

Punde tu hali halisi na ushahidi ukadhihirisha kuwa mfumo mpya wa Serikali ya Kitaifa haukuweza kushamiri wakati mfumo wa *Khilafah* ukiwa nao bado upo. Vikundi vya Wazalendo wa Kituruki vilitambua kuwa Serikali ya Taifa dhidi ya mfumo na hali halisi ya Uislamu ndani ya Uturuki aidha vililazimika kukusanya nguvu na kuchukua madaraka ya kuusimamia Uislamu ili kuuweka chini ya uangalizi wa serikali au kulazimika kukubali matokeo mabaya (ikimaanisha kwa mtazamo wao) ya Uislamu kuchukua mamlaka ya nchi na kurudisha *Dar al-Islam*.

Hivyo halikuwa jambo la kushangaza, pale ambapo Bunge Kuu la Taifa la Uturuki lilipopitisha mnamo tarehe 3 mwezi wa Tatu (Machi) mwaka 1924, sheria ya kusitisha na kuvunja Khilafah. Kifungu cha kwanza cha Sheria hiyo kinasema:

---

[6] ili kufanya mjadala wenye mvuto na hamasa kuhusu suala hili, tazama kitabu cha mwandishi Toynbee, Ed. Uchambuzi wa Masuala ya Kimataifa, 1925, Toleo 1 ukurasa 55 – 68, hususan ukurasa wa 55. Pia angalia sura

"Khalifa ameondolewa. Utawala wa Khalifa umesitishwa, kwa kuwa Ukhalifa kimsingi umejumuishwa kimaana na kiumuhimu ndani ya maneno Serikali (Hukumah) na Taifa (Jumhuriyyah)"[7].

Kupitishwa kwa sheria hii kuliashiria wakati muhimu mno kihistoria, na pia kulileta athari kubwa sana, kwenye hali na mwenendo wa *Ummah*.

Baada ya muda wa miaka elfu moja na mia tatu ambamo ndani yake *Khalifah* alikuwa akitambulika na waumini wote duniani (ikimaanisha waislamu wote wa Sunni), akiwa kama chombo muhimu kwenye dini yao, hata pale ambapo nafasi hiyo alipewa mtu ambaye uteuzi na uchaguzi wake ulikuwa na dosari au ulifanywa kinyume na misingi ya Uislamu, *Ummah* wa Kiislamu ulijikuta unaingia kwenye karne ya kumi na nne ya kuwapo kwake bila ya kuwa na *Khalifah*. Na hali kwa uhakika ilikuwa ikionyesha kuwa mabadiliko hayo ni ya kudumu kiasi kwamba mtu angedhani na ingebidi asamehewe kwa kuhitimisha hivyo; kuwa ulimwengu wa Kiislamu hivi sasa daima umeingia katika enzi za baada ya-*Khilafah*.

## *Majibu na msimamo wa Chuo Kikuu cha Al-Azhar kuhusu kusitishwa kwa Khilafah ya Ottomani*

Umuhimu wa kusitishwa na kuvunjwa kwa *Khilafah* kulikuwa kunapatikana ndani ya Kifungu Cha Kwanza cha Sheria hiyo ya usitishaji wa *Khilafah*, ambamo kwa ujanja na maarifa, Serikali ya Kitaifa yenye msimamo na mtazamo wa kidunia ndiyo ilikuwa inachukua nafasi ya *Khilafah*. Chombo ambacho kilikuwa kikitambulika kama sehemu muhimu ya Uislamu kilikuwa kikiondolewa na badala yake kupachikwa mamlaka ya kitaifa yenye msimamo wa kidunia ulioelekea kusimamishwa kwa misingi ya itikadi na nadharia za utamaduni wa kimagharaibi, zinazosimamiwa na *Dajjal*, na kwa misingi ya mfumo wa kisiasa ambao umeanzishwa na kushikiliwa na nchi za jamii ya kimagharibi, na misemo au istilahi (kama vile Hukumah na Jumhuriyyah) zilizotumika zilitumiwa kwa namna tofauti alimradi kuweza kwenda sambamba na mfumo na hali mpya iliyojitokeza.

---

ya mwisho iliyoandikwa na Sylvia Haim ndani ya kitabu hicho cha Arnold, T: Khilafah, toleo la pili, Oxford University Press, 1965, ukurasa 205 -244.

[7] Maandishi mahususi ya Kituruki kwenye Qawanin Majmuasi 1924/1340, nambari 431, Ankara; iliyopigwa chapa na Bunge Kuu la Uturuki, kiambatanishi cha 11 (3), ukurasa wa 575.

Pamoja na kuwa ni msomi na mkufunzi stadi na hodari, Dr. Muhammad Iqbal anaonyesha kutoweza kuelewa fika hali halisi na misingi ya mabadiliko ambayo yalikuwa yakijitokeza wakati ule, na matokeo yake amefanya kosa kubwa sana.[8]

Kwa kuwa *Khilafah* ilikuwa ni sehemu ya dini ya Kiislamu ilikuwa dhahiri kuwa (kwa mtazamo wa kidini) tendo kubwa na baya mno lenye haki ya kubeba lawama za aina zote la *Bid'ah* lilikuwa likitendwa na kupitishwa na hali hiyo ilihitaji hatua makini za kutoa majibu na mwongozo wa kidini. Siku ishirini na mbili baada ya kupitishwa kwa sheria hiyo na Bunge la Taifa la Uturuki, Mkuu wa Chuo Kikuu cha Kiislamu cha *Al-Azhar* cha Kairo alikutana na ulamaa viongozi wa Chuo na wa nchi nzima ya Egypt na kwa pamoja walitoa tamko lifuatalo kuhusiana na *Khilafah*:

> "*Khilafah* ambao unatambulika sawa na *Imamah* (Uongozi / Uimamu), ni kitengo cha jumla cha uongozi (*Ri'asah*) katika mambo yanayohusu *al-Din* na *al-Duniya*. Kazi yake na wajibu wake muhimu ni kusimamia maslahi ya *Millat* na utawala wa *Ummah*."

Tamko hilo liliweka wazi jukumu la 'jumla la uongozi' kwenye kitengo cha *Imam*, ambaye alitajwa kama:

> "...kiongozi msimamizi wa sheria za dini kwa lengo la kulinda imani, kwa kusimamia utekelezaji wa amri hizo za kidini na pia kuwa na mamlaka ya uamuzi wa masuala yote ya siku hadi siku kama vile ambavyo *Shariah* inavyoamrisha.

[8] "Hebu sasa tuangalie jinsi gani Bunge Kuu la Taifa la Uturuki lilitumia uwezo huu wa *Ijtihad* kuhusiana na taasisi ya *Khilafah* (Ukhalifah). Kwa mujibu wa sheria ya ki-Sunni, kuchaguliwa kwa Imam au Khalifah hakuna mjadala. Swali la kwanza linalojitokeza kuhusiana na hilo zoezi ni hili: Je, Ukhalifah ukabidhiwe au uwekwe mikononi mwa mtu mmoja? Kwa mujibu wa *Ijtihad* hiyo ya Uturuki ni kuwa wanaona kwa mujibu wa msimamo wa Kiislamu, Khilafah au himaya chini ya Imam inaweza kukabidhiwa chombo kinachojumuisha kundi la watu, au Bunge lililochaguliwa kwa kura (mfano; Bunge Kuu la Taifa la Uturuki). Wanazuoni wa Kiislamu wa Egypt na India, kwa kadiri ninavyojua, hawajatoa maoni yao kuhusu suala hili. Binafsi naamini kuwa msimamo na mtazamo wa Waturuki uko sawa sawa. Hakuna hata sababu wala umuhimu wa kujadili na kupinga msimamo huu. Mfumo wa serikali wa kijamhuri siyo tu kuwa unaenda sambamba na kupatana na mfumo na kanuni za Kiislamu, bali pia umekuwa ni muhimu kwa mujibu wa mtazamo na nguvu mpya ambazo zimejitokeza baada ya kuahiwa huru ndani ya ulimwengu wa Kiislamu." [Iqbal, M: Kuundwa Upya kwa Fikra za Kidini katika Uislamu; Oxford University Press. London. 1934, Sura ya VI, "The Principle of Movement in the Structure of Islam", ukurasa 149.

"*Imam* anakuwa kiongozi mhusika wa usimamizi wa malipo ya utii (*Bai'ah*) juu ya wale wote wenye uwezo wa 'kushindwa na kujisalimisha' (*ahl al-halli wal-aqd*)[9] (loose and bind) au vinginevyo kuchaguliwa na aliyemtangulia kuchukua nafasi yake.

Utawala wa Imamu pia unaweza kunyakuliwa kwa kutekwa ikimaanisha kuwa ikiwa upande wa pili umeweza kuichukua *Khilafah* na kuyahamishia kwake madaraka na mamlaka ya *Khalifah*, *Khalifah* aliyenyang'anywa madaraka anapoteza nafasi hiyo. Wakati mwingine hutokea kuwa baada ya kutekwa, kupotezwa huko kwa madaraka kunaimarishwa kwa Khalifah aliyetekwa kukiri na kutoa tamko la utiifu kama ilivyokuwa ikitokea kwa wengi baina ya *Khulafah* waliopita[10]

Wakirudi kwenye hali halisi iliyokuwa ikiwakabili, tamko hilo liliulaumu uamuzi huo kuwa ni wa *Bid'ah*, uamuzi ambao haujawahi kuchukuliwa kwenye historia nzima ya Uislamu, ikiwemo kwanza uteuzi wa Abdul Majid kuwa *Khalifah* ambaye amechaguliwa kushika nafasi kwenye cheo ambacho kimekwishavuliwa nguvu na mamlaka yake yote, mamlaka ambayo yalichukuliwa na kuhamishiwa kwenye Bunge Kuu la Uturuki, na pili kuvunjwa na kusitishwa kwa *Khilafah*.

Kwa kuwa vitendo vya *Bid'ah* ni vitendo vinavyoenda kinyume kabisa na amri na malengo ya imani ya dini, ulamaa walikubaliana kuwa liitishwe Kongamano la Kiislamu, kwa kutoa mwaliko kwa wawakilishi kutoka jumuiya zote za Kiislamu za dunia nzima ili liamue jukumu la kusimamia *Ukhalifah* wa Kiislamu likabidhiwe kwa nani.

Hili lilikuwa ni jibu la mwanzo liliokuwa muhimu la Jumuiya ya Kiislamu kuhusiana na kuvunjwa kwa *Khilafah* ya *wa-Ottomani*. Lakini ni muhimu kukumbuka kuwa pendekezo hilo lilikuwa lina tofauti kubwa na za msingi kulingana na hulka za kisiasa zilizokuwa zikitumika kwenye mfumo asilia wa Uislamu. Pangeweza pia kupatikana kwa mtazamo kuwa huo nao ulikuwa ni *Bid'ah. Ulamaa* wa Al-Azhar walipendekeza kutumia Kongamano la Kiislamu, japo lingekuwa na wawakilishi kutoka jumuiya zote za Kiislamu kama washiriki, kumchagua *Khalifah* mpya.

---

[9] Kundi hili lilipaswa kujumuisha chombo cha maamuzi ya kuchagua kama livyo kwenye mfumo halisia wa Kiislamu. Hata hivyo, katika historia yote ya Uislamu ilibakia kuwa chombo kilichoundwa na kubaki kwenye nadharia peke yake kwani hakikuwa na hakikuweza kutimiza jukumu lolote kwenye utaratibu wa kufanya maamuzi muhimu.

[10] Tamko hili ni muhimu sana hususan kwenye maudhui ya jitihada za sasa za kutaka kuurudisha Mfumo halisi na halali wa Mpangilio mzima wa Jamii ya Kiislamu kwa mujibu wa Shariah. Linadhihirisha makosa ya wazi kabisa kwenye uelewa wa mfumo na utaratibu wa uongozi wa Kiislamu uliofanywa na chombo hicho cha juu kabisa cha kisomi cha Kiislamu. Tamko kamili: Uchambuzi, Op, cit., Kiambatanishi 111, kurasa 576 – 578.

Haijawahi kutokea tangu nusu ya kwanza ya karne ya kwanza ya historia ya Uislamu, kuchaguliwa *Khalifah* kwa kupigiwa kura na watu. Na pia haijawahi kutokea katika historia nzima ya *Ummah* wa Kiislamu kwa *Khalifah* kuchaguliwa na Bunge au na Kongamano lililowakilisha Waislamu wote.[11]

Pendekezo lilikutana na changamoto nyingi kiasi kufikia kuwa kamati maalum iliyopewa jukumu la kupanga na kuandaa Kongamano ililazimika kubadili ajenda yenye joto kubwa ya uchaguzi wa *Khalifah* mpya na badala yake kweka ajenda iliyokuwa na kukubalika kwa wepesi zaidi ya uchambuzi wa hali iliyojitokeza na utafutaji wa suluhisho la hali iliyotokana nayo. Kilichokuwa na umuhimu mkubwa na wa kipekee, hata hivyo, ilikuwa ni tukio lenyewe ambamo kwa mara ya kwanza katika historia ya Uislamu, wazo lilipitishwa na jumuiya au jopo la *Ulamaa* wa Kiislamu, kuwa mambo muhimu kuliko yote yanayowahusu waislamu na *Ummah*, yanaweza kujadiliwa na maamuzi yakapitishwa na mkutano au kongamano linalowajumuisha Waislamu wote.

Ni vigumu sana kufikia uamuzi wa kuwa je ni kweli, matokeo haya yalipata kuathiriwa na ushawishi ulioshinikizwa na utamaduni wa kimagharibi, kama vile ambavyo Toynbee anavyotutaka tuamnini kuwa ndivyo.[12] Pamoja na yote, ukweli unabaki pale pale kuwa kama Kongamano lingetumia *Shurah* na *Ijma'a* katika maamuzi yake, hilo lingeyafanya maamuzi hayo kuwa karibu zaidi na hali halisi ilivyokuwa wakati wa Uislamu wa awali kuliko vile ambavyo *Khilafah* ilivyokuwa, kwani ukiacha miaka isiyozidi makumi kadhaa ambamo ilikuwa ikifuata nyayo asilia, muda wote uliobaki haikuwa na dalili za kufanya hivyo

[11] Pendekezo lilikuwa jipya na la aina yake kinamna kiasi ambacho lilishutumiwa na kukataliwa na Qadhi Mkuu wa Transjordania kuwa hilo nalo ni tendo la ubunifu ambalo linaenda kinyume na taratibu halisi na halali za Kiislamu. Uchambuzi, Op. cit., ukurasa 84.

[12] "Wakati Bunge Kuu la Taifa la Angora (Ankara) lilipopitisha uamuzi wa kuvunja na kusitisha Ukhalifa wa Ottomani na wakati Wahhabi walipowafukuza ufalme wa Hashimi kutoka Hejaz, msukumo wa kiujumla wa majibu ya Waislamu kukabiliana na hali hiyo ulikuwa ni kutumia taratibu za kisasa za utamaduni wa ki-Magharibi wa kuitisha kongamano la kimataifa na siyo kufuata utamaduni wa utaratibu wa Kiislamu wa kuitisha Vita Takatifu." Uchambuzi, Op. cit., ukurasa 24.

# Sura ya Tatu

## *Kongamano la Khilafah, Kairo (Mwezi wa Tano, 1926)*

Ilikuwa katika kujibu uharibifu na uchafuzi wa mwenendo safi wa dini, pale ambapo mjukuu wa Mtume (rehma na amani juu yake) Imam Husain (radhiallahu anhu), kishujaa alipoinua juu zaidi kiwango cha upinzani dhidi ya madai haramu ya *Bai'ah* kutoka kwa Yaziid, mtoto wa Amir Muawiyah (radhiallahu anhu). Upinzani wake ulipelekea kuuawa kama Shahiid kwenye mbuga za Karbala. Hata hivyo, bado pana mapinduzi ambayo bado hayajafikia kikomo hapo Karbala ambayo yatakamilishwa kishujaa wakati wa kuibuka kwa *Imam al-Mahdi* (alaihi al-Salam). *Ni mapambano kuirudisha dini iliyosimamishwa na Mtume wetu mbarikiwa (rehma na amani juu yake) ambayo imechafulliwa na nguvu zinazopinga mapinduzi hayo.*

Eskatolojia ya Kiislamu ingeweza kuliongoza Kongamano kugundua kuwa dunia hivi sasa imeshikiliwa na Ya'juj na Ma'juj, na kwa kadiri mpangilio wa dunia kwa mujibu wa Yajuj na Majuj utakuwa ukiendelea, haitowezekana kuirudisha Khilafah asilia na halali kama ilivyokuwa awali

# *Ajenda*

Kongamano la *Khilafah* ambalo hatimaye lilifanyika mjini Kairo, mnamo mwezi wa Tano mwaka 1926, lilikuwa na masuala yafuatayo katika ajenda yake, mambo ambayo yalikusudiwa kuangaliwa kwa kina:

1. "Kufafanua na kuelezea *Khilafah* na kuweka wazi vigezo vinavyohitajika kutimizwa na anayechaguliwa kuwa *Khalifah*.

2. Je, *Khilafah* ni muhimu kwenye Uislamu?

3. Jinsi gani *Khilafah* itungwe kimkataba?

4. Je, inawezekana katika wakati uliopo kujenga *Khilafah* ambayo ingetimiza mahitaji na matakwa yote ya *Shari'ah?*

5. Je, ikiwa jibu la swali namba nne hapo juu likiwa ni "hapana, haiwezekani", je hatua zipi zichukuliwe?

6. Mathalani Kongamano likiamua kuwa ni muhimu kumchagua *Khalifah*, je, ni hatua zipi zinalazimika kuchukuliwa ili kuhakikisha uamuzi huo unatendeka?"

# *Wajumbe*

Wajumbe walioshiriki kwenye Kongamano walitoka Egypt, Libya, Tunisia, Moroko, Afrika ya Kusini, Indonezja, Yemen, *Hejaz* (sasa iko ndani ya Saudi Arabia), Palestina, Iraqi, na Polandi. Kilichojitokeza wazi ni kukosekana kwa wajumbe wawakilishi wa nchi na jumuiya nyingi muhimu za Kiislamu kama vile Uturuki, Persia (sasa Iran), Afghanistani, *Najd* (sasa iko ndani ya Saudi Arabia) na jumuiya za Kiislamu za Urusi, China na India.

Uturuki iliukataa mwaliko kupeleka wawakilishi kwa jibu la mkato kuwa Uturuki kama nchi haina tatizo la *Khilafah*. Persia, nchi ya madhehebu ya *Shia*, haikutaka kuonyesha ushahidi wowote kuwa ina nia wala haja ya kushiriki kwenye Kongamano la *Khilafah* ya ki-*Sunni*. Waislamu wa Urusi, China na India, wakiwa ni wachache kwa idadi na wanaoishi kwenye nchi zilizo na waumini wengi wa dini zisizokuwa za Kiislamu, kwenye mazingira yasiyokuwa rafiki kidini, wote walionyesha msimamo wa aina moja. Hawakuhudhuria Kongamano la Kairo la mwezi wa Tano mwaka 1926, wakilichukulia Kongamano hilo kuwa kama ni zoezi la kisomi tu, mkusanyiko usiokuwa na nguvu za uhakika na za kweli na halisi, na mkusanyiko ambao usingeweza kuwapa wao kinga wala faida ya aina yoyote ile inayoweza kupimika kwa namna yoyote.

Lakini, ikumbukwe kuwa walifanya hivyo kwa sababu palikuwa na Kongamano pinzani, lililokuwa limetayarishwa na wale ambao walionekana kuwa kama vile ndiyo wenye nguvu za kiukweli na za uhakika, Abd al-Aziz ibn Saud. Kwa hakika, yeye binafsi, alikuwa na khofu kubwa juu ya uwezekano wa kuzaliwa upya kwa *Khilafah* kwani ni punde tu alikuwa amefanikiwa kujinyakulia mamlaka juu ya miji mitakatifu ya Makkah na Madina na kuiingiza kwenye utawala wa kifalme wa ukoo wake.

Mwisho, miongoni mwa wajumbe waliohudhuria Kairo, alikuwamo kiongozi wa *Sanusi* (sufi), al-Sayyed idris al-Sanussi, aliyeteuliwa kama *Amir* wa Barka na Tripoli. Habari zilikuwa zikivuma kuwa palikuwa na uwezekano mkubwa sana wa yeye, al-Sayyed Idris al-Sanussi kuteuliwa kuwa *Khalifah*, pindi kama ingeamuliwa na kufikiwa uamuzi kwenye Kongamano hilo la Kairo kuwa *Khalifah* ateuliwe.[13]

## *Vikao vya Kongamano*

Kongamano lilifanya jumla ya vikao vinne mnamo tarehe 13, 15, 18 na 19 za Mwezi wa Tano, mwaka 1926. Katika kikao cha kwanza, Kamati maalum ya Kwanza iliteuliwa “kuyaangalia kwa kina na kuyachunguza mapendekezo na kisha kuyawakilisha mbele ya wajumbe wa Kongamano”. Kamati mara moja ikapendekeza kuwa majadiliano ya Kongamano yafanyike ‘kwa siri’. Pendekezo hili lilikataliwa katika kikao cha nne cha Kongamano, na matokeo yake ni kuwa tunaweza kupata nyaraka ambazo ziko wazi zinazojumuisha matamshi yote yaliyotamkwa kwenye Kongamano hilo.[14]

---

[13] Sylvia Haim anadai kuwa palikuwa na ushahidi wa kutosha kwamba Kongamano lilipangwa na kutayarishwa kwa msisitizo wa Mfalme Fuad ambaye kwa siri alikuwa na matumaini ya kujipatia mamlaka ya Ukhalifa yeye binafsi. Lakini jambo hili lisingewezekana kwa sababu ya upinzani wa ndani na nje ya Egypt. Cf. Arnold, Op. cit. kurasa 241 – 242. Wakati huenda taarifa hizi zikawa ni za kweli, msimamo wa kijumla uliokuwa ukijulikana wazi na jamii ni kuwa Fuad hakuonyesha dalili zozote za kuyataka mamlaka hayo. S’ad Zaghlul, Waziri Mkuu wake, naye alionyesha msimamo usioegemea upande wowote kwenye suala hili.

[14] Mazungumzo na mijadala ya Kongamano ilirekodiwa na kutafsiriwa kwenye lugha ya Kifaransa na yalichapishwa na A. Sekaly katika *Revue du Monde Musulman*, Toleo 1, p. XIV, Paris, 1926. Ni chapisho hili ambalo mwandishi analitumia.

Kamati maalum ya Pili na ya Tatu ziliteuliwa katika kikao cha pili cha Kongamano na Kamati ya Pili ilipewa jukumu la kuyaangalia na kuyachunguza masuala nambari 1, 2 na 3 yaliyo kwenye ajenda ya Kongamano, wakati kamati ya Tatu ilipewa jukumu la kuyaangalia na kuyachunguza masuala nambari 4, 5 na 6 ya ajenda ya Kongamano. Ripoti za Kamati ya Pili na ya Tatu na majadiliano na maamuzi yaliyopitishwa kufuatia ripoti hizo ndizo hasa zilijenga msingi wa kazi ya Kongamano. Hapa tunaelekeza jitihada zetu katika kuziangalia ripoti hizi kwa kina.

## *Kamati ya Pili*

Katika kuifafanua taasisi ya *Khilafah*, Kamati ya Pili iliyategemea maandishi yanayopewa uzito wa aina yake ya wasomi kama vile al-Mawardi, Ibn Khaldun na wengine. Miongoni mwake, walisisitiza umuhimu wa kuwa *Khalifah* lazima ajumuishe katika mamlaka yake uongozi na uamuzi wa masuala ya 'kidini' na pia uongozi na uamuzi wa masuala ya mpito ya kidunia kwa kuwa Uislamu hauruhusu utenganishaji wa 'kanisa' na 'Taifa'. Pili, patalazimika kuwapo kwa *Khalifah* mmoja tu katika muda husika kwa kuwa, miongoni mwa mambo mengine, jukumu la taasisi ya *Ukhalifah* ni kuunganisha *Ummah* uwe kitu kimoja.[15]

Swala la pili lililoikabili Kamati (*Je, Khilafah ni muhimu katika Uislamu?*) lilikuwa, kwa kusema kwa uchache kabisa, la kushangaza mno. Hapa tunazungumzia taasisi ambayo daima ilikuwa yenye umuhimu mkubwa wa aina yake kwa Waislamu wa *Sunni* na mfumo wao mzima wa kisiasa na utawala, taasisi ambayo imekuwa imo ndani ya mfumo wa Uislamu tangu baada ya kifo cha Mtume (*rehma na amani juu yake*). Katika kipindi chote cha historia ya *Ummah*, si tu *Ukhalifa* umekuwa upo kwa wakati wote, bali pia kama nyongeza, *Ummah* haujawahi hata kufikiria kuwapo kwa mfumo mbadala.

Kwa kweli kabisa, hata tu kile kitendo cha mtu kujaribu kupendekeza mfumo mbadala wa mfumo wa *Khilafah* kuwa unawezekana, basi mtu huyo alikuwa anafungua mlango hatari sana wa kuweka uwezekano wa kupewa na kushutumiwa na madai ya kujiingiza kwenye *Bid'ah*. Hata hivyo, hiyo ikiwa ni matokeo ya uamuzi binafsi wa mtu mmoja, Mustafa Kamal wa Uturuki, hapa tunakikuta kikao kikubwa kabisa cha *Ulamaa* wa Kiislamu wa takriban dunia nzima, walikuwa wakipendekeza swali kwa wajumbe wa Kongamano - *Je, Khilafah ni muhimu katika Uislamu?*

---

[15] Baada ya kutoa hoja kuwa Khalifah alikuwa anahitajika kubeba majukumu ya "kupitisha maamuzi ya hukumu kwa mujibu wa Shariah, kusimamia maamuzi halali yanayopitishwa, kusimamia bandari, kuunda majeshi n.k." Kamati iliona pana umuhimu wa kutosha kunukuu Ahadith ya Mtume isemayo:

"*Yeyote atakayekutwa na umauti ilhali hakumjua Khalifah wa kipindi cha uhai wake, mtu huyo amekufa kifo cha kipagani"; na "Yeyote atakayekutwa na umauti bila ya kutoa kiapo cha utiifu kwa Khalifah au Amir cha Bai'ah, mtu huyo amekufa kifo cha kipagani*." Revue, Op. cit., kurasa 74 -76

Pamoja na yote, inawezekana kabisa kuwa, hili lilikuwa swali muhimu kuliko yote katika historia nzima ya *Ummah*, ambalo *Ummah* ulipaswa kulijibu. Kwani kama ilivyojitokeza, jambo ambalo halikuweza kuepukika, Kamati ilithibitisha kuwa taasisi ya *Khilafah* katika Uislamu ni muhimu, ila kwa muda na kipindi kile kilichokuwapo, haikuwezekana kutekelezwa.[16] Kwa maneno mengine, Mwenyezi Mungu, Allah, alikuwa ameweka jukumu juu ya Waislamu ambalo hawakuweza, katika kipindi kile, kulitekeleza. Lakini jibu hilo halijitoshelezi na wala halina mashiko kwani mwenyezi Mungu, Allah, kwa sifa yake ya kuwa Mjuzi wa Yote, asingeweza kuweka jukumu juu ya waja wake, jukumu ambalo Yeye Allah analijua fika kuwa hawaliwezi kulitekeleza.

Hivyo, aidha *Ukhalifa* haukuwa ni muhimu katika Uislamu, au ulikuwa ni muhimu katika uislamu bali haukuweza kutekelezwa. Ikiwa ni hivyo, basi tendo la kushindwa kuisimamisha upya *Khilafah*, ni tendo la dhambi ya pamoja, dhambi ambayo waumini watapaswa kuadhibiwa.

Kamati haikutilia kabisa maanani kuwa Waislamu mwaka 1926 walikuwa tayari wamo kwenye *Akhir al-Zaman*, na kuwa Ya'juj na Ma'juj (Gog na Magog) walikwishauibia Ummah wa Nabii Muhammad (rehma na amani juu yake) Taifa la *Khilafah* na *Dajjal* alikwishawafunga bao na kujinyakulia ushindi na kuhakikisha kuwa Khilafah haiweze kurudishwa upya.

Kufuatia swali la tatu (*Jinsi gani Khilafah itungwe / iundwe kimkataba?*) kamati ilijibu kama ifuatavyo:

1. "Kwa uteuzi wa *Khalifah* aliyetangulia.

2. "Kwa uteuzi wa jamii maalum ya Waislamu wenye sifa maalum za maamuzi mema na bora, kama vile *Ulama*, ma-*Amiri*, watu/viongozi mashuhuri wenye mwenendo mzuri na imara wa kidini, wanadharia na watawala wenye sifa na ujuzi wa masuala ya kidini.

[16] Kurasa 75 -76. Kwa kufanya hivyo, Kamati ilikuwa imeyaacha maoni ya Mu'tazilaiti ambao waliiona *Khilafah* kuwa si jambo lenye umuhimu kuwapi, na Khawarij ambao walikuwa na msimamo unaosema kuwa palikuwa hapana haja ya kurudisha *Ukhalifah*. Kamati pia iliamua kuyaacha maoni ya Shaikh Ali Abd al-Razaq, muhitimu wa Al-Azhar, ambaye aliwakilisha hoja, kwenye Makala iliyochapishwa Egypy, inayosema kuwa Ukhalifa si muhimu kwenye Uislamu. Mawazo na maoni yake yaliibua hisia kali na mshituko wa kutosha ndani ya Egypt.

3. “Kwa kutekwa na Muislamu hata ikiwa kama hatimizi sifa zilizotajwa.” [17]

Kuwakilishwa kwa Ripoti hii na Kamati ya Pili kulipelekea kutokea kwa mjadala muhimu na wa kusisimua baina ya Abd al-Aziz al-Effendi, Profesa wa ki-Tunisia ambaye alikuwa ni mmoja wa wajumbe waliowakilisha Iraqi, na Sheikh Muhammad al-Ahmadi al-Zawahiri, kiongozi wa wajumbe wa Egypt[18] kuhusu uwezekano wa utekelezaji wa kanuni za kinadharia za Kiislamu na umuhimu wa *Ijtihad*:

Thalibi Effendi:

> “Hakuna hata mtu mmoja ambaye anaweza kudiriki kupinga ukweli kuwa suala la *Khilafah* ni jambo muhimu kupita yote na jambo ambalo pia ni gumu kuliko yote kulitatua. Hivyo basi, napendekeza kuahirisha Kongamano hadi mwaka ujao ili tupate nafasi na muda wa kuliangalia kwa makini tatizo hili kwa kina na kwa mitazamo ya namna zote. Haitatosha kuliangalia tatizo hili kutoka upande mmoja tu wa kinadharia. Lazima kiasi fulani cha mtazamo tofauti kitiliwe maanani cha umuhimu wa mazingira na mahali, (na) na athari zilizoshinikizwa juu ya taasisi za Kiislamu na dola fulani ya kigeni zenye nguvu kubwa.”

Shekhe al-Zawahiri:

> “Katika kuchambua masuala ya kitheolojia ambayo yaliwakilishwa kwetu, hatukutaka kukimbilia kwenye *Ijtihad* na kuunda mafundisho mapya ya kiimani. Tulijiwekea kikomo na mipaka kwa kuhakikisha kuwa tunaangalia tu kanuni zinazofahamika na zilizokubalika ndani ya kanuni zilizopo za Uislamu. Juu ya suala la uwezekano wa utekelezaji wa kanuni hizi, ni juu yenu kuamua na kutangaza kuwa jambo hilo liko nje ya uwezo wetu.”

Thalibi Effendi:

> “Sipendekezi mafundisho mapya ya kiimani, wala *Ijtihad*. Ninachokitafuta hapa ni mawazo yenu. Ikiwa unathibitisha kanuni ambazo haziwezi kufinyangwa na kutekelezeka katika zama zetu, je mazingira yatakuwa yapi?”

Shekhe al-Zawahiri:

> “Ni hatari kwa Uislamu kuuliza suala la utekelezaji, katika zama moja na au kudai sivyo katika zama nyingine, za maamuzi ya *Shari'ah*. Tunaamini kuwa utekelezaji wa kanuni za kiujumla za kidini hazipaswi kuwekewa ubaguzi katika utekelezaji wake kwa lengo la madai ya kujali zama zilizopo, na tunaona kuwa hapana hali yoyote inayoruhusu kuundwa kwa vipengele vipya vinavyodaiwa kuwekwa kwa madai ya ulazima wa kukidhi matakwa muhimu ya zama hizi wala zozote zile zijazo.”[19]

---

[17] Revue, Op. cit., kurasa 76 – 77.
[18] Baadaye aliteuliwa kuwa Mkuu wa chuo cha Al-Azhar mnamo mwaka 1929.
[19] Revue, Op. cit., kurasa 77 – 78.

*Shekhe* al-Zawahiri alikuwa, bila ya shaka, na haki zote kusistiza kuwa *Shari'ah*, au sheria takatifu iliyopokelewa kwa wahyi ya Kiislamu, hairuhusu wala kuacha mwanya wa kuweka marekebisho ili kuenda na wakati na kukidhi haja za zama husika. *Shari'ah* lazima ibaki kwenye hali yake halisi kama ilivyopokelewa na isibadilishwe bila kujali kama waislamu wamejikuta wana hali inayowawezesha au kutowawezesha kuitimiza katika muda husika. Na hivyo basi, kwa *Shekhe* Zawahiri, kufufuliwa kwa *Khilafah* ni jukumu la kidini. Hapo alikuwa yuko sawa na sambamba kabisa na ukweli!

Thalibi Effendi naye alikuwa na haki zote za kuwakilisha swali, ambalo hakupata jibu lake, kuwa ikiwa kufufuliwa kwa *Khilafah* ni jukumu la kidini juu ya Waislamu, je, kukosa kwa Waislamu kutimiza jukumu hilo kutasababisha hukumu gani juu yao?

Upungufu wa kimsingi wa mtazamo wa *Shekhe* Zawahiri na ule wa Thalibi Effendi ni kukosa kwao kuona na kufuata matamshi ya mwenyezi Mungu, Allah katika Qur'ani ambamo Allah anasema kuwa ameiteremshia kila jumuiya ya kidini *Shari'ah* na pia *Minhaj* (au njia iliyo wazi).[20] Hivyo basi, kutokana na maagizo hayo ya Allah, ni kuwa pamoja na kuwapo kwa sheria iliyoteremshwa na kupokelewa kwa wahyi ambayo daima lazima ibaki kama ilivyo na inatupasa tuifuate kama vile ilivyoteremshwa, kitu ambacho Shekhe Zawahiri anakisema (akiwa yuko sahihi kabisa) lakini ziada ya hapo paliteremshwa pia *Minhaj*, ambamo fikra na uwezo wa kiakili wa binaadamu unaweza kujitosheleza kwa kujipanga katika mazingira yanayobadilika ili kuweza kuendana na Sheria Takatifu, nayo itekelezeke kama ilivyokusudiwa na Mwenyezi Mungu.

Suala la msingi lililobeba tatizo ambalo Kamati ya Pili na Kongamano kwa pamoja vilishindwa kulitambua na hivyo kushindwa kulipatia suluhisho, kitu ambacho kilipelekea Kongamano kushindwa kutimiza lengo lake, lilkuwa ni tatizo la kuiangalia upya tafsiri ya Uislamu wa jadi hususan mwelekeo wa Mfumo wa Maadili ya jamii ya Kiislamu (*Dar al-Islam*) na mtazamo wa Mfumo wake wa Kimataifa. Taasisi ya *Khilafah* haikuwa ikipatikana kwenye hali ya kuwa peke yake bila kuwapo kwa mazingira yaliyojitosheleza na kuimarisha kuwapo kwake. Ukhalifa ilikuwa ni sehemu ya *Dar al-Islam*. *Dar al-Islam* haikuwapo tena ilipofikia mwaka 1924. Haikuwapo pia hata Makkah na Madina. Ulimwengu wa Kiislamu ulikuwa umerudi nyuma na kufikia kiwango cha hali yake ya kabla ya *Hijri* ya historia yake.

## *Eskatolojia ya Kiislamu na kuvunjwa kwa Taifa la Khilafah*

Kwa kuwa Qur'ani inasema kuwa "inaelezea kila kitu / mambo yote"[21] wanazuoni wa Kiislamu walipaswa waelekeze fahamu zao kwenye Qur'ani ili kupata yale ambayo yangeweza kuelezea kuanguka na kurudi nyuma kwa *Khilafah* na *Dar al-Islam*. Hapo, Kongamano lingeweza kufaidika kutokana na maelezo hayo.

[20] Qur'ani, al-Maidah, 5:48

[21] Qur'ani, al-Nahl, 16:89

Hadi kufikia mwaka 1926, palikuwa pameshapita zaidi ya miaka 30 tangu Alama muhimu sana ya *Akhir al-Zaman*, inayotajwa kwenye Qur'ani, ilipojitokeza duniani. Alama hii ilikuwa ni kugunduliwa na kupatikana kwa mwili wa Fir'auni ambako kulibashiriwa kwenye *Surah Yunus:*

فَالْيَوْمَ نُنَجِّيكَ بِبَدَنِكَ لِتَكُونَ لِمَنْ خَلْفَكَ آيَةً ۚ وَإِنَّ كَثِيرًا مِّنَ
النَّاسِ عَنْ آيَاتِنَا لَغَافِلُونَ ﴿٩٢﴾

"[Hapana] lakini leo, basi, tutausitiri / tutaulinda mwili wako, ili (mwili huo) (pale utakapogunduliwa) uwe (kama) Ishara kwa ajili ya (watu) watakaokuja baada yako: Na hakika watu wengi wameghafilika na Ishara Zetu!

(Qur'ani, Yunus, 10:92)

Ubashiri huu huu unarudiwa tena sehemu nyingine ya Qur'ani:

وَنَادَىٰ فِرْعَوْنُ فِي قَوْمِهِ قَالَ يَا قَوْمِ أَلَيْسَ لِي مُلْكُ مِصْرَ وَهَٰذِهِ
الْأَنْهَارُ تَجْرِي مِن تَحْتِي ۖ أَفَلَا تُبْصِرُونَ ﴿٥١﴾

"Na Firauni alitoa tangazo kwa watu wake, akisema: "Enyi watu wangu! Kwani mimi sinao huu ufalme wa Misri, na hii mito inapita chini ya miguu yangu? Je! Hamwoni [kuwa mimi ni mungu wenu mkubwa]?

أَمْ أَنَا خَيْرٌ مِّنْ هَٰذَا الَّذِي هُوَ مَهِينٌ وَلَا يَكَادُ يُبِينُ ﴿٥٢﴾

"Je, mimi si bora Zaidi kuliko huyu aliye mnyonge, ambaye hata hawezi kusema jambo akaeleweka waziwazi? [anamaanisha nini]"

فَلَوْلَآ أُلْقِىَ عَلَيْهِ أَسْوِرَةٌ مِّن ذَهَبٍ أَوْ جَآءَ مَعَهُ ٱلْمَلَٰٓئِكَةُ
مُقْتَرِنِينَ ﴿٥٣﴾

“Basi mbona hakuvikwa vikuku vya dhahabu, au hawakuja Malaika wakiandamana pamoja naye?”

فَٱسْتَخَفَّ قَوْمَهُۥ فَأَطَاعُوهُ ۚ إِنَّهُمْ كَانُوا۟ قَوْمًا فَٰسِقِينَ ﴿٥٤﴾

“Basi aliwachezea watu wake, na wakamt'ii. Kwa hakika hao walikuwa watu wapotovu.”

فَلَمَّآ ءَاسَفُونَا ٱنتَقَمْنَا مِنْهُمْ فَأَغْرَقْنَٰهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٥٥﴾

“Walipo tukasirisha tuliwapatiliza tukawazamisha wote!”:

فَجَعَلْنَٰهُمْ سَلَفًا وَمَثَلًا لِّلْءَاخِرِينَ ﴿٥٦﴾

“Kisha tukawafanya kuwa watangulizi (waliopita) na mfano kwa (wale watu) wa baadaye.”

(Qur’ani, al-Zukhruf, 43:51-56)

Ni jambo linalofahamika na kukubalika takriban kote duniani kuwa mwili wa Fir’auni uliogunduliwa na Loret huko Thebes mwaka 1898 ni ule mwili wa Fir’auni ambaye alizamishwa kwa amri ya Mwenyezi Mungu ambayo inajulikana. Watu pekee ambao jambo hili na ukweli huu wanaonyesha dalili za kulikataa ni Wazayonisti.

Kabla ya mkao wa Kongamano la *Khilafah* la mwaka 1926 kutafuta suluhisho na majibu kufuatia kusitishwa kwa *Khilafah* ya wa-Ottomani, ikiwamo kusambaratishwa Abd al-Aziz ibn Saud kwa *Khilafah* ya ki-Arabu iliyodumu kwa muda mfupi ya Sharif Husain, wanazuoni wa Kiislamu walikuwa na muda wa takriban miaka 30, kabla ya kugunduliwa kwa mwili wa Fir’auni, ili kuweza kujibu maswali muhimu na mazito sana.

Laiti kama utaratibu mahususi wa usomaji na uchunguzi wa Qur'ani ungetumika kwenye kulifuatilia suala hili la Alama iliyotajwa kwenye Qur'ani ya *Akhir al-Zaman* (ikim., kugunduliwa na kupatikana kwa mwili wa Fir'auni), kungewapeleka wanazuoni wa Kiislamu kwenye somo la eskatolojia ya Kiislamu, ambamo wangekutana na maelezo ya ukweli wa hali halisi iliyowakabili kwenye Kongamano la mwaka 1926.

Je, ni Alama gani ambayo Mwenyezi Mungu Mtukufu anaizungumzia ambayo imo kwenye kuulinda kimaajabu mwili wa Fir'auni kwa miaka takriban 3000? Je, ni watu gani hao ambao wangekuja kipindi kijacho ambao kupatikana kwa mwili wa Fir'auni kungejumuisha onyo kubwa kuliko maonyo yote?

Mara moja tunaweza kuyaacha madai ambayo ni wazi kabisa hayatoshelezi, kuwa huu ulikuwa ni ubashiri ambao pindi utakapojitokeza, ulipaswa kutoa Ushahidi kwa binaadamu wote kuwa Mwenyezi Mungu ndiyo chanzo cha Qur'ani. La hasha. Qur'ani imelizungumzia suala hilo sehemu nyingine tofauti vizuri kabisa na kwa kujitosheleza vilivyo. Ajabu hili limekusudiwa kuleta uju mbe mwingine kuliko huo, au hata zaidi ya huo!

Maoni yetu ni kuwa ajabu hili linabeba ujumbe kuwa patatokea watu ambao watakuja baada ya Fir'auni, ikim., wakati wa kipindi cha *Akhir al-Zaman*, ambao kwa kuwa wataishi maisha yao kama vile alivyoishi Fir'auni, basi itawatokea kufa kama alivyokufa Fir'auni. Fir'auni alikufa baada ya amri ya Mwenyezi Mungu, na wakati anafikiwa na umauti, aliacha imani yake potofu na akaukubali Ukweli wa Uislamu (ikim., imani katika Mungu wa Abrahamu 'alaihi al-Salam'). Pamoja na kukubali kwake Ukweli wakati wa kifo chake, kukubali kwake hakukumsaidia chochote kwani bila kujali hilo, alikuwa ameshaandikiwa kwenda kwenye moto wa jahannamu:

وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا مُوسَىٰ بِـَٔايَٰتِنَا وَسُلْطَٰنٍ مُّبِينٍ ﴿٩٦﴾

"Na hakika tulimtuma Musa pamoja na Ishara zetu na uthibitisho ulio wazi [toka Kwetu]"

إِلَىٰ فِرْعَوْنَ وَمَلَإِيْهِۦ فَٱتَّبَعُوٓا۟ أَمْرَ فِرْعَوْنَ ۖ وَمَآ أَمْرُ فِرْعَوْنَ
بِرَشِيدٍ ﴿٩٧﴾

"Kwa Firauni na waheshimiwa wake. Lakini wao walifuata amri ya Firauni [pekee], na amri ya Firauni haikuwa yenye uwongofu."

يَقْدُمُ قَوْمَهُۥ يَوْمَ ٱلْقِيَـٰمَةِ فَأَوْرَدَهُمُ ٱلنَّارَ ۖ وَبِئْسَ ٱلْوِرْدُ
ٱلْمَوْرُودُ ﴿٩٨﴾

"[Hivyo basi] siku ya Qiyama atawatangulia watu wake [kama vile alivyowaongoza hapa duniani] na atawaingiza Motoni. Na muingio muovu ulioje huo!"

(Qur'ani, Hud, 11:96-98)

Onyo la Qur'ani ni kwa watu ambao watakuja baada ya Fir'auni na kuwa wataishi kama Fir'auni alivyoishi na matokeo yake watakufa kwa amri ya Mwenyezi Mungu kama Fir'auni alivyokufa – ikim., wataukubali Ukweli wa Uislamu wakati wa kukutwa na umauti, lakini kukubali kwao kwa huo Ukweli hakutowasaidia chochote nao pia watapewa adhabu ya moto wa Jahannamu. Ubashiri huu utatokea pale ambapo mwili wa Fir'auni utakapogunduliwa. Je, hawa ni watu gani?

Ukweli ni kuwa swali la kutaka kujua utambulisho wa hawa watu kumejumuishwa kwenye sehemu ya historia kubwa kabisa ambayo historia itaishia, na kupatikana kwa mwili wa Fir'auni, kunaashiria kwa mwanzo wa hesabu za siku kuelekea kwenye zama ambazo zitashuhudia kupatikana kurudiwa upya kwa kinyang'anyiro baina ya Fir'auni na Musa (alaihi al-Salam).

Tayari ulikuwa ukweli unaojulikana kuwa eskatolojia ya Kiislamu ilikwishatambua kurudi kimaajabu kwa Yesu, Masihi wa Kweli, kuwa ni tukio la kiroho linaloongozwa na Mwenyezi Mungu, tukio ambalo litashuhudia fainali na ushindi wa mwisho wa ukweli na haki dhidi ya uwongo, ugandamizaji na wapinzani dhidi ya Ukweli. Tukio hilo la kiroho ambalo litashuhudia kurejea kwa Yesu (alaihi al-Salam) pia litashuhudia kuangamizwa kwa watu katika namna kama ile ambayo watu wa Fir'auni na majeshi yake walivyoangamizwa, na wakati wa kuangamia kwao, wakiwa wanakufa watu hao wataukubali ukweli kama vile jinsi ambavyo Fir'auni alivyoukubali kabla hajafa. Je, watu hao ni watu gani?

Kwa bahati nzuri kwetu, Qur'ani inalijibu swali hilo:

وَقَوْلِهِمْ إِنَّا قَتَلْنَا ٱلْمَسِيحَ عِيسَى ٱبْنَ مَرْيَمَ رَسُولَ ٱللَّهِ وَمَا قَتَلُوهُ وَمَا
صَلَبُوهُ وَلَـٰكِن شُبِّهَ لَهُمْ ۚ وَإِنَّ ٱلَّذِينَ ٱخْتَلَفُوا۟ فِيهِ لَفِى شَكٍّ مِّنْهُ ۚ مَا لَهُم
بِهِۦ مِنْ عِلْمٍ إِلَّا ٱتِّبَاعَ ٱلظَّنِّ ۚ وَمَا قَتَلُوهُ يَقِينًۢا ﴿١٥٧﴾

“Na kwa kusema kwao (kwa kujisifu): Hakika sisi tumemuuwa Masihi Isa, mwana wa Maryamu, [anayedai kuwa] Mtume wa Mwenyezi Mungu - nao hawakumuuwa wala hawakumsulubu, bali walifananishiwa tu [ilionekana tu kwao kuwa wamemuua]. Na hakika wanao khitalifiana katika haya wamo katika shaka nayo[kubwa]. Wao hawana ujuzi nayo wowote, ila ni kufuata dhana tu. Kwa yakini wala hawakumuuwa:

بَل رَّفَعَهُ ٱللَّهُ إِلَيۡهِۚ وَكَانَ ٱللَّهُ عَزِيزًا حَكِيمٗا ١٥٨

“Hapana, bali Mwenyezi Mungu alimchukua Kwake, na hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu, Mwenye Hekima.”

وَإِن مِّنۡ أَهۡلِ ٱلۡكِتَٰبِ إِلَّا لَيُؤۡمِنَنَّ بِهِۦ قَبۡلَ مَوۡتِهِۦۖ وَيَوۡمَ ٱلۡقِيَٰمَةِ يَكُونُ
عَلَيۡهِمۡ شَهِيدٗا ١٥٩

“Na [pokeeni onyo] hakutakuwa katika Watu wa Kitabu [ikim., hapatokuwa hata na Myahudi mmoja atakayemkataa Yesu kama Masihi na Mtume wa Allah, na hapatokuwa hata na Mkristo mmoja atakayedai kuwa Yesu inabidi aabudiwe kama Mungu na kama mtoto wa Mungu] ila hakika watamuamini yeye [Yesu] [ikim., wakati atakaporejea tena kimaajabu] kabla ya kufa kwake. Naye Siku ya Qiyama atakuwa shahidi juu (dhidi) yao [Hivyo watakufa kifo kama kile cha Fir’auni]”

فَبِظُلۡمٖ مِّنَ ٱلَّذِينَ هَادُواْ حَرَّمۡنَا عَلَيۡهِمۡ طَيِّبَٰتٍ أُحِلَّتۡ لَهُمۡ
وَبِصَدِّهِمۡ عَن سَبِيلِ ٱللَّهِ كَثِيرٗا ١٦٠

Hivyo basi, kwa dhulma waliyotenda wafuasi wa imani ya Kiyahudi tuliwaharimishia baadhi ya vitu vizuri walivyo halalishiwa [kabla ya hapo]. Na [Tulifanya hivyo] kwa sababu ya wao mara nyingi kuiacha njia ya Mwenyezi Mungu,

وَأَخۡذِهِمُ ٱلرِّبَوٰاْ وَقَدۡ نُهُواْ عَنۡهُ وَأَكۡلِهِمۡ أَمۡوَٰلَ ٱلنَّاسِ بِٱلۡبَٰطِلِۚ وَأَعۡتَدۡنَا
لِلۡكَٰفِرِينَ مِنۡهُمۡ عَذَابًا أَلِيمٗا ١٦١

"Na [kwa] kuchukua kwao riba, nao wamekatazwa, na kula kwao mali ya watu kwa dhulma. Basi tumewaandalia makafiri [wanaoendelea kuukataa Ukweli] katika wao adhabu yenye uchungu."

(Qur'ani, al-Nisa, 4:157 – 161)

Aya hizo hapo juu kwanza zimewatambulisha watu wa Ahl al-Kitab, na kisha zimeendelea na kuwaelezea kwa kuwataja wazi kabisa kuwa hao ni Wayahudi. Hivyo basi kugunduliwa kwa mwili wa Fir'auni mnamo mwaka 1898 kulipaswa kuushituwe Ummah wa wanazuoni wa Kiislamu kuwa kuanzia hapo patajitokeza matukio katika dunia ambayo yatapelekea kurudiwa tena kwa tukio kubwa la aina yake sawa sawa na lile la Fir'auni na Musa (alihi al-Salam) katika mazingira ambayo yataishia kwa kurejea kwa Yesu (alaihi al-Salam). Hapo Wayahudi watapata pigo kubwa kama lile alilolipata Fir'auni. Matukio haya yanajuuisha kiini na moyo wa eskatolojia ya Kiislamu.

Matukio yalishaanza kujitokeza mwaka mmoja kabla ya kugunduliwa kwa mwili wa Fir'auni, matukio ambayo yalipaswa yaushituwe ulimwengu wa wanazuoni wa Kiislamu. Kongamano la kwanza la Wazayonisti lilifanyika mjini Basel, Uswisi kuanzia tarehe 29 hadi 31 ya Mwezi wa Nane, Mwaka 1897 na liliitishwa chini ya uenyekiti wa Theodor Herzl, mwanzilishi wa ushirika wa Wazayonisti. Makongamano ya pili na tatu pia yalifanyika kwenye mji huo huo wa Basel mnamo miaka 1898 na 1899. Sababu ya kuchaguliwa mji wa Basel ni kuwapo kwa upinzani mkubwa dhidi ya Wazayonisti kwenye jumuiya zilizokwisha kuwa zimejijenga sehemu nyingi zilizobaki za bara la Ulaya. Lakini mnamo mwaka 1900, Wazayonisti walifanikiwa kupata upenyo uliowaletea kukubalika wakati Kongamano lao la nne lilipofanyika mjini London, na kuanzia hapo waliweza kujipatia fursa ya kujijengea mazingira mazuri kwa kutumia mapokezi mazuri kwenye maoni ya jamii ya Wayahudi wa Uingereza.

Kongamano lilirudi tena Basel mwaka 1905 (la tano) na tena mwaka 1903 (la sita), na hadi wakati huo Herzl alikuwa amekwishakutana na Sultani Abdul Hamid kwenye mji wa Konstantinopol katika jitihada zake za kumtaka Sultani ashirikiane naye kwenye mpango wa Wazayonisti wa kuanzisha Taifa la Wayahudi ndani ya Palestina, juhudi ambazo hazikufanikiwa. Makongamano yaliyofuata yalifanyika Basel mwaka 1905 (la saba), The Hague mwaka 1907 (la nane) na Hamburg mwaka 1909 (la tisa). Palipatikana faraja ya kutosha kwenye Kongamano la Hamburg kwani mapinduzi ya 'Vijana wa Kituruki' dhidi ya Sultani wa ki-Ottomani ndani ya Taifa la Ottomani yaliashiria mafanikio ya malengo na ndoto za Wazayonisti. Palifanyika Makongamano mawili mjini Basel mwaka 1911 (la kumi) na Vienna mwaka 1913 (la kumi na moja) kabla ya kuibuka kwa Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia mwaka 1914.

Mara tu baada ya vita hiyo kuanza, Sharif Husain, ambaye alikwishakuwa mteja wa Wazayonisti wa Kiyahudi-Kikristo wa Uingereza, alitangaza kutoutambua utawala na mamlaka ya Taifa la wa-Ottomani, na kujinyakulia mamlaka na utawala wa Makkah na Madina na kuiweka miji hiyo chini ya himaya yake, baada ya kupewa rushwa ya paundi za Kiingereza milioni 7 kila mwaka.

Punde tu baada yah apo, serikali ya Uingereza ilitangaza Azimio la Balfour ambamo Uingereza iliitangazia wazi dunia sera zake zenye lengo la kuundwa kwa Taifa la Kiyahudi ndani ya Palestina. Na katika mwaka huo huo, Jenerali wa jeshi la Kiingereza, Allenby alilishinda jeshi la Ottomani na kuuteka mji wa Jerusalem. Ligi ya Mataifa ndipo ilipoikabidhi Uingereza jukumu la kuitawala Palestina.

Kushindwa kwa Taifa la wa-Ottomani kwenye Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia na baadaye kuvunjwa na kusitishwa kwa Khilafah kulikofanywa na 'Vijana wa Kituruki' hakukupaswa kuwe ni mambo ya kuwashangaza wanazuoni wa Kiislamu kwani ishara zake zote zilikuwa zinaelekea kule ambako ni eskatolijia ya Kiislamu peke yake ndiyo ilikuwa na uwezo wa kuyaelezea. Na maelezo yake ni kuwa haitowezekana kuirudisha Khilafah hadi sura ya muda wa mwisho wa historia uwe umemalizika na wale Wayahudi ambao ni wagandamizaji wapate pigo kama lile ambalo alilipata Fir'auni.

[Wasomaji nawasihi kuvipitia vitabu vyangu vyenye majina: '*Jerusalem katika Qur'ani'*, '*Surah al-Kahf na Zama za Kisasa'*, na '*Mtazamo wa Kiislamu kuhusu Gog na Magog katika Dunia ya Kisasa'* ili kupata maelezo ya ziada kuhusu somo hili. Kitabu cha nne chenye jina '*Mtazamo wa Kiislamu kuhusu Dajjal Mtume wa uongo au Anti-Christ'* bado kiko kwenye kutayarishwa.]

Eskatolojia ya Kiislamu ingeliongoza Kongamano kugundua kuwa dunia sasa hivi iko chini ya himaya ya Gog na Magog (Ya'juj na Ma'juj), na kadiri dunia itakapokuwa chini ya himaya ya mfumo wao, haitowezekana kuirudisha *Khilafah* halali na halisi kama ilivyokuwa kabla.

*Surah al-Kahf* ya Qur'ani ingelipatia Kongamano *Minhaj* au mkakati wa uanzishaji wa *Khilafah* ndogo ndogo, ambazo kupitia kwazo, Waislamu wangefanikiwa kuunda wingi wa *Jama'at* katika sehemu zote za dunia ya Kiislamu, kila moja ikiwa na *Amiri* / *Imam* wake, huku kila *Imam* akipokea *Bai'ah* kutoka kwa wanajumuiya wa *Jama'ah* yake na huku akiendesha kwa makini masuala ya *Jama'ah* kwa kiasi kikubwa iwezekanavyo, kwa namna ambayo inaendana na *Shari'ah*. Wakati wowote itakapopatikana fursa ya kuyaondoa mamlaka ya *Wahhabi wa Saudia* juu ya *Hejaz*, yaondolewe, na Waislamu warudishe uhuru wa kweli juu ya *Hejaz*, na ndipo itakapowezekana kwa *Dar al-Islam*, iliyoanzishwa na Mtume Muhammad mwenyewe (rehma na amani juu yake), irudishwe. *Amir* angeteuliwa

kuisimamia *Dar al-Islam*, na kila *Amir* mwingine yeyote aliyekuwa akiisimamia *Jama'ah* yake kote duniani angelazimika kutoa kiapo cha *Bai'ah* kwa *Amir* wa *Dar al-Islam*!

Ilikuwa ni amri ya Mtume (rehma na amani juu yake) kuwa ikiwa pana watu wawili na kila mmoja wao anadai kuwa ni *Amir* juu ya J*ama'ah* ya Waislamu, katika muda huo huo (ikim., katika *Dar al-Islam*), basi wa pili kati ya hao auawe.

Ni jambo lenye umuhimu wa juu sana kugundua kuwa aya ya Qur'ani:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا أَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ وَأُولِي الْأَمْرِ مِنْكُمْ ۖ فَإِنْ
تَنَازَعْتُمْ فِي شَيْءٍ فَرُدُّوهُ إِلَى اللَّهِ وَالرَّسُولِ إِنْ كُنْتُمْ تُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ
الْآخِرِ ۚ ذَٰلِكَ خَيْرٌ وَأَحْسَنُ تَأْوِيلًا ﴿٥٩﴾

"Enyi mlioamini, mumtii Allah [na kufuata amri zake] na mumtii Mtume wake [Allah] [na kufuata amri zake] na pia muwatii wale ambao wana mamlaka (waliyoyapata kisheria / kihalali) watokanao miongoni mwenu…"

(Qur'ani, al-Nisa, 4:59)

Amri hii haikuamrisha kumtii *yule* (ikim., mtu mmoja) ambaye ameshikilia madaraka. Badala yake imeamrisha utii kwa *wale* wenye madaraka. Hivyo basi Qur'ani wazi kabisa imetambua kuwa pana uwezekano wa kuwapo kwa viongozi wengi (wa mpito) katika *Ummah* katika kipindi kile ambapo hapatokuwa na *Dar al-Islam* na hali hiyo kupelekea kutowezekana kuchaguliwa kwa *Amir* mmoja kuiongoza *Dar al-Islam*.

Kamati ya Pili ilishindwa kuchunguza uwezekano huu na hivyo, kupelekea kwa Kongamano nalo kushindwa kufikia lengo lake. Ripoti ya Kamati ya Pili pia ilikuwa na hitilafu nyingine ambayo ni muhimu na ina uzito wa kutosha, hitilafu ambayo inajikita kwenye nadharia mahsusi ya Kiislamu ya kisiasa. Kwa mujibu wa Ripoti hiyo, *Khalifah* anachaguliwa aidha kwa '*uteuzi*' wa *Khalifah* aliyemtangulia, au mamlaka hayo ya *Khalifah* yanaweza kutwaliwa kwa *nguvu ikiwa ni matokeo ya kutekwa*.

Hilo halimo katika Qur'ani, na pia halimo katika *Sunnah* ya Mtume, na wala hakuna mfano wowote katika mlolongo wote wa ma-Khalifa wa *Rashidun* (*Khulafa al-Rashidun*) msingi wa aina yoyote unaoweza kuweka imani kuwa katika Uislamu uongozi unaweza

kupatikana kwa kuuteka au kwa uteuzi wa *Khalifah* aliyetangulia. Lakini ni vizuri kujifunza na kugundua kuwa pamoja na hayo, mara nyingi katika historia ya Uislamu na hata katika dunia ya kisasa ya Kiislamu tunawakuta viongozi wakiteuliwa kama viongozi kwa kuwa wanatokana na koo za kifalme au kupitia utekaji wa nguvu (utawala wa kisasa wa kijeshi unakuwa ni moja ya aina za 'utekaji' huo).

Vizazi vilivyofuata vya *Ulama* na wanazuoni wa Kiislamu walikosa kuelewa ukweli halisi wa kinachodaiwa kuwa ni uteuzi wa *Khalifah* wa pili, Umar, uliofanywa na *Khalifah* wa kwanza, Abu Bakr (*radhiallahu anhu*). Kwa hakika panajitokeza wasiwasi kuwa *Ulama* wengi wa *Sunni* waliitumia vibaya dhana hiyo katika wakati wao kwa karne kadhaa kwa kujenga nadharia ya kithiolojia ya baada-ya-tendo ili kutoa, kuweka na kujenga uhalali wa utawala wa ufalme kwa misingi ya ukoo wanaotokana nao. Ukweli ni kuwa Abu Bakr (*radhiallahu anhu*) alimteua Umar (*radhiallahu anhu*), si kwa sababu yeye kama *Khalifah* anayo au alikuwa na madaraka na mamlaka ya uteuzi, bali kwa sababu watu, ambao ndiyo wenye haki ya kumchagua *Khalifah* mpya, wao wenyewe kwa hiari yao, walimpa Abu Bakr (*radhiallahu anhu*) mamlaka hayo.

Ukweli ni kuwa *Ulama* walikuwa wamefanya kosa kubwa kwa kutoa tamko kuwa *Shari'ah* inaruhusu *Khalifah* aliye kwenye mamlaka ana ruksa ya kumchagua *Khalifah* anayefuata, na hivyo basi, hilo likapelekea kuwapa wote nafasi ya kufanya hivyo katika historia ya Ukhalifa, na kufikia hata leo hii, koo za kifalme kama vile Ummayyadi, Abbasidi, *Ukhalifa* wa Ottomani, ukoo wa Ufalme wa Saudi Arabia, ukoo wa ufalme wa Hashemite wa Jordan, ukoo wa ufalme wa Sharifian wa Moroko na wengineo wengi kwenye falme za Ghuba.

Juu ya yote hayo, ziada inayoongeza ubaya, *Ulama* baada ya kushauriana walipitisha azimio kuwa Abu Bakr, Umar, Uthman na Ali (Mwenyezi Mungu awarehemu wote) ni *Khulafa al-Rashiduun* (ma-*Khalifah* waliokuwa sawa kimuongozo), na hivyo basi kuthibitisha kuwa palikuwa na tatizo fulani kwenye *Ukhalifah* wa Muawiya na wengine waliomfuatia. Kinachoshangaza kuhusiana na *Ukhalifah* wa hao ma-*Khalifah* wanne wa mwanzo, ni kukosekana kabisa kwa hata kuwapo wazo tu wala tetesi ya kuwapo kwa uongozi/ufalme kwa ukoo au kujinyakulia mamlaka kwa kuteka kwa kutumia nguvu za kijeshi. [Tunafahamu kuwa kuna wale ambao hawaridhishwi na uamuzi huo uliopitishwa na *Ulama* kwa kufunga na kulivuta chini pazia la ma-*Khalifah* wanaochukuliwa kuwa ni walio sawa kimuongozo (*Khulafa al-Rashidoon*) baada ya kifo cha Ali (radhiallahu anhu). Wanadai kuwa Muawiya naye pia aingizwe kwenye listi hiyo. Hata hivyo, wenye kudai hivyo, ni wachache sana, na tuna matumaini wanakwisha, miongoni mwa wasomi wa Kiislamu wa *Sunni*]

Matatizo waliyokutana nayo *Ulama* kwenye Kongamano la Kairo la mwaka 1926 yalikuwa, na inabidi bado yaendelee kuwa, chanzo cha wasiwasi mkubwa kwetu. Mwaka 1924, walipinga kuvunjwa kwa Khilafah ya Ottomani ambao kikweli ulikuwa ni utawala wa ukoo wa kifalme, ambao uliihamisha Khilafah kutoka kwenye ulimwengu wa ki-arabu na

hivyo kutengeneza mazingira ya kuanguka kwake. Wakati walipokutana mwaka 1926 hawakuweza kabisa kushituka, hata kwa uchunguzi na udadisi wa kifikra tu, kujaribu kubadili mfumo uisokuwa wa Kiislamu wa utawala kwa koo za kifalme uliokuwa ukiitwa *Khilafah* ya wa-Ottomani na badala yake kupendekeza utawala wa mfumo wa jumuiya ambao ungeenda sambamba na matakwa ya dini.

Aya ya msingi inayosimamia masuala yote yanayohusiana na uongozi kwenye Qur'ani katika mfumo wa Kiislamu inaeleza kuwa waislamu wanapaswa waendeshe mambo yao kwa misingi ya kushauriana:

"…na wanao mwitikia Mola wao Mlezi, na wakashika Sala, ***na [utawala wao katika mambo yao yote yanayowahusu] yakawa ni kwa kushauriana baina yao***, na kutokana na tulicho waruzuku wakawa wanatoa…"

(Qur'ani, al-Shurah, 42:38)

Kinachojitokeza baada ya kuipitia aya hii ni kuwa katika jumuiya ya Kiislamu kuchaguliwa au kuteuliwa kwa kiongozi na kuondolewa kwake na kuwekwa mwingine badala yake (kitu ambacho ni muhimu kuliko vyote katika masuala yanayowahusu waislamu wakiwa kama jumuiya inayotaka kuishi kwa pamoja) lazima kutekelezwe kwa kupitia mchakato wa kushauriana miongoni mwa waumini wote. Katika kuitambua haki ya *Khalifah* aliyeko madarakani kumteua *Khalifah* mrithi wa madaraka au haki ya madaraka ya *Khalifah* kunyakuliwa kwa kutekwa, *Ulama*[22] walikuwa wametenda tendo lenye kosa lililo wazi na linalopingana na Qur'ani kwa kuwa waumini walikuwa wananyang'anywa haki yao waliyopewa na Mwenyewe Mwenyezi Mungu, Allah.

Kwa hakika, waumini kwa kipindi chote cha historia ya *Ummah*, walipatwa na pigo jingine kubwa zaidi. Walipewa wito wa kuridhia na kukubali (ikichukuliwa kama kuwa ni wajibu wao wa kidini kupitia kiapo cha *Baiy'ah*) huku wito huo ukiwaletea majanga na maafa katika maisha yao, kwani uteuzi huo wa viongozi hao, wao wenyewe hawakuhusishwa kwa namna yoyote ile. Kwani ilikuwa wazi kuwa kukataa kuridhia uchaguzi / utezi huo kungechukuliwa kama ni kitendo cha kumkataa kiongozi huyo na hivyo basi kuwa ni tendo la wazi na tishio kwa *Khalifah* mhusika ambaye alikuwa tu na lengo la kuhalalisha utawala wake.[23] Ilikuwa kwenye kupinga uchafuzi huu wa dini ndipo mjukuu wa Mtume (rehma na amani juu yake), Imam Husain (radhiallahu anhu), kwa ushujaa mkubwa aliinua juu zaidi kiwango cha upinzani dhidi ya madai yasiyo halali ya *Bai'ah* kutoka kwa Yaziid, mtoto wa Amir Muawiyah (radhiallahu anhu).

---

[22] Msomaji anaelekezwa kupata mazingatio ya ziada ya kinachozungumzwa hapa kwa kupitia kutazama kwenye himaya kama zile za al-Mawardi (*al-Ahkam al-Sultaniyyah*), al-Ghazzali (*Ihya ulum al-Din*). Ili kupata maelezo kamili ya maoni ya Ulama tazama Arnold, T. Op. cit.

[23] *Khalifah* wa tano, Muawiyah, alimteua mwanawe, Yazid, kuwa *Khalifah* aliyemrithi madaraka hayo. Mjukuu wa Mtume, Husain, alipinga uhalali wa *Ukhalifah* wa Yazid na alilipa upinzani wake kwa kupoteza maisha yake kwa kuuawa. Hapakuwa na Waislamu wengi waliojali kufuata mfano wa Husain kwenye karne zilizofuata baada ya hapo.

Kutokana na upinzani wake, aliuawa na hivyo kufa kama Shahiid kwenye mbuga za Karbal. Na bado pana mapinduzi ambayo hayajamalizika Karbala ambayo yatakamilika kwa kuibuka kwa *Imam al-Mahdi* (alaihi al-Salam). *Ni jitihada za kuirudisha dini ilivyofundishwa na kujengwaw na Mtume wetu mbarikiwa, Muhammad (rehma na amani juu yake) ambayo ilichafuliwa na nguvu zinazopinga mapinduzi.*

Jibu la Kamati ya Pili kwa swali - Jinsi gani *Khilafah* itungwe kimkataba? – lilikuwa na kasoro kama ungeliangalia kwa mtazamo tofauti. Namna ya kwanza na ya tatu ya uteuzi wa *Khalifah* (kwa uteuzi na kwa kuteka), kama tulivyoonyesha hapo juu, zilikuwa zinapingana na Qur'ani na namna hizo zilikuwa hazina mifano ya kuiunga mkono katika *Sunnah* za Mtume na pia katika *Khulafa al Rashidoon*. Lakini, hata tukiangalia kwa mujibu wa namna ya pili ya uteuzi, ikiwa ni 'uchaguzi wa waumini', Kamati ya Pili ilishindwa kueleza kwa uwazi ni jinsi gani ingepaswa kufanywa ili namna hiyo ya uteuzi iweze kutimizwa mnamo mwaka 1926.

Mwishowe tunaweza kugundua wazi kuwa kutokana na mijadala ya Kamati ya Pili iliyofanyika *Ulama* wa Azhar, walionekana kuwa hawakufanya au hawakuweza kuyasoma vyema na kuielewa misingi na kanuni ya 'fikra mpya za kisasa', au labda hawakuweza kugundua sera na misingi kamili ya mfumo wa kisasa wa Kitaifa ambao ndiyo kwanza ulikuwa uko mbioni kulazimishwa kuingizwa kwenye dunia na jumuiya ya Kiislamu na hivyo basi baadaye kupelekea kuyateka nyara na kuufunga mwelekeo uliokuwapo wa mawazo, fikra na hisia za kisiasa za Kiislamu.

## *Kamati ya Tatu*

Kamati ya Tatu ilikuwa ni yenye mtazamo wa hali halisi kwenye mijadala yake na ilikuwa shupavu na kuweza kuweka wazi hitimisho lake ambalo kwa muhtasari lilisema kama ifuatavyo:

"... *Khilafah*... haiwezi kufufuliwa katika muda uliopo kutokana na hali ambayo Waislamu hivi sasa wamejikuta wamo.[24] Sababu zilikuwa:

"... kwanza kabisa bado hakuna chombo ambacho kinatambulika kinachojumuisha watu ambao wamepewa mamlaka maalum ya kisheria kufanya malipo ya utii na kujishirikisha (*Baiy'ah*.")[25]

Kamati ya Tatu hapa ilikuwa ikikiri kuwa mfumo halisi wa utekelezaji wa matakwa ya jumuiya (*Ahl al-Halli wal-Aqd*) ambao ndiyo ungepaswa kutumika katika utekelezaji wa matakwa ya wanajumuiya, ulikuwa haupo na haufanyi tena kazi mwaka 1926.

---

[24] Revue, Op. cit. ukurasa 103.

[25] Ibid. ukurasa 108. Ripoti kamili ya Kamati ya Tatu inapatikana kwenye Uchambuzi, Op. cit. Kiambatanishi cha 4, kurasa 578 – 581.

Kamati ingekuwa wazi na yenye ukweli zaidi kama pia ingekiri kuwa mfumo huo halisi wa utekelezaji wa matakwa ya jumuiya kwa ufupi haukuwahi kutumika kwenye historia ya Uislamu. Hata hivyo Kamati ya Tatu ilikuwa wazi na kweli kwa kuweza kukiri zaidi kuwa:

"... *Khilafah*, kwa mujibu wa Sheria za Kiislamu na kwa mujibu wa maana halisi ya istilahi (*Khalifah*), ulipatikana kwenye Uislamu wa awali peke yake." [26]

Kamati ilitamka kuwa Kongamano limejaribu kuwakusanya mjini Kairo wajumbe wanaowakilisha Waislamu wote wa dunia nzima na kuwapa jukumu la kujaribu kuufufua na kumchagua *Khalifah* mpya. Kamati ya Tatu ilielezea kuwa, pamoja na yote, Kongamano hilo halikuweza kudai kuwakilisha waislamu wa dunia nzima kwa kuwa kulikuwa na sehemu muhimu za dunia ya Kiislamu ambazo hazikuleta wawakilishi wake. Kinachosemwa hapa kwenye kauli hii, inachotubidi tukigundue, ni kuwa kama Kongamano lingefanikiwa kujumuisha wajumbe na wawakilishi kutoka sehemu zote duniani zenye Waislamu, basi lingeweza kuchagua *Khalifah* mpya. Hili, ukiachilia mbali ukweli kuwa uchaguzi huo ungekuwa ni wa kwanza na wa namna yake kihistoria kwa muda wote wa kuwapo kwa Uislamu, bali, na cha kukusisimua zaidi miongoni mwa sababu zilizowekwa wazi na Kamati ya Tatu kilichofanya uchaguzi huo wa *Khalifah* mpya usiweze kufanyika, ni ukweli kuwa:

"... *Khalifah*, kama atachaguliwa, hatoweza kutimiza wajibu wake wa msingi wa utekelezaji wa mamlaka yake juu ya *Dar al-Islam*. Sehemu nyingi za *Dar al-Islam* zilikuwa chini ya utawala wa kigeni. Na zile chache ambazo zilikuwa huru, zimetingwa na misukosuko ya kitaifa zenye nadharia za kizalendo ambazo zinapelekea kundi moja kutoukubali na kuupinga uongozi wa kundi la pili, bila kutaja kukubali uongozi huo kuingilia kati kwenye maamuzi ya masuala yao ya kijamii."[27]

Kamati ya Tatu haikuonyesha hata chembe ufahamu wa ukweli kuwa mfumo mzima wa kisiasa wa *Dar al-Islam* wenyewe ulikuwa chini ya mashambulizi maangamizi yaliyokuwa yakiendeshwa na mfumo wa kidunia wa kisasa wa kimagharibi usiomtambua Mungu, na *Dar al-Islam* ilikuwa njiani kuelekea kutoweka kabisa duniani kote.

Kilichokuwa kikishangaza ni ukweli kuwa sehemu fulani za dunia ya Kiislamu zilizokuwa chini ya utawala wa kigeni kuweza kuitwa *Dar al-Islam.* Kitendo pekee cha kuwa chini ya utawala na mamlaka ya kigeni kulipelekea sehemu hizo kutokuwa tena *Dar al-Islam* (na hii inatokana na maana halisi ya neno *Dar al-Islam* kulihitaji kuwa ni sehemu yoyote ya ardhi (eneo la nchi) ambamo sheria za mwenyezi Mungu, Allah zilikuwa zikipewa kiupaumbele, kutekelezwa, kutimizwa na kufuatwa na waumini). Pili, ikiwa *Khalifah* mmoja asingeweza kumiliki mamlaka ya kutawala sehemu zilizobaki za Jumuiya ya Kiislamu, jambo hili wala lisingekuwa jipya katika Uislamu.

---

[26] Ibid. ukurasa 106.

[27] Revue, Op. cit. ukurasa 106.

Na halikuwa jambo liliouzuia mfumo mzima wa *Ukhalifah* kutoweza kuwapo na kutimiza majukumu yake katika miaka elfu moja na mia tatu iliyotangulia hapo.

Ukweli ni kuwa Kamati ya Tatu ilipaswa itamke wazi kuwa miji ya Makkah na Madina ilikuwa chini ya utawala wa *Wahhabi wa Saudia*, na hivyo basi, *Khalifah* yeyote ambaye angechaguliwa, angekutwa na tatizo lisiloweza kupatiwa suluhu nyepesi na lisiloweza kujulikana jumla ya athari zake kwenye mamlaka yake, la kutokuwa na mamlaka ya kujumuisha utawala wake ndani ya *Haramain*. Katika kipindi ambacho kulikuwa hakuna *Khalifah*, na wadhifa huo ulikuwa ukipigwa vita, hivyo ilipaswa itiliwe mkazo mkubwa na uzito mkubwa zaidi uwekwe kwenye kipindo hicho, ili kuhakikisha kuwa yeyote atakayeteuliwa kubeba majukumu ya wadhifa huo, awe na mamlaka juu ya *Haramain*, na hivyo basi, hiyo kupelekea yeye kuwa ni kiongozi wa ibada nzima ya *Hajj*. Suala hili, ndilo hasa lilikuwa msingi wa madai na jitihada za Sharif al Husain kujitangaza yeye binafsi kuwa ni *Khalifah*.

Mtawala wa *Wahhabi wa Saudia* ambaye alikuwa na mamlaka juu ya *Haramain* alikuwa ameshadhihirisha kwa *Ummah* kwa vitendo kuwa yeye anawakilisha dola isiyotaka mzaha, na zaidi ya hilo, hakuonyesha dalili zozote kuwa ana nia wala mvuto wowote, na kudhihirika kuwa hana moyo kabisa juu ya suala la kurudishwa kwa *Khilafah.* Hapo basi ndipo lilipokuwa linajitokeza tatizo kubwa kuliko yote lililolikuta Kongamano la Kairo la *Khilafah.*

Kitu ambacho Kamati ingepaswa ikifanye, kitu ambacho haikukifanya, ilikuwa ni kufikia hitimisho jepesi na lililo wazi kuwa haiwezekani kuteuliwa *Khalifah* na kupata kutambuliwa na Waislamu wote duniani ilhali jumuiya ya kigeni ya Magharibi yenye nguvu kubwa ya Wazayonisti wa Kiyahudi-Kikristo ikiwa inadhibiti na kuunga mkono kisiasa na kijeshi kwa utawala wa Wahhabi wa Saudia ambao wana mamlaka juu *Haramain* na *Hajj*. Na jumuiya hiyo itaendelea kudhibiti na kuwa na uwezo wa ushawishi wa kisiasa kwenye maeneo hayo daima ilhali utawala wa Wahhabi utaendelea kuwa na mamlaka juu ya *Haramain*.

Kutokana na hali hiyo, jambo muhimu kuliko yote lililojitokeza baada ya uchambuzi huu kwa wakati ule, ilikuwa ni kutafuta njia na namna itakayoweza kukabiliana na diplomasia ya Kiingereza katika Ghuba na kuuondoa utawala wa ushirika wa mamlaka ya Wahhabi-Uingereza juu ya *Haramain* na *Hejaz* na hivyo basi kurudisha mamlaka hayo ya utawala wa *Haramain* kwa *Ummah* kwa kuirejesha *Khilafah.* Moja ya mambo ya mwanzo kabisa ambayo *Imam al-Mahdi* atafanya ni ukombozi wa *Haramain* na *Hajj* kutoka mikononi mwa mamlaka ya *Wahhabi wa Saudia*.

Ripoti ya Kamati ya Tatu iliwasihi wajumbe wa Kongamano wasikate tamaa kwa kushindwa kutimiza lengo lao la kutatua tatizo la *Khilafah* na kushindwa kumteua *Khalifah* mpya:

"Inatosha kabisa kutambua kuwa Kongamano limefanya jitihada kubwa na kutoa msaada mkubwa kwa Waislamu kwa kuweza kuuchambua kwa niaba yao ugonjwa na hivyo kuweza kuweka wazi dawa ya ugonjwa huo ambayo yanapaswa kufanyika kurekebisha hali hiyo isiyokubalika." [28]

Marekebisho yalikuwa ni mapendekezo kuwa:

"... Jumuiya za Kiislamu katika nchi zote za Kiislamu kwa pamoja wajiandae kutayarisha Makongamano ambayo yangewapa fursa ya kuweza kubadilishana mawazo kila yanapofanyika hadi watakapoweza kulitatua tatizo la Khilafah kwa mujibu wa sheria na kanuni za dini ya Kiislamu na kwa faida ya Uislamu." [29]

## *Maazimio ya Kongamano*

Kongamano lilisikitishwa na ripoti ya Kamati ya Tatu ambayo iliiona kuwa ni yenye mwelekeo wa kusikitisha na kukata tamaa. Ukweli ni kuwa *Shekhe* al-Zawahiri aliibandika jina ripoti hiyo na kuiita "*hotuba ya mazishi ya Uislamu*." Wajumbe ambao mwanzoni waliruhusu wananchi wa kawaida na waandishi wa habari kuhudhuria bila kipingamizi, hapa waliamua kuwa kifungu kimoja cha ripoti kisiruhusiwe kuonyeshwa kwa waandishi wa habari.**[30]** *Shekhe* al-Zawahiri, ambaye alikuwa akiongoza upinzani dhidi ya ripoti ya Kamati ya Tatu aliwasilisha rasimu ya azimio ambayo ilipitishwa na kukubaliwa na Kongamano.**[31]** Azimio hilo lilithibitisha kuwa *Khilafah* inaweza kufufuliwa. Kongamano lingine litayarishwe ambamo jumuiya zote za Kiislamu zipate nafasi ya kuleta wawakilishi na Kongamano lichukuwe hatua muhimu zitakazohakikisha kuundwa upya kwa *Khilafah* na kutimiza matakwa na kanuni zote kwa mujibu wa *Shari'ah*. Kwa ufupi, Kongamano hilo lingemteua Khalifah mpya.

Kongamano liliisha baada ya kupitisha muswada huu wenye kuleta matumaini. Kamati ya Tatu, baada ya 'kupigiwa kura ya turufu' ya kukataa ripoti yake na Kongamano kupitisha azimio hilo, ilijikuta ikitetewa na hali halisi ya matukio baada ya Kongamano, kwani Kongamano hilo lililotarajiwa kuitishwa na kumchagua *Khalifah* mpya halikutokea tena. Dunia ya Kiislamu, kwa ufupi, ilikuwa ikiingia kwenye kipindi kipya tunachoweza kukiita 'baada ya - *Khilafah*' cha historia yake. Ikumbukwe kuwa pingamizi la msingi la kutoweza kuwapo kwa nafasi hiyo, ni utawala wa *Wahhabi wa Saudia* juu ya *Hejaz na*

---

[28] Revue, Op. cit. ukurasa 106.

[29] Ibi. Ukurasa 107.

[30] Ibara hii inapatikana kwenye Revue, Op. cit. ukurasa 108, "De ce qui procede…" na kwenye Uchambuzi, Op. cit.., ukurasa 580, "Hivyo kutokana na maelezo yah apo juu…"

[31] Maandishi ya Revue, Op. cit., ukurasa 118; Uchambuzi, Op. cit., kurasa 89-90.

*Haramain*, na hatimaye kuundwa kwa Serikali ya kitaifa ya *Wahhabi wa Saudia* ikiwa kama 'nchi mteja' wa ulimwengu wa ki-Magharibi wa Wazayonisti wa Kiyahudi-Kikristo usiomtambua mungu.

Hadi pale ambapo vumbi lililotimuliwa lilipotua kuhusiana na wito wa Chuo Kikuu cha *Al-Azhar* katika jitihada zake za kujibu matokeo ya kusitishwa kwa *Khilafah* wa Ottomani, hali ilionyesha wazi kuwa upinzani wa Waingereza wakijumuika na mkakati wa Wazayonisti wa Kiyahudi ulikuwa umezaa matunda mazuri kwao na kuwapa ushindi dhidi ya Waislamu kwani palikuwa pamezaliwa hali mpya: Uislamu baada ya-*Khilafah!*

۞۞۞

# Sura ya Nne

## *Ulaghai wa Utawala wa Wahhabi wa Saudia ukijifanya ni Mbadala wa Utawala na Mamlaka ya Khilafah ya Kiislamu*

"Siyo jambo ambalo lilikuwa likiwasumbua ya kwamba mfumo wa nchi za Kitaifa, ambao ni zao jipya la utamaduni wa kimagharibi usiomtambua Mungu, na ambao ulijumuisha misingi ya mfumo mpya wa jumuiya zisizomtambua Mungu, ulikuwa unapingana wazi kabisa na Mfumo wa Kijamii za Kiislamu unaotokana na *Shari'ah*. Kilichokuwa muhimu kwao ni ukweli kuwa mfumo wa Kiislamu wa nchi-Taifa ungeuweka utawala wa *Wahhabi wa Saudia* kwenye nafasi isiyoweza kuingilika juu ya mamlaka ya *Hejaz*. Hivyo basi Taifa la *Wahhabi* ambalo liliibuka na kupinga kwa nguvu zote mambo yote yaliyokuwa ni *Bid'ah* (ikim., ubunifu katika dini) hivi sasa, lenyewe, lilikuwa likipendekeza *Bid'ah* kubwa kuliko zote katika historia ya *Ummah* wa Kiislamu!

## *Kongamano la Kiislamu la Kimataifa la Makkah Mwezi wa Sita - Saba, mwaka 1926*

Kongamano la Kiislamu la Kimataifa ambalo lilifanyika Makkah mwezi wa Saba, Mwaka 1926, lilikuwa katika miongoni mwa chanzo cha kuitishwa kwake, kujadili athari zilizosababisha kusitishwa kwa *Khilafah* ya Ottomani katika Ghuba ya Uarabu (*Jaziratul 'arab*) na, hasa athari kwenye Nyumba ya ukoo wa Saud ambao ulikuwa ndiyo kwanza umeanzisha utawala wake juu ya Arabia.

Abdul Aziz ibn Saud alikuwa ameiteka upya Najd (ikim., jimbo mashariki mwa Arabia, ambako toka huko kungejitokeza, kutokana na bashira ya Mtume Muhammad, "pembe za Shetani") baada ya kufanya hivyo kinamna kwa mara ya kwanza alipoiteka Riyadh mnamo mwaka 1902. Lakini katika kujenga hoja za kisiasa kwa kuwapo kwa utawala (*raison d'etre*) ukoo wa Nyumba ya Saud kwa misingi ya itikadi za kidini za *Wahhabi wa Saudia*, ilikuwa haizuiliki kuwa *Najd ya Wahhabi*, lazima iipe changamoto *Hejaz*, popote ilipopata mwanya wa kufanya hivyo, ili kuhakikisha kuwa maeneo ya chimbuko la Uislamu yanawekwa chini ya itikadi (zinazoonekana kuenda sambamba na itikadi za *Wahhabi*) za imani ya kweli.

Lakini palikuwa na mpango wa *Wahhabi wa Saudia* ambao ulikuwa ni wa uovu mkubwa Zaidi ulioihusu *Hejaz*. Ushirika wao wa mwaka 1916 na Uingereza ulilazimika kuwekwa wazi kwa Mkataba ambao ulikamilishwa baina ya Saudia na Uingereza. Kama vile ambavyo wenzao wengi waliofuatia baadaye, *Wahhabi wa Saudia* waligundua kuwa njia inayowapeleka kwenye ushindi wa kijeshi na kisiasa kwenye bara la Arabia inapitia kwa Wazayonisti wa London (na baadaye wa Washington).

Na hawakusita kuvunja amri ya Allah iliyo kwenye Qur'ani ili kujihakikishia wanapaka siagi ya Wazayonisti wa Kiingereza kwenye mkate wao. Walikuwa tayari kutimiza matakwa waliyopangiwa na washirika wao Wazayonisti wa Kiingereza ya kuyachukua mamlaka juu ya *Hejaz* popote fursa itakapojitokeza na kuhakikisha kuwa hawatoi nafasi kwa yeyote mwingine kuwang'oa kutoka hapo. Waingereza walilazimika kulipia ushirika wao na *Wahhabi wa Saudia*. Bei ilikuwa paundi za Kiingereza 5000 (elfu tano) kila mwezi.

Fursa hiyo ilijitokeza wakati Husein bin Ali (Sharif wa Makkah aliyeteuliwa mwaka 1908 na *Khalifah* / Mtawala wa Ottomani), alipojinyakulia madaraka kutoka kwa Wa-Ottomani wa Uturuki na kujitangaza kuwa mtawala wa *Hejaz* mwaka 1916, ikiwa kama ni mkakati alioufanya pamoja na umoja na Mataifa Yaliyojijumuisha wakati wa Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia, hivyo basi, kulazimisha utawala wa ukoo wa Nyumba ya *Hashimite* ya Husain. Alipofanya hilo, alikuwa amewazuia *Wahhabi* kufanya ibada ya *Hajj*. Pamoja na tofauti za kiitikadi zilizokuwapo baina yake na *Wahhabi* ambazo alizitumia kuhalalisha uamuzi wake wa kuwazuia *Wahhabi* kufanya *Hajj*, al-Husain alikuwa akifahamu fika kuwa *Wahhabi* wa Najd walikuwa wakiwakilisha tishio kubwa kuliko yote kwa utawala wake juu ya *Hejaz.*

Husain alikuwa akiwasiliana kwa siri wakati wa vita (ikim., Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia) na serikali ya Uingereza kupitia kwa Balozi wa Uingereza nchini Egypt, McMohan. Alikuwa hapendezewi kabisa na mabadiliko yaliyokuwa yakitokea kwenye Uturuki yaw a-Ottomani kwa kuibuka kwa 'Vijana wa Kituruki' waliokuwa na msimamo wa kidunia usiomtambua Mungu. Alihisi kuwa muda ulikuwa umefika kwa Waarabu kujikwamua kutoka kwenye utawala wa wa-Ottomani na kuirejesha *Khilafah* ya kiarabu, na kukubali wito wa McMohan kwake wa kutoa msaada wa Waarabu kwenye vita.

Husain bin Ali akaamua kuasi, kwa kutangaza uhuru kutoka kwenye utawala wa wa-Ottomani na kujitawaza mwenyewe kuwa Mfalme wa Waarabu. Alitoa tamko hilo kwenye hotuba ndefu yenye hamasa kubwa aliyoitoa tarehe 27 mwezi wa Sita, 1916. (*Tazama hotuba kamili kwenye kiambatanisho nambari 3*). Hotuba ilikidhi hisia za Waislamu wengi kote duniani, lakini haikutaja kabisa wala kugusia kuisaliti amri ya Qur'ani ambayo inakataza kuingia kwenye ushirika na Wazayonisti wa Kiyahudi-Kikristo wa Uingereza (tazama Qur'ani, al-Maidah, 5:51). Pia, ilikidhi haja ya kuonyesha kutopendezeshwa na matendo ya wazalendo wenye msimamo mkali wa Kituruki (Kamati ya kupigania Umoja na maendeleo) ambao walikuwa wamechukua madaraka ya serikali kwenye Taifa la wa-Ottomani kwa

kusambaza kwa makusudi hisia hasi dhidi ya wa-Ottomani miongoni mwa Waarabu na hivyo basi kupanda mbegu kwa ajili ya ‘Mchipuko wa Kiarabu’ wa kwanza kushamiri.

Wanafunzi wa historia watakuta mambo mengi yatakayowapa fursa ya kuyatafakari kwa kina kwenye maandishi haya na mengine kama vile barua walizokuwa wakiandikiana baina ya Husain na serikali ya Uingereza (kupitia kwa Balozi wa Uingereza). Pia watakuta kiasi cha kutosha cha Ushahidi ambao utawafadhaisha kwa kugundua uovu, uongo na upotozeshaji wa makusudi kwenye tabia na mwenendo wa diplomasia ya Waingereza na Wafaransa kwenye kipindi hicho cha kusikitisha kwenye historia ya nyanja za kisiasa, kidiplomasia na kidini.

Wote wawili, yaani Husain na Ibn Saud walijiunga kwenye muungano na Uingereza wakati wa vita na, hiyo ilipelekea, Ibn Saud kushindwa kufanya jitihada zozote za kujaribu kuyachukua maeneo ya *Hejaz* wakati wote ambamo vita ilikuwa ikiendelea kupiganwa. Hata baada ya vita kuisha, ilikuwa ni kitendo chenye hekima kusubiri kidogo ili kuweza kuona je ni hatua gani *Khalifah* aliyekuwa Konstantinopol angekuwa tayari kuzichukua ili kurudisha mamlaka yake juu ya *Hejaz.*

Na pale ilipothibitika kuwa *Khilafah* imesitishwa, mnamo tarehe 7 Mwezi wa Tatu, 1924 ndipo muda ulikuwa umetimia ili kuweza kuelekeza majeshi yake dhidi ya Husain. Husain naye kwa upande wake alikuwa akiyafahamu fika haya yote, na hivyo basi jitihada zake za kujihakikishia kuungwa mkono na Waislamu waliobaki duniani dhidi ya Ibn Saud alizozifanya mnamo tarehe 7 Mwezi wa Tatu, 1924 (siku nne baada ya kuvunjwa Ukhalifa wa Ottomani) hazikuweza kuzaa matunda aliyoyatarajia.

Mwaka 1924 ulijitokeza kuwa mwaka wenye matukio makubwa na yenye athari za kutosha katika historia ya Uislamu. Kwani Ibn Saud alijibu tangazo la *Ukhalifa* wa Husain kwa kuishambulia *Hejaz*. Majeshi ya Najd ya Ibn Saud yaliiteka Taif mnamo tarehe 5, Mwezi wa Tisa, 1924, hatimaye Makkah mnamo tarehe 13, Mwezi wa Kumi na Madina mnamo tarehe 5, Mwezi wa Kumi na Mbili. Baada ya mwaka mmoja, mnamo tarehe 19, Mwezi wa Kumi na Mbili, 1925, Jeddah ilitekwa na *Khalifah* ‘asiyekuwa na bahati’ na ‘Mfalme wa Waarabu’ alikimbilia uhamishoni. Hapo haikuwa jambo la kushangaza wakati watu mashuhuri wa Makkah walipomtangaza Ibn Saud kuwa Mfalme wa *Hejaz*.

Hivyo basi, ‘Mchipuko wa Kiarabu’ wa kwanza uliopangwa na Wazayonisti ukawa umekamilika kwa ushindi na kuweza kukamilisha malengo yake.

*Jaziratul arab*, ambayo hadi hapo ikawa imeungana chini ya utawala wa *Wahhabi wa Saudia*, takriban mara moja ilianza kulazimisha madai ya kuwa kiongozi wa *Ummah* na, katika kufanya hivyo, iliziba mwanya kwa kuweka mfumo mbadala wa umoja wa Waislamu usiokuwa ule wa mfumo wa *Khilafah*, kwa hekima, njia ya mshikamano ndani ya umoja wa kitaifa uliomo ndani ya mfumo wa mataifa huru ya Serikali za kitaifa. *Dajjal* akawa tayari yumo safarini kuelekea kwenye ushindi.

Watawala wa *Hejaz* wa *ki-Wahhabi wa Saudia* walikuwa wakifahamu fika kuwa Ulimwengu wa Kiislamu usingekuwa tayari kuubali utawala wao juu ya *Hejaz*. Hivyo basi hilo lilisababisha kutoweza kukubalika kwa *Khilafah ya Wahhabi wa Saudia*. Kwa upande wa pili, kama Waislamu waliobaki wa dunia nzima wangeweza kukusanyika pamoja na kumchagua *Khalifah*, basi hilo lingekuwa jambo la hatari sana na tishio kubwa kwa utawala wa *Wahhabi wa Saudia* juu ya *Hejaz*. Hiyo ingeweza kupelekea kutokea kwa marudio ya matukio yaliyojitokeza karne moja kabla ya hapo wakati *Wahhabi* walipoondolewa kwa nguvu kutoka *Hejaz* na jeshi lililotumwa kutoka Egypt.

Ikiwa ni matokeo ya khofu ya madhara yaliyokuwa yakijiri ya Kongamano la Kairo la *Khilafah* la Mwezi wa Tano, 1926, *Wahhabi wa Saudia* walianza kutafuta suluhisho la mfumo mbadala wa kisiasa na jukwaa jipya badala ya *Khilafah*. Jibu walilipata ndani ya mfumo wa Serikali za kitaifa za Kiislamu na ushirikiano na mshikamano wa Kimataifa wa nchi za Kiislamu.[32] Misingi ya mfumo mpya ilikuwa tayari imeshawekwa, baada ya kurahisishwa kabisa kama vile kwa niaba ya *Wahhabi wa Saudia*, kwa kuundwa na Mustafa Kamal, kwa Jamhuri ya Uturuki ndani ya makazi ya *Khalifah*.

---

[32] Cf Faruqi, Kamal: Approaches to Muslim Unity – Namna ambazo Umoja wa Waislamu unaweza kupatikana. Pakistani Horizon. Toleo XXV, Na. 2, kurasa 3 -12 ambamo anazungumzia muundo huu mbadala wa Khilafah, au Pan-Islamism, ikiwa kama Uislamu kiujumla – ambao ungetegemea umoja unaojengwa na imani na mienendo ya kidini ya pamoja nay a aina moja miongoni mwa Waislamu mbalimbali. Faruqi, haangalii, hata hivyo, ukweli ulio wazi wa kuwa Khilafah ilijengwa kwa misingi na ilipata uhalali wake kutokana na imani hizo hizo na mienendo ya Waislamu.

Haikuwasumbua hata chembe ukweli kwamba mfumo wa Serikali za kitaifa, ulikuwa ni mfumo uliobuniwa na kuundwa na mataifa yenye sera za kidunia ya kimagharibi, ambao ulikuwa ni msingi wa kuunda mfumo mpya wa jamii za kidunia, usiyomtabua Mungu, na mfumo ambao wazi kabisa unapingana na kwenda kinyume na Mfumo wa Jamii wa Maadili wa Kiislamu unaoundwa kwa mujibu wa *Shariah*. Kilichokuwa muhimu kwao ni ukweli kuwa mfumo wa Kiislamu wa Serikali za kitaifa ungeuweka utawala wa Wahhabi wa Saudi juu ya *Hejaz* katika nafasi ambayo isingekuwa rahisi kuushambulia na kuuondoa. Taifa la Wahhabi ambalo lilikuwa limejenga hoja kubwa sana ya kupinga *Bid'ah* (ikimaanisha uvumbuzi wa mambo mapya katika dini), sasa, wenyewe ulikuwa mstari wa mbele katika kupendekeza *Bid'ah* kubwa kuliko zote katika historia ya *Ummah!*

Mkakati wa *Wahhabi wa Saudia* ulielekea kwenye kutayarisha Kongamano pinzani dhidi ya Kongamano la Ukhalifa la Mwezi wa Tano, 1926. Waliliita Kongamano lao *Mu'tamar al-Alam al-Islami* (Kongamano la Dunia la Kiislamu) na walilitayarisha Makkah mnamo Mwezi wa Saba, 1926 katika kipindi cha *Hajj*. Kutokana na njia na mifumo ya usafiri iliyokuwa katika kipindi hicho cha mwaka 1926, ingewawia vigumu kwa wajumbe kuweza kuhudhuria makongamano hayo yote mawili. Wasaudia hapo walikuwa wakifuma mpango wa ujanja wa kisiasa ambao ungeulazimisha ulimwengu wa Kiislamu kuamua kuhudhuria aidha Kongamano la Kairo tu au la Makkah peke yake. Isingewezekana kushiriki kwenye makongamano hayo yote mawili katika kipindi hicho. Kwa kuwa Kongamano la Makkah lilikuwa likifanyika wakati wa kipindi cha *Hajj*, kongamano hilo llilikuwa na nafasi kubwa zaidi ya kupata washiriki wengi zaidi.

Historia, siku moja itadhihirisha kiasi gani diplomasia ya Uingereza, pamoja na msaada wake wa kipesa uliotolewa kuhakikisha kuwa mpango wa kulihujumu Kongamano la Kairo unafanikiwa.

Sababu maalum ya Kongamano la Makkah ilikuwa ni kuhakikisha kuwa Mfumo wa Jamii wa Maadili wa Kiislamu unazikwa na badala yake unapitishwa mfumo mpya wa Serikali za kitaifa za Kiislamu. Ndani ya Mfumo mpya wa mataifa ya Kiislamu, *Wahhabi wa Saudia* wangetia jitihada zao kuhakikisha kuwa utawala wao juu ya *Hejaz* unatambuliwa.

Nyaraka za matayarisho ya Kongamano (*travaux preparatoire*) zinaonyesha kuwa, pamoja na hayo, kiongozi huyo wa Saudia alijionyesha kwa waalikwa wote kuwa yeye ni 'mpiganiaji bingwa' wa Uislamu na aliahidi kuurudisha Uislamu wa kweli na halisi kwenye *Jaziratul Arab*.

*Wahhabi*, kama tulivyodokeza awali, walikuwa wakifahamu fika kuwa ulimwengu wa Kiislamu usingewakubali wao kumteua Khalifah atakayetokana miongoni mwao. Lakini kabla ya hapo, Muhammad Abdul Wahab mwenyewe alikuwa ameshaathirika na mawazo ya yule mwanataaluma wa Kiislamu, Imam ibn Taimiyyah. Msimamo wao ulikuwa kwamba *Khilafah*, kwa kuwa haukuteuliwa kwa kufuata misingi yake makhsusi, ilikuwa yenyewe ikitumika kama chombo kinachovunja umoja wa *Ummah*. Hivyo basi, Ukhalifa hauwezi

kuwa ni alama na msingi wa umoja wa Waislamu. Jukumu hili lazima likabidhiwe kwa *Shari'ah*.

Hvyo basi, ilikuwa ni jambo la kulitegemea, kuwa *Wahhabi Najd* na *Hejaz* zilizokuwa zimehimiliwa na *Wahhabi* kutoonyesha aina yoyote ya nia wala mvuto wa kutaka kuhudhuria Kongamano la Kairo. Pamoja na ukweli kuwa ni punde tu walikuwa wamejinyakulia nafasi muhimu ya mamlaka juu ya maeneo ambayo ni chimbuko la Uislamu, ni jambo rahisi kutabirika kuwa uongozi wa *Wahhabi* ungeitumia nafasi iliyojitokeza kwa kuvunjwa kwa Ukhalifa wa Ottomani na pia kuangamizwa kwa Khalifa wa ukoo wa Sharifu (al-Husain), aliyedumu kwa kipindi kifupi tu, kuupeleka *Ummah* kwenye mtazamo mpya kuhusu umoja.[33]

Pia ukweli kwamba tarehe iliyochaguliwa kufanyika Kongamano la Makkah aliloliita Kongamano la Dunia la Kiislamu ilikuwa ni Mwezi wa Sita-Saba 1926 (ikiwa ni mwezi mmoja tu baada ya Kongamano la Kairo) ilionyesha wazi kuwa Kongamano lilikuwa likitayarishwa kama mbadala au upinzani wa Kongamano la *Khilafah* la Kairo.

Palikuwa na sababu nyingine tena ya ziada iliyopelekea uamuzi wa kuandaa Kongamano la Makkah. Ibn Saud alitaka kupata kutambulika kwa mamlaka yake juu ya ardhi iliyokuwa ni chimbuko la Uislamu na jumuiya ya Kiislamu ya dunia nzima. Hili lilikuwa jambo lenye umuhimu mkubwa na wa aina yake kwani palikuwa na tofauti za kutosha za kiitikadi za kidini baina ya *Wahhabi* na dunia iliyobaki ya Kiislamu. Mojawapo ya tofauti hizo ni ukweli kwamba *Wahhabi* wanafuata mafunzo ya *Hanbali* ya sheria za Kiislamu na kwa namba ni wachache sana katika jumla ya jumuiya nzima ya Waislamu ambao wengi zaidi ni wafuasi wa mafunzo ya sheria za Kiislamu za *Hanafi, Shafei* na *Maliki*.[34]

Ikumbukwe kuwa wakati *Wahhabi* walipojinyakulia mamlaka juu ya *Hejaz*, japo ilikuwa kwa muda mfupi tu, mnamo karne ya 18, walisababisha maafa na umwagaji damu mkubwa sana, kutokana na msimamo wao wa kiitikadi na siasa kali. Tukio hilo lilisababisha kuenea kwa hisia mbaya, hasira na kutopendeza kwa msimamo wao miongoni mwa Waislamu wa dunia nzima na jeshi la Egypt lilitumwa kuingia *Hejaz* na kuwashinda na kusababisha waliobaki kukimbilia jangwani. Hii mara ya pili, *Wahhabi* walijizatiti kuhakikisha kuwa jumuiya ya Kiislamu inautambua utawala wao juu ya ardhi hiyo ya *Hejaz* na *Haramain*.[35] Hili lilikuwa ni lengo kuu la pili la Kongamano la Dunia la Kiislamu.

---

[33] Faruki, Op. cit., kurasa 3 – 12

[34] Sunni wanatambua na kuwakubali hao ma-Imamu wote wanne kuwa misimamo yao ina uzito sawa sawa.

[35] Hadi kufikia tukio la Mapinduzi ya Iran, Wahhabi wa Saudia walikwishafanikiwa kupata kutambuliwa na serikali zote zilizokuwa zikitawala kwenye mataifa ya Kiislamu. Miongoni mwa Waislamu wa kawaida, hata hivyo, bado pana hisia za kutosha za kutoridhishwa na hali iliyopo.

# *Wajumbe wa Kongamano*

Kongamano la Dunia la Kiislamu lilifanyika Makkah mnamo mwezi wa Sita, Mwaka 1926 kufuatia jitihada za Ibn Saud, na lilitambulika kuwa ulikuwa ni mkutano wa kwanza wa aina yake katika historia ya Uislamu. Ibn Saud mwenyewe aliliita hivyo katika hotuba yake ya ufunguzi:

> "Ukiangalia kwa upande wa jinsi lilivyo na pia ukiangalia malengo yake, mkutano wenu bila ya shaka yoyote ni mkutano wa aina ya peke miongoni mwa matukio katika Uislamu."[36]

Kuanzia mwanzo, hili lilikusudiwa kuwa ni shirikisho la kudumu:

"Tunamuomba Mwenyezi Mungu atuwezeshe ili Kongamano lifanyike tena na tena kila mwaka (wakati wa Hajj)."[37]

Tofauti na Kongamano la Khilafah la Kairo, Kongamano la Makkah lilijumuisha wawakilishi wa kutosha na waliokuwa na hadhi kubwa. Jumuiya zote muhimu za Kiislamu na nchi zote huru za Kiislamu (isipokuwa Persia) ziliwakilishwa. Kutoka kwenye bara dogo la Asia ya Kusini ulikuja ujumbe wa hali ya juu wa mashirikisho yote muhimu ya Kiislamu. Kwa mfano, Said Sulaiman Nadvi aliongoza wajumbe waliowakilisha Shirikisho la Harakati za Ukhalifa la India.[38] Wajumbe wengine watatu kwenye timu hiyo walikuwa *Maulana* Muhammad Ali Jauhar, kaka yake *Maulana* Shaukat Ali, na mkwe wake, Shoaib Quraishi. Palikuwa na wajumbe walioongozwa na Sayyed Muhammad Kifayatullah wakiwakilisha Muungano wa *Ulama* wa India na ujumbe mwingine ulioongozwa na *Shekhe* Sanaullah wakiwakilisha *Ulama Ahl al-Hadith* wa India.

Mufti Mkuu wa Palestina, Sayyed Amin al-Husseini, aliongoza ujumbe wa Palestina, Jenerali Ghulam Jilani Khan, aliongoza ujumbe wa Afghanistani, Edib Saroit – aliongoza ujumbe wa Uturuki, Shekhe al-Zawahiri – aliongoza ujumbe wa Egypt na Reazuddin Fakhrudin – aliongoza ujumbe wa Waislamu wa Urusi. Pamoja na Fakhruddin, palikuwa na wajumbe kutoka Oufa, Astrakan, Kazan, Krimea, Siberia na Turkistan. Wajumbe wengine walikuja kutoka Java, Sudan, Najd, *Hejaz*, Yemen n.k.

Baadhi ya wajumbe walikuja kwenye Kongamano kwa mialiko maalum. Katika kundi

---

[36] Revue, Op. cit. ukurasa 128

[37] Ibid.

[38] Lilikuwa jambo la kushangaza kuona kuwa Shirikisho la Harakati kufufua Khilafah liliacha kuhudhuria Kongamano la Khilafah la Kairo la Mwezi wa Tano na badala yake kuhudhuria Kongamano la Dunia la Kiislamu la Mwezi wa Sita ambalo kwenye ajenda yake suala la Khilafah lilikuwa halipo.

hili walikuwamo *Shaikh* Rashid Rida, msomi maarufu wa ki-Siria ambaye alikuwa mwanafunzi wa *Shaikh* Muhammad Abdu, na pia Sardar Iqbal Ali Shah, msomi wa ki-Afghanistani ambaye alikuwa na makazi yake makuu London, ambaye alikuwa mwandishi wa mfululizo wa makala kuhusu kongamano kwa ajili ya wachapishaji wa Kiingereza.[39] Jumuiya muhimu ambazo hazikuleta wajumbe zilikuwa Persia, China, Sanusi wa Libya na maeneo yaliyobaki ya Maghreb.

Wajumbe wa Kongamano la Kairo na lile la Makkah pia walitofautiana katika namna nyingine iliyo muhimu. Wakati wajumbe wa Kairo hawakutambulika kama wawakilishi rasmi, kwani wote walikuja kama wawakilishi binafsi, hilo halikuwa hivyo kwa wajumbe wa Kongamano la Makkah. Kwenye Kongamano la Makkah, nchi na jumuiya za Kiislamu zilituma wajumbe rasmi, na kwa kufanya hivyo, walionyesha kulipenda zaidi Kongamano na jukwaa la Makkah, na hivyo basi, kuchagua mfumo na mtazamo mpya wa umoja. Hapa ndipo panapopatikana sababu nyepesi na ya kimsingi inayoelezea shirikisho la kisasa la dunia ya Kiislamu kama mfumo wa Serikali za Kitaifa, kwa ujanja: Jumuiya za Kiislamu bila hoja zimeuchagua mfumo huo kwa sababu mbili:

- Kwa sababu ya hali mbaya ya malengo ambayo Dunia ya Kiislamu ilikuwa ikiyakabili,
- Kwa kuwa *Ulama* hawakuweza kuieleza na kuifafanua kwa ufanisi misingi ya Mfumo wa Maadili ya Jumuiya ya Kiislamu (*Dar al-Islam*) na Kanuni za Kiislamu za Mfumo wa Kimataifa ambamo *Dar al-Islam* ilipatikana.
- Kushindwa kabisa kwa wanazuoni wa Kiislamu kuitumia Qur’ani kupenya na kuweza kuelewa hali halisi ya zama ambamo walikuwa wakiishi ambazo siyo tu ilikuwa nchi zote za Kiislamu ziko chini ya athari za mfumo wa Kiyahudi-Kikristo wa kikoloni, bali pia Jerusalem ilikuwa imekwishapotezwa kwa kuchukuliwa na Wazayonisti na Khilafah ikawa ndiyo kwanza imevunjwa. Maelezo, bila ya shaka, yalipatikana kwenye eskatolojia ya Kiislamu.

## *Mfalme na Kongamano*

Kongamano lilipangiwa kusikiliza hotuba mbili kutoka kwa Mfalme Abdul Aziz ibn Saud.

Hotuba ya kwanza ya ufunguzi wa Kongamano, Mfalme alizungumzia hali ya kusikitisha ya historia ya *Hejaz* iliyoishia kwa udikteta wa Husain ambaye, miongoni mwa madhambi mengine, aliiweka *Hejaz* chini ya “athari za kigeni za wasiokuwa Waislamu.”[40] Kwa kuwa jambo hili lilikatazwa na Mtume Muhammad (rehma na amani juu yake), hapa palikuwa panapendekezwa uhalali wa mashambulizi ya Najdi juu ya *Hejaz*.

---

[39] Makala zake zingeweza kusomwa leo hii zingekuwa zinaleta msisimko mkubwa.

Matokeo ya mashambulizi hayo, Mfalme alikuwa na furaha kutangaza kuwa, hivi sasa *Hejaz* iko kwenye hali ya amani. Kongamano likakaribishwa kufanya vikao vyake katika hali ya amani na uhuru.Vikomo pekee vilivyowekewa Kongamano kutovizungumzia ni vikomo kwa mujibu wa Sheria za Kiislamu na "*kutojichanganya kwenye siasa za kimataifa au kwenye tofauti zinazowatenga baadhi ya Waislamu na serikali zao.*"[41] Hata hivyo, Ibn Saud hakuwa mkweli katika hotuba yake ya ufunguzi kwani naye pia alikuwa na makosa kama vile alivyokuwa na makosa Husain kwa kuzisaidia na kuziwezesha athari za Waingereza kuingia kwenye Ghuba. Alikuwa ni mteja wa serikali ya Uingereza ambaye alikuwa akipokea malipo ya paundi 5000 kila mwezi.

Mambo mawili yalijitokeza zaidi kwenye hotuba ya Mfalme. La kwanza, uongozi wa *Wahhabi* ulikuwa ukionyesha na kuutangaza uso wake kwa kuonyesha upande ulio mzuri kuliko pande zake zote ili kuweza kupata kuungwa mkono na Kongamano, kwa kuahidi 'amani/usalama' na 'uhuru bila kikomo'. Lakini, la pili, ambalo lilikuwa ni la muhimu zaidi, kutoruhusu kuzungumzia siasa za kimataifa kwenye majadiliano ya Kongamano kuliweka wazi viashiria kuwa usalama wa taifa la *Wahhabi* na nia yao ya kudumisha uhusiano na washirika wake (hususan Waingereza) kulipewa kiupambele dhidi ya mawazo ya *Ummah* bila kujali kama mawazo hayo yangejadiliwa katika mfumo wa *Shurah* kwenye Kongamano la Kiislamu, ilikuwa ni kitu ambacho 'hakijawahi kutokea' kwenye historia ya Uislamu.

Mfalme alilipa Kongamano 'kazi salama' ya *kutafakari ni jinsi gani hatua muhimu inabidi zichukuliwe kuhakikisha kuwa maeneo matakatifu yanakuwa vituo muhimu vya utamaduni na elimu za Kiislamu, pia maeneo hayo yanakuwa maeneo bora kuliko yote kimafanikio na usafi, na kuwa nchi ya Kiislamu inayojitofautisha kimuono kwa kuutambua Uislamu.*"[42].

Ilikuwa wazi kutokana na hotuba hii kuwa Mfalme alikuwa anajaribu kulilazimsha Kongamano liweke tenganisho bandia baina ya 'siasa' na 'dini' na kuunda nadharia mpya inayosisitiza kuwa mambo pekee ambayo Kongamano la Kiislamu linapaswa kuyajadili ni mwenendo wa 'dini' peke yake, na masuala ya 'kidini' tu. Hili nalo, lilikuwa ni jambo

lililopaswa kukosolewa kwa nguvu zote kwani lilikuwa kwa uhakika ni *Bid'ah* na wazi linapingana na Qur'an na *Sunnah* za Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) likipingana na misingi ya mila za Kiislamu.

---

[40] Inazungumzia kuhusishwa Husain na Waingereza.

[41] Revue, Op. cot. Kurasa 128 -131.

[42] Revue, Op. cit. Kurasa 128 -131

Kwa ufupi, Mfalme alikuwa akijaribu kubadilisha *al-Islam*, ambayo ilikuwa ni *al-Din*, na badala yake kuwa 'dini' katika maana yake iliyo finyu na iliyopotoka ambazo ndizo maana zinazotumika kwenye misamiati na uelewa wa tamaduni za kidunia za kimagharibi.

Mnano tarehe 2 Mwezi wa Saba, Mwaka 1926 ikiwa ni kikao cha 15 cha Kongamano, Mfalme alilihutubia tena Kongamano kwa mara ya pili, ambapo alijaribu kutimiza lengo la pili la mkakati wa *Wahhabi*, kwa ujanja, kutambuliwa na jumuiya ya Kimataifa ya Kiislamu na kutambulika kwa mamlaka ya *Wahhabi* juu ya *Hejaz.*

Mfame alifafanua *siasa* zake kuhusu *Hejaz* kama ifuatavyo:

1. "Haturuhusu nchi yoyote ya kigeni kuingilia kati kwa namna yoyote ile kwenye maeneo haya matakatifu.

2. "Haturuhusu upendeleo wa aina yoyote kwa jamii moja na kuwanyima jamii nyingine, chochote kitakachofanyika katika nchi hii lazima kiendane na matakwa na misingi ya *Shari'ah*.

3. "*Hejaz* lazima iwe na utawala usiofungamana na upande wowote. Nayo haipaswi kuingia vitani kama mshabuliaji au kushambuliwa, na nchi zote huru za Kiislamu lazima zihakikishe (dhamana ya) kutofungamana huko.

4. "Iko haja ya kuliangalia kwa kina suala la misaada ya kifedha ambayo *Hejaz* inapewa na nchi nyingi za Kiislamu, jinsi gani zigawanywe na (umuhimu wa kuhakikisha kuwa) zinasaidia maeneo matakatifu."[43]

Kitu ambacho Mfalme alikuwa akijaribu kukifanya hapa katika hotuba hii, ilikuwa si kingine bali ni kupendekeza sera mpya za kisiasa za Kiislamu. Ilikuwa kama vile *Wahhabi wa Saudia* walikuwa wakiamini kuwa wao ndiyo Waislamu pekee, hivyo *Hejaz* na *Najd* (kwa sasa Saudi Arabia) zilizokuwa chini ya utawala wao, zilikuwa ni *Dar al-Islam* halisi. Hivyo, maeneo yote nje ya *Hejaz* na *Najd* ni maeneo ya 'kigeni.' Na Mfalme alipokuwa akizungumzia mahitaji ya kuzuia 'wageni' kuingilia kati katika *Hejaz*, alikuwa akimaanisha uingiliaji kati uliotokea takriban karne moja kabla. Katika kuutaja *Ummah* wote wa Kiislamu nje ya *Hejaz* na *Najd* kuwa ni 'wageni', Mfalme alikuwa karibu sana na kutenda tendo la *Kufr*.

Wazo la pili alilolizungumzia, bila ya shaka, lilikuwa jambo la kupendeza, ikimaanisha, utekelezaji wa vipengele vya *Shari'ah* bila ubaguzi wala upendeleaji. Isipokuwa, wazo la pili

---

[43] Revue, Op. cit.

lilikuwa linapingana na wazo la kwanza. Ulimwengu wa Kiislamu ulikuwa ukibandikwa nembo ya 'ugeni', ambao, bila ya shaka yoyote, hawatoweza kutegemea kupewa haki ambazo zitakuwa wazi kwa *Wahhabi wa Saudia*. Wageni, kwa mfano, wangehitaji kupata viza ili waruhusiwe kuingia *Hejaz*, hata kwa lengo la kuja kufanya ibada ya *Hajj*. Wakati *Wahhabi wa Saudia* hawatohitaji viza kwa kuwa wao ni raia wa nchi mpya iliyokuwa inatarajiwa punde kuanzishwa ya Saudi Arabia, na hivyo basi, *Hejaz* ni mali yao, kama sehemu ya eneo la nchi yao. Waislamu ambao siyo raia wa Saudi Arabia, wangeweza kufungwa jela kwa kuzidisha muda wao waliopewa wa viza, kwani sasa walikuwa ni wageni, na *Hejaz*, ambayo sasa siyo tena *Dar al-Islam*, siyo mali yao tena, na hawana uhusiano nayo kwa namna yoyote ile japo nao ni Waislamu. Hapo hapo, *Wahhabi wa Saudia* wangeweza kubaki ndani ya *Hejaz* kwa kadiri ya mapenzi yao kwani sasa *Hejaz* ni mali yao.

Kwa ufupi, Mfalme alikuwa amevunja *Dar al-Islam* ambayo ilikuwa imeanzishwa na kujengwa na Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*), pamoja na masahaba wake, ndani ya *Hejaz*, na alikuwa amewanyang'anya Waislamu chimbuko la Uislamu, na pia akawa amewatukana Waislamu, na aliweza kuokoka pamoja na kufanya matendo hayo yaliyohitaji ujasiri wa aina yake kwa karibu miaka mia moja.

Waislamu wa India kwa miaka mingi walikuwa wakituma pesa kwenda Hejaz kuwasaidia ndugu zao katika Uislamu wa *Hejaz* kulipia gharama zao mbalimbali. Watu wa Makkah walikuwa masikini na hawakuwa na pesa za kutosha kujikimu na pia kugharimia mahitaji ya waumini waliokuwa wakija kuitembelea nyumba ya Allah. Uislamu ni familia na wale ambao wana uwezo, wanawasaidia wale ambao hawana uwezo. Kutokana na kitendo cha Wahhabi wa Saudia cha kuiteka nyara ardhi ambayo ni mali ya Waislamu wote, muda utatokea ambapo m-Pakistani mwenye asili ya India na muislamu wa ki-Bangladeshi watatendewa na kufanywa kama vile ni watumwa kwenye ardhi hiyo hiyo.

Jambo la tatu ambalo Mfalme alilizungumzia kwenye hotuba yake lilikuwa jambo la kustaajabisha mno. Pasingeweza kuwa na wasiwasi wa aina yoyote kuwa hilo lilikuwa ni jambo lililo wazi kuwa ni *Bid'ah*. Haikupatikana aidha kwenye Qur'ani, au kwenye *Sunnah* za Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) na pia kwenye historia nzima ya Uislamu, suala la *Hejaz* kutofungamana. Ukweli ni kuwa msemo na madai kuwa *Hejaz* isiweze kutangaza vita ni kuyatoa maeneo matakatifu na chimbuko la Uislamu kwenye *Jihad*, na hilo wazi kabisa ni jambo ambalo linapingana na amri za Qur'ani. Hapa pia, Mfalme alikuwa akijitembeza kwenye uchochoro wa *Kufr*.

Kufuatana na ombi la Mfalme kuwa nchi zote huru za Kiislamu lazima ziutambue utawala wa *Hejaz* 'kutofungamana' ilikuwa wazi kuwa Mfalme alikuwa akitumia ujanja

kuficha jaribio lake la kuweza kutambuliwa na Dunia ya Kiislamu kwa mamlaka ya *Wahhabi wa Saudia* juu ya *Hejaz*.

Kongamano liliijibu hotuna ya Mfalme kwa kutumia kwa busara na hekima uhuru wa majadiliano ambao Mfalme aliuruhusu. Wajumbe walitoa michango yao bila kusita na kwa

kuangalia tu kwa haraka ripoti ya hotuba za Kongamano, hapapatikani ishara zozote kuashiria kuwa utawala wa Mfalme na watayarishaji wa Kongamano walizuia uhuru wa kutoa michango hiyo. Mara chache, inaonekana kuwa Wajumbe wa *Hejaz* walijikuta wakishindwa hoja kwa kukosa kura za kutosha.[44]

Kwa ujumla, Kongamano liliheshimu mipaka iliyowekewa ya kutojiingiza kwenye siasa za kimataifa. Kufuatana na hilo, suala la *Khilafah* halikujadiliwa kabisa. Hili lilikuwa ni ushindi mkubwa kwa msimamo na mfumo mpya wa umoja wa Waislamu. Hata hivyo, Kongamano lilijiingiza kwenye siasa wakati linapitisha azimio lake[45] kudai kurudishiwa *Hejaz* mamlaka ya maeneo ya *Maan* na *Aqaba* baada ya maeneo hayo kunyakuliwa na Waingereza na kuwekwa chini ya *Transjordan* (ambamo Uingereza ilikuwa na mamlaka nayo) kwa kuwa tendo hilo, kwa mujibu wa Rashid Rida, lilikuwa linaenda kinyume na amri ya Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) kuwa Ghuba ya Uarabuni lazima isiingizwe kwenye himaya ya wasiokuwa Waislamu.[46]

Wakati Ibn Saud mwenyewe alipozileta *siasa* za kimataifa kwenye Kongamano kwa mapendekezo dhidi ya *Hejaz*, Kongamano liliyajadili mapendekezo hayo kwa kina na hatimaye kuonyesha msimamo wenye busara, uadilifu na imani halisi na kamili ya Uislamu wa kweli kwa kukataa kuyatambua mambo ambayo Mfalme aliyataka. Kongamano liliamua 'kuyasikia' matamshi ya Mfalme. Na uamuzi huu ulikuwa, labda, uamuzi mmoja wa aina yake ulio muhimu na uliochukuliwa na chombo kilichokuwa kikiuwakilisha *Ummah* katika kipindi kilichopita tangu kuangushwa kwa *Khilafah* ya wa-Ottomani.

---

[44] Kwa mfano, Kongamani lilipitisha uamuzi wa kujenga njia mbili za reli kutoka Jeddah hadi Makkah na kutoka Yanbu hadi Madina pamoja na kuwapo kwa pingamizi kutoka kwa wajumbe wa Hejaz "ambao walipinga kwa hoja za kidini ujengaji wa njia za reli kwenye nchi ambayo maisha yake yalitegemea usafiri wa ngamia" Revue, Op. cit. ukurasa wa 193. Tunabaki na hamu ya kutaka kujua ni jinsi gani Ulama wa ki-Saudia alijielezea pingamizi lake kuhusu ujengwaji wa reli kwa maudhui ya njia hiyo kuchukua nafasi ya njia ya usafiri ambayo Allah ameiumba. Utawala wa Saudia huenda ungegundua hatari ambayo kuingia kwa teknolojia za kisasa kuliashiria kwenye kuchukua nafasi ya usafiri wa asilia na pengine ingehakikisha kuweka nafasi yake pembeni ya njia hizo mpya.

[45] Maandishi ya Revue, Op. cit. kurasa 207 – 208. Egypt, Uturuki na Afghanistani hazikupiga kura.

[46] Kwa mujibu wa Toynbee: "moja ya matokeo ya vita ya 1914-1918 ilikuwa ni kuwaondoa Waturuki kutoka Arabia na kuongeza mipaka ya eneo lililo chini ya athari za moja kwa moja za Taifa la Uingereza kwenye Ghuba (Uchambuzi, Op. cit. ukurasa 272). Lakini pia ni muhimu kugundua kuwa mnamo ushindi huu wa aina yake usiokuwa wa kawaida wa Waingereza, ambamo ndani yake pia inapatikana kashfa na usaliti wa amri ya Mtume Muhammad (rehma na amani juu yake) kwa mara ya kwanza katika kipindi chote cha miaka elfu moja na mia tatu ya historia ya Uislamu, Waingereza walisaidiwa na kupewa ushirikiano na Hussain na Ibn Saud. Haina shaka kuwa wote wawili walidai malipo ya pesa katika kutoa huduma hiyo kwa Waingereza. Majeshi ya kiarabu ya Husain yalipigana vita dhidi ya Waturuki yakiwa upande wa Waingereza.

Hilo lilikuwa ni pigo kubwa kwa Ibn Saud na matokeo yake ikawa kuwa Kongamano lilidumaa kwa miaka 20 iliyofuatia hapo na halikuweza tena kukutana Makkah, kama ilivyokubaliwa kuwa litakutana kila mwaka mnamo kipindi cha *Hajj*.

Kuhusu suala la pili ambalo pia lilikuwa tete, Kongamano liliamua kuwa ni jambo la busara kukubaliana na matakwa ya mwenyeji wao. Ibn Saud alilitaarifu Kongamano kuwa, yeye akiwa kama ni mmoja wa viongozi wa Taifa la Kiislamu, japokuwa Waislamu wote wana uhuru wa kufanya ibada ndani ya maeneo matakatifu kwa mujibu wa mafunzo ya madhehebu zao, utawala wa *Wahhabi* hautoruhusu matendo yoyote ambayo yatakwenda kinyume na kanuni za *Shari'ah*. Suala hili lilisababisha moja ya mijadala mikali iliyokuwa na shika shika kubwa miongoni mwa wajumbe wa Kongamano. *Shaikh* al-Zawahiri alituliza hali kuwa shwari kwa kutoa pendekezo la rasimu ya muafaka ambayo iliruhusu uhuru wa ibada lakini haikuingilia kati masuala yenye utata, kwa mfano, masuala ya ukarabati wa makaburi ya masahaba wa Mtume ambayo yalikuwa yameharibiwa na *Wahhabi* n.k.

Suala hilo liliwapiga na kuwaumiza mioyo *Wahhabi*, japokuwa halikufuatiliwa na kuachwa kuwiva na kuwa mgogoro kamili, kwani wajumbe walitumia busara na subira kwa kutomshinikiza Ibn Saud kwa nguvu zote, hali iliyopelekea ujumbe wa India kuondoka huku wakiwa na hisia za uchungu mkubwa. Hii, inaelezea, kwa upande fulani, kwanini Kongamano halikuweza kukutana tena Makkah, kama ilivyokubaliwa.

---

Kutokujihusisha kwa makusudi kwa Ibn Saud kwenye harakati hizo kuliwaongezea Waingereza nafasi ya kupata ushindi. Hadi mwaka 1920 ambamo malipo yake ya kila mwezi yalisitishwa na Waingereza, Hussain alikuwa amepokea takriban paundi za Kiingereza milioni sita. Ibn Saud, ambaye pia alipokea kutoka kwenye Serikali hiyo hiyo ya Kiingereza kiasi cha paundi 350,000 ikiwa ni jumuisho la paundi 5000 kila mwezi, alitoa maelezo ya kifidhuli kwa kudai kuwa hayo ni malipo ya *Jizyah* (kodi inayolipwa na raia wasiokuwa Waislamu wanaoishi chini ya himaya ya Dar al-Islam). Uchambuzi, Op. cit. ukurasa 273. Ilikuwa ni nchi ya Uingereza (ambayo ilikuwa na mamlaka juu ya Transjordan) ambayo ilijinyakulia maeneo ya Maan na Aqaba na kuyaweka chini ya himaya yake mwaka 1925. Japokuwa Mfalme aliyekuwa hayupo madarakani wakati huo, Mfalme Husain, akiwa uhamishoni Cyprus alishutumu na kukilaani kitendo hicho, na Ibn Saud alilishauri Kongamano la Dunia la Kiislamu la Jeddah kupitisha tamko la kupinga kitendo hicho, mwenendo wa Waingereza wazi kabisa ulikuwa ni *fait accompli*. Ni jambo la msingi kugundua kuwa kama amri ya Mtume Muhammad (rehma na amani juu yake) isingevunjwa na Hussain na Ibn Saud kwenye kutoa kwao msaada kwa Waingereza kwa kudhani kuwa wanafanya jambo lenye manufaa la kuwaondoa wa-Ottomani kwenye Ghuba ya Arabia, isingewezekana kutimizwa kwa Tamko la Balfour na hatimaye pia isingewezekana kwa Taifa la Wazayonisti kuundwa ndani ya Palestina iliyokuwa chini ya Waislamu. Vizuri na muhimu kugundua kuwa kama *Aqaba* ingebaki chini ya mamlaka ya *Hejaz*, Saudi Arabia ingekuwa Taifa lililo mstari wa mbele kwenye machafuko ya Mashariki ya Kati. Historia huenda siku moja itadhihirisha kuwa moja ya sababu za Waingereza kuichukua miji ya *Maan* na *Aqaba* ilikuwa na lengo la kujenga ukanda wa kinga kati ya maeneo tete kiamani yaliyokuwa ni chimbuko la Uislamu na makazi ya Taifa ya Wayahudi ndani ya Palestina ambayo tamko la Balfour liliyakusudia kuyasimamia kuyaanzisha. Ieleweke wazi kuwa mapambano ya moja kwa moja baina ya *Hejaz* (sasa hivi Saudi Arabia) na makazi ya ki-Taifa ya Wayahudi Palestina (sasa hivi Taifa la Israeli) yangeibua hisia kali na ngumu kuzimudu, jambo ambalo bado linabaki kuwa ni tishio pekee kwenye kusalimika kwa Taifa la Wazayonisti.

Hatuwezi kukamilisha sura hii bila kuweka wazi ukweli kuwa Abdul Aziz ibn Saud hatimaye alifanikiwa kupata kukubalika kama mtawala na kukubalika utawala wa Saudia juu ya *Hejaz* kama alivyotaka. Alichobakisha kufanya ni kutangaza rasmi kuundwa kwa Taifa la Saudi Arabia na kuweka mahitaji ya viza za Saudia kuingia kwenye ardhi ya nchi hiyo – hata pale ambapo msafiri alikuwa akiingia hapo kwa nia ya ibada ya *Hajj.*

[Mwandishi huyu anajikuta amebaki peke yake kwenye kupinga kuikubali hii *Bid'ah*, na hivyo basi ametenga pesa zikiwa kwenye Dinari, pesa zinazohitajika kufanya safari ya ibada ya *Hajj*. Ikiwa atakufa kabla ya utawala wa *Wahhabi wa Saudia* juu ya *Hejaz* haujatupwa kwenye pipa la takataka la historia yake, anaomba ili siku hiyo kwa mara nyingine tena: "na wewe uko huru kwenye mji huu (ikim., Makkah)" (Qur'ani, al-Balad, 90:2) basi atokee mtu afanye ibada ya *Hajj* kwa niaba yake. Amin!]

Kwani ilikuwa ni kiongozi wa ujumbe wa Waislamu wa India, Maulana Shaukat Ali, ambaye ndiye aliyefanya jitihada kubwa na binafsi za kutayarisha mkutano mkubwa wa tatu wa Kiislamu, mnamo mwaka 1931, baada ya mikutano hiyo miwili ya mwaka 1926. Wala hakusita kuiruka Makkah na kuichagua Jerusalem kuwa ndiko mkutano ufanyike.

Miongoni mwa kazi nzuri zenye mafanikio mema ya Kongamano la Makkah ilihusu uboreshaji wa mazingira ya *Hajj*, usafiri (hususan reli ya *Hejaz*), huduma za afya, upatikanaji wa chakula na maji, na kinga kwa mahujaji dhidi ya unyonyaji. Haya yalikuwa masuala ambayo yaliwagusa mahujaji kila mwaka na kuhusu mambo hayo Kongamano liliyajadili kwa urefu na kwa kina na kupitisha maazimio mengi yaliyokuwa na tija.

۞۞۞

# Sura ya Tano

## *Ulimwengu wa zamani wa Kiislamu – Jaribio la mwisho la ufufuzi*

> Lakini Wayahudi asilia waliokuwa Jerusalem, ambao waliishi na kufanya shughuli zao mbali mbali huku wakiwa hawajihusishi kabisa na Wazayonisti, walilikaribisha Kongamano lilipoanza na kulitakia mafanikio mema. Walisema kuwa Wayahudi hawazihitaji sehemu tajatifu na hawakuwa na haki nazo, isipokuwa walilisihi Kongamano lisipinge desturi ya tangu zamani ya Wayahudi ya kusali na kumuomba Mungu kwenye Ukuta wa Kilio. Na Kongamano, lilifanya kadhalika.

## *Kongamano Kuu la Kiislamu la Jerusalem Mwezi wa Kumi na Mbili mwaka 1931*

Kwa kipindi kirefu cha miaka mitano baada ya mikutano hiyo miwili ya mwaka 1926, hapakuwa na jaribio lolote la msingi ambalo lilifanywa na jumuiya ya Kiislamu katika kutafuta suluhisho la kuanguka kwa *Khilafa* yakiwemo matukio mengine mazito yaliyokuwa yakijitokeza yenye changamoto za hatari ambayo yalikuwa yakiikumba dunia. Jitihada za pumzi za mwisho za kifo cha *Dar al-Islam* zilifanyika kwenye Kongamano Kuu la Kiislamu ambalo lilifanyika Jerusalem mwezi wa Kumi na Mbili, mwaka 1931, kufuatia jitihada za kitaifa kati ya India na Palestina.[47] Kongamano lilikuwa na lengo moyoni mwake la kurudisha kwa namna moja au nyingine mfano wa mfumo wenye uadilifu ndani yake ili kuokoa hali iliyokuwa ikizorota siku hadi siku baada ya kuvunjika kwa mfumo ulioachwa na Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*).

[47] Ni makosa kudai (kama jinsi Kongamano la Dunia la Kiislamu la Karachi hivi sasa linavyodai) kuwa Mkutano wa Kiislamu uliofanyika Jerusalem mwaka 1931 ulikuwa ni kikao cha pili cha Kongamano la Dunia la Kiislamu (ikieleweka kuwa la kwanza lilifanyika Makkah mwaka 1926). Kwanza, Kongamano la Jerusalem lilijichagulia jina tofauti na kujiita "Kongamano Kuu la Kiislamu" (al-Mu'tamar al-Islami al-Am). Pili, Kongamano lilijiwekea Malengo yake lenyewe, nayo yalikuwa tofauti na malengo ya Kongamano la Dunia la Kiislamu.

Hata hivyo Kongamano lilishindwa kupata suluhisho la aina yoyote. Kama Makongamano ya Kairo na Makkah, nalo lilionekana kufa wakati linazaliwa.

Kwa Mufti Mkuu wa Palestina, *Hajj* Amin al-Husaini, ukorofi wa Wazayonisti wa kuendelea kujinyakulia ardhi ya Palestina baina ya miaka 1926 na 1931 kulijitokeza kama ni tishio kwa Uislamu. Tishio hilo halikuweza kukabiliwa ila na umoja wa Waislamu wa dunia nzima. Uamuzi wa kulitayarisha Kongamano hilo Jerusalem, mji ambao ulikuwa chini ya mamlaka ya Waingereza, peke yake inabidi uchukuliwe kuwa kama ni kipimo cha kutokujua, kutokujitambua na kukosa fikra za kina za mpangilio wa kimkakati wa nadharia za Kiislamu za kisasa, kwa kudhani kuwa sulushisho la tatizo hilo ingepatikana tu kwa kutayarisha Kongamano jingine. Salahuddin Ayyubi lazima angeguswa na hisia kali kaburini mwake. Ilionekana kama vile dunia ya wasomi wa Kiislamu wamepoteza mwelekeo kuhusu uhusiano imara unaosisitizwa na kuwekewa misingi yake ndani ya Qur'an baina ya 'nguvu' 'uhuru' na 'imani.'

Mnamo Mwezi wa Nane, Mwaka 1929 palitokea machafuko baina ya Waislamu na Wayahudi yaliyohusu Ukuta wa Maombolezo / Kilio uliopo Jerusalem. Jumuiya ya Mataifa (Ligi ya Mataifa) ilituma Kamati ili kuchunguza chanzo cha machafuko hayo na miongoni mwa matokeo ya utafiti wake Kamati iliripoti kuwa Waislamu walikuwa na '*haki za kumiliki*' maeneo ya Ukuta huo lakini Wayahudi walikuwa na '*haki za ibada*' kwenye Ukuta huo. Ripoti hii haikuwafurahisha Waislamu na pia haikuwafurahisha Wayahudi na inawezekana kabisa kusema kuwa ilisababisha, kwa namna moja au nyingine, kuitishwa kwa Kongamano hilo la Jerusalem.

Mwanzoni mwa Mwaka 1931, wakati wa mazishi ya kiongozi wa Waislamu wa India, *Maulana* Muhammad Ali Jawhar[48], ndani ya mipaka ya *Haram al-Sharif*, Jerusalem, makubaliano yalifikiwa baina ya kaka yake *Maulana* Shaukat Ali, na *Hajj* Amin al Hussaini juu ya umuhimu wa kuandaa mkutano huo. Miezi michache baadaye, Mwezi wa Sita, Mwaka 1931, ripoti ya Kamati ya Ukuta wa Maombolezo / Kilio ilitangazwa rasmi, na Baraza Kuu la Waislamu wa Palestina ndipo lilipotangaza rasmi nia ya kuandaa mkutano.

Tangazo rasmi la makubaliano ya kufanya mkutano huo na uamuzi juu ya tarehe ya mkutano vilifanyika tarehe 4 Mwezi wa Tisa, Mwaka 1931, na *Maulana* Ali Shaukat ndiye aliyetoa tangazo hilo baada ya sala ya mchana katika msikiti wa Al-Aqsa, Jerusalem.

---

[48] Muhammad Ali Jauhar alikuwa amefariki akiwa London alikokuwa akishiriki kwenye Mkutano wa Majadiliano kuhusu India. Wapalestina walipendekeza azikwe ndani ya Haram al-Sharif kwa kutambua umaarufu na umuhimu wake na pia kwa kutaka kupata msukumo mkubwa Zaidi wa msaada kutoka India dhidi ya Wazayonisti na nguvu za 'Usimamizi' wa Waingereza.

Waislamu wa India, sasa wangeweza kuwa wamepata nafasi ya aina yake na iliyo muhimu sana ya uongozi katika dunia ya Kiislamu.

## *Tarehe na Jukwaa*

Kongamano la Kiislamu lilifanyika Jeruslem kuanzia tarehe 6 hadi 16 Mwezi wa Kumi na Mbili, Mwaka 1931. Hii ni sawa na Mwezi wa *Rajjab 27* hadi *Shaban 7* kwa Kalenda ya Kiislamu. Tunaweza kutaja katika kupitia kwetu na kumbukumbu kuwa tarehe iliyochaguliwa kuwa ni ya kuanza kwa Kongamano kwa kalenda ya Kiislamu, *27 Rajjab*, na chaguo la msikiti, *Al-Aqsa* navyo vina umuhimu wake wa pekee kidini.[49]

Tukiangalia kwa makini tutaona kuwa wakati Kongamano la *Khilafah* lililofanyika Egypt, ambayo kwa kwa jina ilikuwa nchi huru ambayo kiukweli ilikuwa eneo ambalo liko chini ya athari za Uingereza, na pia Kongamano la Kimataifa la Kiislamu, ambalo lilifanyika *Hejaz,* ambayo nayo ilikuwa pia eneo huru kwa jina tu, nalo lilikuwa chini ya athari za Uingereza, Kongamano la Aqsa la Kiislamu lilikuwa linafanyika kwenye eneo ambalo lilikuwa moja kwa moja chini ya utawala na mamlaka ya Uingereza. Jerusalem hata haikuweza kuwa na 'jani la figi' la kuiwezesha kujisitiri hali yake ya kuwa lilikuwa ni eneo 'lililonyakuliwa' kwa nguvu au kwa ila. Wako wale ambao wanapendekeza hoja kuwa eneo hilo lililonyakuliwa lingepaswa lipewe wadhifa wa *Dar al-Harb!*

Hilo lazima lilikuwa ni tamasha la ajabu na la aina yake kwa Dunia ya Kiislamu kukutana kwa ajili ya Kongamano Kuu la Kiislamu la Dunia kwenye eneo 'lililonyakuliwa' likiwa na lengo la kuirudisha hali iliyopotea na kuijenga upya misingi ya Itikadi ya Kijamii ya Kiislamu kwa mujibu wa *Shari'ah*. Kwa upande huu, Kongamano Kuu la Kiislamu la Jerusalem lilikuwa ni la kipekee na lisilowahi kutokea kabla yake katika historia nzima ya Uislamu.

---

[49] Pana kiungo muhimu sana baina ya tarehe 27 ya *Rajab*, *Masjid al-Aqsa* na Ukuta wa Kilio /Maombolezo, kiungo ambacho kinaleta hisia kali na msukumo mkubwa wa kiroho miongoni mwa Waislamu duniani. Maelezo yake ni kama ifuatavyo: Sura ya kumi na saba ya Qur'ani, inayoitwa *Surah al-Isra*, inaanza kwa aya ambayo inataja safari ya kiajabu ya usiku ya Mtume Muhammad kutoka *Masjid al-Haram* (msikiti mtukufu wa Makkah) hadi *Masjid al-Aqsa* (msikiti wa mabli, Jerusalem) ambapo mipaka yake, kwa mujibu wa aya, imebarikiwa na Allah, Aliyemchukua kwenye safari kwa lengo la kumuonyesha baadhi ya 'Alama' Zake. Maandishi ya *Hadith* yanaeleza kuwa alipowasili kwenye *Masjid al-Aqsa*, aliongoza sala ya jamaa ambamo Mitume wote walishiriki. Baadaye alisafirishwa hadi peponi na akatunukiwa fursa ya kuingia huko na kuwa kwenye "hali maalum ya kuwapo" pamoja na Allah. Ukuta wa Kilio / Maombolezo au Ukuta wa Magharibi unawakilisha sehemu ya *Haram al-Sharif* ambamo ndani yake upo *Masjid al-Aqsa* ikiwa ni pamoja na mahali ambapo safari ya Mtume kuelekea peponi ilianza. Inaaminika kuwa safari hiiilifanyika tarehe 27 *Rajab*. (Mishkat al-Masabih), Tafsiri ya Kiingereza ya James Robson, Lahore, Shaikh Muhammad Ashraf, 1975, Toleo 2, Sura 23, kurasa 1264 – 1270.

Ukweli ni kuwa hali hii ilidhihirisha hali mbaya na ya kusikitisha ambamo Uislamu ulikuwa umejikuta umo. Inawezekana kuwa, Serikali ya Uingereza ilishangazwa mno na tukio hili. Kwa mujibu wa mtazamo wa Serikali ya Kiingereza, Dunia ya Kiislamu ingekuwa yenyewe inajiweka wazi jukwaani na kuitangazia dunia nzima udhaifu wao. Kwa njonjo na furaha, Serikali ya Uingereza ilijihusisha kidogo sana kwa kumuonya *Hajj* Amin al-Hussaini, kupitia kwa Balozi wa Uingereza, kuwa Serikali yao haitoruhusu kuitishwa kwa Kongamano ambamo masuala fulani yatajadiliwa ambayo yanahusu sera za mambo ya ndani na ya nje ya dola zilizojishirikisha.[50]

Vyombo vya habari vya Wazayonisti, kwa upande wa pili, viliibuka kwa wasiwasi mkubwa baada ya taarifa za kuitishwa kwa Kongamano hilo, na kuishutumu Serikali ya Uingereza kuruhusu kufanyika kwa Kongamano hilo kwa kuwa “Uingereza ilitaka Kongamano hilo lifanyike, na pia ililichochea lifanyike ili kuwaridhisha Waislamu wa Palestina na India na kujaribu kuzihimili jitihada na harakati za Shirikisho la Wazayonisti.”[51]

Inabidi pia tugundue kuwa palikuwa na tetesi nyingi zilizoashiria kuwa Kongamano lingejaribu kumteua upya Abdul Majid kuwa kama *Khalifah* na kuweka Makao yake Makuu Jerusalem. Tendo hilo lingekuwa ni la kudhoofisha utawala wa Angora, (sasa Ankara) na kuwapo kwa *Khalifah* Jerusalem, iliyo chini ya mamlaka ya Uingereza, kingekuwa ni kitu ambacho Waingereza aghlabu wangekipendelea kwa ajili ya fursa ya kufunguka kwa uwezekano wa wao kuitumia nafasi hiyo kwa kujinufaisha kusiko kikomo.[52] Uingereza ingeweza kuwageuza Waislamu kuwa wenye haki ya kuchekwa kote duniani kwa kufanya kosa kubwa kama hilo la kumuweka *Khalifah* awe chini ya mamlka ya Mfalme wa Uingereza. [Takriban miaka 80 baadaye, Mchipuko mwingine wa Kiarabu unatishia kuurudisha utawala kama huo wa *Khilafah* wa bandia]

## *Wajumbe*

Kongamano lilifanyika katika hali na mazingira yaliyokuwa huru na yasiyokuwa na vikwazo

---

[50] Gibb, H.A.R., “Mkutano Mkuu wa Kiislamu wa Jerusalem Mwezi wa Kumi na Mbili, 1931”. Uchambuzi wa Masuala ya Kimataifa, London, Oxford University Press, 1935, ukurasa 103.

[51] Nielsen, A. “Mkutano Mkuu wa Kiislamu wa Jerusalem.” Dunia ya Kiislamu, Mwezi wa Kumi, 1932, Toleo 22, ukurasa 348.

[52] Mfalme Fuad wa Egypt, hususan, alisumbuliwa sana na tetesi kuwa suala la *Khilafah* litajadiliwa na *Khalifah* kuteuliwa kiasi kwamba Mufti Mkuu alilazimika kuenda Kairo yeye binafsi na kutoa tamko la kinywa na kimaandishi kumhakikishia kuwa suala hilo halitojadiliwa. Kwa *Maulana* Shaukat Ali, kwa upande wa pili, hapakuwa na tatizo kwani aliendelea kumtambua Abdul Majid kama Khalifah. (Arnold, T., Op. cit. kurasa 241 – 244).

wala masharti, na ukiachilia mbali kufukuzwa kwa Abd al-Rahman Azzam, raia wa Egypt, kutokana na matamshi yake makali ya kuzilaumu sera za Italia juu ya Libya, Mamlaka ya Kiingereza ya Palestina hayakuingilia kati kwa namna yoyote kwenye Kongamano na pia hawakuweka masharti yoyote kuhusu wajumbe wake.

Wajumbe kwenye Kongamano walikuja kutoka Persia (baadhi ya *Ulama* wa ki-Shia), India (miongoni mwa wajumbe alikuwamo msomi mkubwa na maarufu wa Kiislamu, Dr Muhammad Iqbal), Yugoslavia, Moroko, Algeria, Tunisia, Libya, Syria na Nigeria.

Ingawa Serikali ya Egypt hatimaye iliamua kutoleta ujumbe rasmi, palikuwa na wajumbe kutoka Egypt waliokuja kumuunga mkono Mfalme. Walikuwa wakipingwa na ujumbe uliokuwa ukiwakilisha chama cha *Wafd* cha Egypt. Mashirikisho kadhaa ya kiharakati ya Kiislamu kutoka Egypt pia yalihudhuria.

Serikali za Iraq na Transjordan pia zilituma wajumbe rasmi. Mfalme wa Saudia, Abdul Aziz Ibn Saud hakuwa na msimamo kamili kuhusu Kongamano na mwishowe, kwa ujanja alimtuma muwakilishi ambaye hakuweza kuwasili kwenye Kongamano katika muda uliopangwa kufanyika Kongamano, alichelewa. Uturuki na Afghanistani waliamua kutotuma ujumbe wowote kuja kwenye Kongamano. Ukilinganisha na Kongamano la Makkah la Mwezi wa Saba, mwaka 1926, palikuwa na idadi pungufu zaidi ya wajumbe rasmi waliokuja kuwakilisha Serikali zao kwenye Kongamano la Jerusalem.

## *Majukumu ya Kongamano*

Baada ya ufunguzi rasmi wa Kongamano kwenye Msikiti wa al-Aqsa baada ya sala ya Maghrib siku ya tarehe 6 Mwezi wa Kumi na Mbili (27 Rajjab)[53] kamati nane ziliundwa kuchunguza na kutayarisha ripoti kuhusu masuala yafuatayo:

- Kanuni za Kongamano;
- Propaganda za Kongamano na usambazaji kwenye vyombo vya habari;
- Fedha na mfumo wa utawala;
- Utamaduni wa Kiislamu na pendekezo la Chuo Kikuu cha al-Aqsa;
- Reli ya Hejaz;
- Maeneo Matakatifu na Ukuta wa Ibada / Kilio;

[53]Katika mfumo wa mpangilio wa muda, siku inaanza jua linapotua (linapokucha) na inaisha jua linapotua siku ifuatayo. Hivyo basi *Rajab 27* (au *Lailatul Mi'raj*) haikuanza hadi jua lilipokucha tarehe 6 mwezi wa kumi na mbili.

- Propaganda za Kiislamu na Miongozo;
- Mapendekezo yaliyoletwa mbele ya Kongamano

Kama vile Kongamano la Makkah la Mwaka 1926, Kongamano la Jerusalem lilipitisha Kanuni au Katiba. Katiba ya Makkah iliamua kufanyika kwa Kongamano kila mwaka Makkah. Katiba ya Kongamano la Jerusalem lilipitisha azimio la kufanyika kwa Kongamano mara mbili kila mwaka, mjini Jerusalem. Sekretariati ndogo pia ilianzishwa hapo hapo Jerusalem (kama ilivyofanywa Makkah). Sekretariati iliendelea kufanya kazi kwa miaka kadhaa lakini Kongamano halikuweza kufanyika tena.[54]

Kongamano liliamua kuwa Chuo Kikuu cha Kiislamu kijengwe Jerusalem. Uamuzi huo ulipitishwa dhidi ya hali ngumu ya wivu iliyoonyeshwa na Chuo Kikuu cha Al-Azhar ambacho hakikutaka nafasi yake pekee iliyokuwa nayo katika jumuiya ya Kiislamu ya kuwa chuo pekee cha Kiislamu duniani ivunjwe kwa kuanzishwa kwa chuo pinzani cha Kiislamu.[55]

Lakini jambo lililokuwa ni la muhimu kuliko mambo yote ambayo Kongamano iliyajadili lilikuwa, bila ya shaka yoyote, suala lililohusu tishio la Wazayonisti katika Palestina. Mtazamo mpana na mbinu zilizotumika kwenye Kongamano kulikabili tatizo hilo tete zilikuwa za busara na ustadi wa hali ya juu. Raisi wa Wakala wa Wayahudi, Bwana Sokolow, alikaribishwa kuhudhuria Kongamano kwa lengo la kumtaka atoe maelezo juu ya suala hilo akiwakilisha mtazamo wa Wazayonisti. Mwaliko, uliotolewa na Shaukat Ali, ulikataliwa. Na katika vyombo vya habari vya Wazayonisti, wanaharakati wa Kizayonisti walilifanyia Kongamano maskhara na kulikejeli.[56]

Palikuwa na kundi la pili la Wazayonisti, waliokuwa na msimamo wenye amani zaidi kuliko hilo kundi la kwanza, ambao walikuwa wameanzisha Chuo Kikuu cha Kihebrania. Wazayonisti hawa, walikuwa wakiliongelea Kongamano kwa heshima zaidi, japo nao pia, waliishutumu sana Uingereza, kwa nguvu zote kama vile lilivyofanya kundi la kwanza la Wazayonisti, kwa kuliruhusu Kongamano lifanyike na lizungumzie sera za Uingereza katika Palestina.[57]

---

[54]Gibb, H.A.R., Op. cit., ukurasa 105. Kongamano la Jerusalem lilifufuliwa tena Mwaka 1953 na mikutano mitatu ilifuatia baada ya hapo Mwaka 1953, 1956 na 1960. Mikutano hiyo haijafanyika tena tangu Mwaka 1960. Mojawapo ya sababu ya hilo ni kuwa Raisi wa Kongamano la Jerusalem, *Hajj* Amin al-Husseini, alichaguliwa pia kuwa Raisi wa Kongamano lililofufuliwa la Dunia la Kiislamu. Alipendelea kujihusisha zaidi na kufanya kazi na hilo la pili kwa kuwa lilikuwa likipata kuungwa mkono na Serikali ya Pakistani na pia kupata msaada wa kipesa kutoka kwenye serikali ya Saudi Arabia.

[55]Gibb, Op. cit., ukurasa 102.

[56]Nielsen, Op cit. ukurasa 353.

[57]Ibid.

Lakini Wayahudi waliokuwa na msimamo asili (orthodox) wa Jerusalem, ambao waliishi na kufanya kazi zao tofauti na mbali na Wazayonisti, walilitumia salamu njema Kongamano lilipoanza na kulitakia mafanikio mema. Walieleza kuwa Wayahudi hawayataki maeneo matakatifu na wala hawana haki juu yake, isipokuwa waliliomba Kongamano lisiwazuie desturi yao ya tangu zamani ya Kiyahudi ya kusali kwenye Ukuta wa Maombi / Kilio.[58]

Na Kongamano lilifanya hivyo hivyo kama lilivyoombwa! Kongamano liliikataa ripoti ya Kamati ya Ligi ya Mataifa ya Ukuta wa Maombi / Kilio iliyothibitisha kuwa Waislamu wana haki miliki ya Ukuta huo na kusisitiza haki ya Wayahudi kusali kwenye Ukuta huo.[59] Kwa kufanya hivyo, Kongamano lilisababisha kutengwa kwa Wayahudi hao waliokuwa na msimamo wa asili (orthodox) na kudhoofisha jitihada zao katika harakati za kupingana na Wazayonisti.[60]

Kongamano liliwasilisha malalamiko yake rasmi kwa Ligi ya Mataifa kwa kuingiliwa kati kwa haki za Waarabu na ililikumbusha Ligi la Mataifa msaada uliotolewa na Waarabu kwa Mataifa Yaliyojishirikisha kwenye Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia. Hakuna mtu miongoni wa washiriki, aliyegundua kuwa msaada kama huo uliotolewa na Waislamu kwa Uingereza, Ufaransa na Washirika wao kwenye Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia ulikuwa unavunja amri ya Allah iliyo kwenye Qur'ani.

Kongamano lilionya kuwa 'mamlaka' juu ya eneo haikuwa ikimaanisha kuwa mtawala ana haki ya kuwanyanyasa Waarabu na kuwanyang'anya haki zao. Kongamano halikupinga misingi ya Uhamiaji wa Wayahudi kuja Palestina na kununua ardhi na majengo. Kwa maneno mengine, ilionyesha hapo kuwa, Kongamano lilizitambua haki za Wayahudi kuingia na kuishi Palestina na kumiliki ardhi na majengo. Kuhusu mpango wa kuanzisha Makazi ya Kitaifa ya Wayahudi ndani ya Palestina, Kongamano lilipendekeza kuanzishwa kwa Benki ya Kilimo ambayo ingewapa misaada wakulima wadogo wadogo, mmoja mmoja na waliojijumuisha ili kuwapa nguvu na uwezo wa kudhibiti jitihada za Wazayonisti kununua ardhi zao.

Majibu ya Kongamano kuhusiana na tishio la Wazayonisti yanaweza kuchukuliwa kuwa yalikuwa ni majibu yenye uzito wa wastani. Huu ulikuwa msimamo uliokuwa ni

---

[58]Nielsen, Op cit. ukurasa 353.

[59] Nakala kamili ya ripoti imeambatanishwa kwenye Amri kwa Palestina (ya Ukuta wa Maombi / Kilio au Ukuta wa Magharibi) ya Mwaka 1931 ikiwa kama Ratiba 1 na 2. Angalia Kanuni na Amri za Kisheria za Mwaka 1931. H M Stationery Office, London 1932 kurasa 462-466.

[60]Mtazamo huu ulithibitishwa zaidi baadaye kwa kutamkwa rasmi baina ya Miaka 1948-1967 wakati Jerusalem ya Mashariki ilipowekwa chini ya Mamlaka ya Jordan.

kinyume na msimamo uliochukuliwa na wanaharakati wa kizalendo wa Kiarabu. Ukweli ni kuwa Kongamano halikuruhusu shinikizo na jitihada zilizofanywa na wanaharakati wa

kizalendo wa Kiarabu kuazimia msimamo mkali zaidi. Wanaharakati hao wa kizalendo wa Kiarabu walifanya mikutano yao mbali na Kongamano na waliunda 'Agano la Waarabu' kitu ambacho kilikuwa cha kutegemewa kutokea kutokana na misimamo ya wanaharakati wa kizalendo wa Kiyahudi.[61] Kila mmoja baina yao, alikuwa anapingana na mwenziwe.[62]

Kongamano lilishindwa kugundua, hata hivyo, kuwa majibu ya kidini ya Kiislamu yalipaswa yalenge katika kujenga harakati za pamoja, na yajumuishe mkakati hai uliojumuisha kwenye jitihada zake, juhudi za wale Wayahudi wenye msimamo wa asili, ambao pia walikuwa wakipingana na Wazayonisti na ambao walikuwa na msimamo wa kirafiki na Waislamu.[63] Ingawa Qur'ani ilikataza kujenga urafiki na Wayahudi na Wakristo ambao tayari wamo kwenye ushirika kwa kuwa itawaweka Waislamu kwenye hali tegemezi na iliyo dhalili, haikukataza kuundwa kwa jitihada za pamoja na kuwa na uhusiano wa aina hiyo na Wayahudi (na wengine wasiokuwa Waislamu) kufungamana au kuwa na harakati za pamoja zisizokuwa na hali tegemezi ndani yake.[64]

---

[61] "Ardhi za Waarabu ni kamili na hazigawanyiki, na mgawanyo wowote uliofanywa kwa kulazimishwa haukubaliki na wala hautabuliwi na taifa la Kiarabu..." Gibb, Op. cit., ukurasa 107 fn.

[62] Cf Marmostein, Emile: "Upinzani wa Kidini dhidi ya Uzalendo katika Mashariki ya Kati." Masuala ya Kimataifa, mwezi wa Saba 1952, kurasa 344-357.

[63] Miongoni mwa Wayahudi wenye msimamo wa Asilia alikuwamo msomi, Profesa Jacon de Haan. Aliuawa na Wazayonisti kwa kuwa alikuwa akiupinga kwa nguvu zote Uzayonisti. Katika mahojiano muhimu aliyoyafanya mwanzoni mwa miaka ya ishirini alifafanua mtazamo wake:

> "Je, unadhani kuwa historia si kitu chochote zaidi ya mlolongo wa matokeo ya bahati mbaya mithili ya ajali? Sidhani... Wazayonisti wanakumbwa na tatizo lile lile la upofu wa kiroho ambao ndiyo uliyotuletea maafa na kuanguka kwetu kama Taifa. Miaka elfu mbili ya maisha ya dhiki na kukosa furaha ya uhamishoni ya Wayahudi hayawatufundisha lolote. Badala ya kufanya jitihada za kutafuta chanzo cha ndani cha dhiki zetu na kukosa furaha kwetu, wanajaribu kulizunguka tatizo hilo, na kama ilivyo, wanajaribu kujenga 'Makazi ya Taifa' kwa misingi iliyowekwa na dola na siasa za Kimagharibi. Na katika mchakato wa kujenga 'Makazi ya Taifa' wanatenda uovu wa kuwanyang'anya watu wengine ardhi na makazi yao." Assad, Muhammad, Njia ya Makkah, kurasa 98-99

۞ يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ لَا تَتَّخِذُوا۟ ٱلْيَهُودَ وَٱلنَّصَٰرَىٰٓ أَوْلِيَآءَ ۘ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَآءُ
بَعْضٍ ۚ وَمَن يَتَوَلَّهُم مِّنكُمْ فَإِنَّهُۥ مِنْهُمْ ۗ إِنَّ ٱللَّهَ لَا يَهْدِى ٱلْقَوْمَ ٱلظَّٰلِمِينَ ﴿٥١﴾

Kitu pekee kilichosikitisha hapo ni Kongamano kushindwa, likiwa limekutana hapo hapo kwenye Mji Mtakatifu wa Jerusalem, kufikia na kuweka tathmini halisi ya hali mbaya iliyokuwa imewakumba Waislamu, na hivyo basi kuweza kuweka kwa ushupavu na ubunifu, mikakati madhubuti na ya busara yenye mitazamo ya madira marefu kwa lengo la kuzifufua nguvu za *Ummah*.

Katikati ya mijadala mikali ya kisiasa na yenye kusisimua ya Kongamano, sauti moja ilijitokeza na kujitofautisha kama sauti ya mwanasiasa mweledi, mwingi wa hekima na busara. Dr. Muhammad Iqbal alikuwa na mtazamo na maono ya mbali na kina yaliyomuwezesha kuonya kuwa hatari kubwa zinazoukabili Uislamu siyo mipango miovu ya Wazayonisti, ulafi wa dola za Kifalme na kadhalika, bali ni sera na itikadi za kupinga kuwapo kwa Mwenyezi Mungu na uzalendo wa kitaifa. Ikiwa haya hayatofanyiwa kinga yasienee kwenye jumuiya za Kiislamu, basi Uislamu utaingiliwa na sumu na utapotea.**[65]**

Lakini wakati ilikuwa ni kweli kuwa Iqbal alikuwa na mtazamo na maono ya hatari kubwa za kifalsafa zilizoukabili Uislamu, ikiwemo materializmu, vikijisambaza kwenye utamaduni wa Kiislamu, inaonyesha pia kuwa hakuweza kufikia kuunda upya nadharia ya Mfumo wa Maadili ya Jumuiya wa Kiislamu (wa *Dar al-Islam*) na Mtazamo wa Kiislamu wa Mpangilio na Uhusiano wa Kimataifa na baadaye kuuelezea na kuufafanua kwa ufanisi wa kutosha kiasi kwamba iweze kuwashawishi wasikilizaji na kuona ubora wake ukilinganishwa na mfumo pinzani wa kidunia ambao sasa ulikuwa ukitoa changamoto zake kwa *Dar al-Islam*. Ukweli ni kuwa Iqbal hakujua ni hatua gani inabidi zichukuliwe mwaka 1931 kuhakikisha kuwa nguvu za dola zinarudishwa kwa *Ummah!* Alikosa kabisa mwelekeo kwenye uelewa wake wa eskatolojia ya Kiislamu, na matokeo yake, hakuweza kupenya gamba la nje na kuona ndani kwenye hali halisi iliyokuwa ikiukabili *Ummah* baada ya kuvunjwa kwa *Khilafah*. [Tazama utunzi wangu wenye kichwa cha habari: 'Iqbal na Kipindi cha Ukweli kwa Pakistani'.]

---

"Enyi mlio amini (hii Qur'ani)! Msiwafanye (wale) Mayahudi na (wale) Wakristo kuwa ni marafiki zenu na washirika wenu (wale) ambao ni marafiki na washirika wao kwa wao (baina yao – msiingie kwenye urafiki na ushirika wa Wazayonisti wa Kiyahudi-Kikristo). Na miongoni mwenu mwenye kufanya urafiki nao, basi huyo ni katika wao (umeupoteza Uislamu wako). Hakika Mwenyezi Mungu hawaongoi watu wenye kudhulumu." (Qur'ani, al-Maidah, 5:51)

**[65]**Mashariki ya Karibu na India. Tarehe 24, Mwezi wa Kumi na Mbili, Mwaka 1931. Ukurasa 687.

# Sura ya Tano

## *Yaliyojizi baada ya Kongamano*

Kongamano lilichagua Kamati ya Utendaji[66] ambayo ilifanya kazi kwa bidii na juhudi kubwa kwa muda wa mwaka mmoja. Matawi ya Shrikisho yalianzishwa kwenye nchi tofauti duniani na wawakilishi wa matawi hayo walikutana Jerusalem Mwezi wa Nane, Mwaka 1932 kujadili njia na namna za kukusanya michango ya kifedha. Mwaka 1933 Amin al Hussaini na Altabah Pasha walifanya ziara ya Iraq na India kwa lengo la kukusanya michango. Hawakufanikiwa, hivyo Chuo Kikuu kilichokusudiwa kujengwa Jerusalem, na pia Benki ya Kilimo (kuwasaidia wakulima) havikuweza kuanzishwa.

Mkutano wa pili wa Kongamano, ambao kwa mujibu wa Katiba, ulipaswa kufanyika Mwezi wa Kumi na Moja, Mwaka 1933, haukufanyika. Ukiachilia mbali kuibuka kwa ghafla kwa shughuli za Kamati ya Utendaji kuhusiana na 'usuluhishaji wa mgogoro' mnamo mwaka 1934[67] na kufufuliwa kwa shughuli hizo kwenye miaka ya hamsini, Kongamano la Kiislamu la Jerusalem pia lilikufa kifo cha kawaida.

Sekretariati iliyochaguliwa na Kongamano Mwaka 1931 iliendelea kufanya kazi Jerusalem hadi wakati wa Vita Kuu ya Pili ya Dunia. Haikuweza, hata hivyo, kusalimika kutokana na mazingira magumu yaliyosababishwa na vita hiyo na mgongano wa moja kwa moja baina ya *Hajj* Amin na Waingereza. *Hajj* Amin alikimbilia Egypt mwanzoni mwa vita hiyo.

Kongamano Kuu la Kiislamu la Jerusalem la mwaka 1931 lilishindwa kutimiza malengo yake na kupata suluhu ya matatizo ya *Ummah* kwa sababu zile zile ambazo Makongamano ya Kairo na Makkah ya Mwaka 1926 yalishindwa. Yalikuwa hayakuweza kutoa maelezo na kufafanua kwa ufanisi wa kutosha njia zipi zifuatwe ili Uislamu na Waislamu waweze kujikwamua kutoka kwenye fujo na machafuko ya kiitikadi ambayo dunia

---

[66]Shaukat Ali hakufurahishwa na muundo wa Kamati na alikataa kujishirikisha kwenye kufanya kazi nayo. Hajj Amin alitumia wingi wake kuwaondoa wapinzani ambao miongoni mwao walikuwa watu wenye uwezo mkubwa.

[67]Kamati ya Utendaji ilifanikiwa kusuluhisha vita ya wiki saba baina ya Saudi Arabia na Yemen. Makubaliano hatimaye yalitiwa saini kuvimaliza vita hivyo.

ya Kiislamu ilijikuta imesimikwa. Hayakuweza kuja na pendekezo la kifikra lililoweza kupambana na mfumo wa kisiasa wa kidunia uliokuwa ukipendekezwa na jamii iliyokuwa ikijiamini na yenye kiburi ya utamaduni wa kimagharibi ambayo ilikuwa ikilazimisha juu ya jamii iliyodumaa kifikra ya Kiislamu mfumo wa Serikali za kimataifa wa kidunia kuchukua nafasi ya *Dar al-Islam*.

Kutokomea kwa *Khilafah* kulishuhudia kuondolewa na kusambaratika kwa mfumo na muundo wa kisiasa ambao *Ummah* ulikuwa umezaliwa nao, mfumo ambao ulikuwa ukitambua kufuata muongozo wa itikadi, miongozo na kanuni za Uislamu katika maisha ya jumuiya, ambayo ilipewa kipaumbele. Kuzaliwa kwa Serikali ya Kitaifa ya kidunia ya *Wahhabi wa Saudia* ndani ya maeneo ambayo ni chimbuko la Uislamu kulimaanisha kuwa Uislamu sasa ulikuwa unaelekea kwenye uchochoro wa kugeuzwa na kufuata misingi ya mfumo wa kidunia usiomtambua mwenyezi Mungu kama *al-Malik*, *al-Akbar* na *al-Hakam.* Nyanja zote ambazo itikadi, miongozo na kanuni za Kiislamu zilikuwa zikitumika kwenye maisha ya siku hadi siku ya Waumini, sasa zinaondolewa jukumu hilo, zinashushwa daraja na kufanywa kuwa ni eneo la uamuzi binafsi na matumizi ya Shariah yatafanyika pale tu ambapo yatakuwa na thamani ya kipodozi. Wafuasi wa *Tabligh Jamaat*, ambao hawajihusishi na siasa na *Salafis* ambao wanaunga mkono utawala wa *Wahhabi* hivi sasa wataanza kuziba pengo lililojitokeza. Na tafsiri ya Qur'ani ya Abdullah Yusuf Ali iliyotafsiriwa kuepuka kupingana na mwenendo wao, sasa itaanza kusambazwa na kukuzwa miongoni mwa vizazi visivyojitambua vya Waislamu ambavyo vilikuwa vimeduamaa kisiasa kwa kutokujua msimamo wa kiislamu wa mfumo na uhusiano wa Taifa na ki-Mataifa.**[68]**

۞۞۞

[68]Abdullah Yusuf Ali alikuwa ni bingwa wa fasihi. Tafsiri yake ya Qur'ani ilikuwa ni kazi kamili, nzuri yenye ustadi na umahiri mkubwa ambayo iliegemea kutafsiri kuwa Kiingereza kazi kubwa na nzuri ya *Tafsir* ya wanazuoni wa lugha ya ki-Urdu. Lakini, alikuwa na uzoefu mdogo katika uelewa wake wa mafunzo na miongozo ya kisiasa na kiuchumi iliyomo kwenye Qur'ani. Utiifu na uaminifu wake wa hali ya juu usiotetereka kwa Serikali ya Uingereza kulimpelekea kuwa na mtazamo wa kifikra uliomfanya asiweze kugundua na kuuelewa ukweli wa kimsingi wa kuwa Allah aliishusha dini iliyo bora kabisa ya Kiislamu ili ichukuwe nafasi ya juu kabisa katika kusimamia mambo yote ya kimaisha ya binafsi ya na jumuiya. Pia alishindwa kugundua kuwa nyongeza ya faida ya mabenki ni Riba. Tazama kitabu mahiri kinachomzungumzia Abdullah Yusuf Ali 'biography' kilichoandikwa na M.A. Sharif chenye kichwa: '*Searching for Solace'*, Islamic Book Trust. Kuala Lumpur, 1994.

# Hitimisho

> "Kuvunjwa kwa mfumo wa umoja wa Uislamu wa Taifa la *Khilafah* na kuwekwa kwa mfumo mbadala wa ma-Taifa ya kidunia yasiyomtambua Mungu ambayo yako chini ya Umoja wa Mataifa ulio mikononi mwa Wazayonisti ni matokeo ya njama za siri na kishetani za *Dajjal* zilizotungwa na Waingereza na Wazayonisti wa Kiyahudi. *Wahhabi wa Saudia* wamekuwa washirika wa hiari na kujitolea kwenye tendo hilo la jinai dhidi ya *Ummah*."

*Khilafah* ilikuwa kama ni alama ya mfumo wa muundo wa kisiasa (ikimaanisha *Dar al-Islam*) wa Jumuiya ya Kiislamu ambayo ilikuwa ikizitambua kanuni, itikadi na miongozo ya Uislamu kuwa ni amri kuu zenye wajibu wa kufuatwa misingi na maamrisho yake katika maisha ya siku hadi siku ya jamii na pia katika kujenga uhusiano wa kimataifa miongoni mwa dunia ya Kiislamu.

Kuibuka kwa mataifa yenye Serikali za Kitaifa za Uturuki na Saudia kwenye makao makuu ya *Khilafah* na kwenye maeneo ambayo ni chimbuko la Uislamu, kulipekekea kuchongwa barabara iliyoelekea kwenye kuingizwa kwa muundo wa mfumo wa kidunia wa kisiasa usiomtambua Mwenyezi Mungu kwenye ardhi za Waislamu. Na kwa kuwa sasa ni serikali za nchi zilizo na msimamo wa kidunia za nchi za Kitaifa ndani ya dunia ya Kiislamu ndizo ambazo zingekuwa zikiuwakilisha Uislamu, hali hiyo ilipelekea kuwa Uislamu haukuwa tena na kiupaumbele na uliondolewa hali yake ya juu kabisa ya uwakilishi wa kanuni na maadili yake kwa jamii, na kwenye uhusiano wa kimataifa baina ya nchi au jumuiya za Kiislamu duniani na badala yake, itikadi na kanuni za Uislamu zinashushwa daraja na kufanywa kuwa ni maeneo ya uamuzi binafsi. Hivyo basi, kwenye uhusiano wa kijamii ndani ya dunia ya Kiislamu, Allah siyo tena *Akbar!*

Hadi Taifa la Pakistani lilipoanzishwa mnamo mwaka 1947, muhuri wa Taifa la Saudia ulikwishachapishwa na Taifa la Kiislamu la *Khilafah* likawa limekwishapelekwa kwenye kumbukumbu za kihistoria. Hakuna mwanasiasa, au chama cha siasa au mwanazuoni yeyote wa Pakistani ambaye leo hii angetarajia kuendelea 'kuwapo kisiasa' ikiwa atadiriki "kipumbavu" kutamka kuwa anaanzisha harakati za kulirudisha Taifa la *Khilafah*.

Hakuna Muislamu ambaye atasoma maelezo haya na kisha asijisikie kushikwa na hasira kubwa dhidi ya wale ambao wamemsaliti Mwenyezi Mungu Mtukufu na Mtume Wake (rehma na amani juu yake)! Kiwango cha *Iman* ya Muislamu kinaweza kupimwa kwa kuangalia jinsi ambavyo atakabiliana na hali hii mbaya na ya kusikitisha iliyopo. Kuvunjwa kwa mfumo wa umoja wa Uislamu wa Taifa la *Khilafah* na kuwekwa kwa mfumo mbadala wa ma-Taifa ya kidunia yasiyomtambua Mungu ambayo yako chini ya Umoja wa Mataifa ulio mikononi mwa Wazayonisti ni matokeo ya njama za siri na kishetani za *Dajjal* zilizotungwa na Waingereza na Wazayonisti wa Kiyahudi. *Wahhabi wa Saudia* wamekuwa washirika wa hiari na kujitolea kwenye tendo hilo la jinai dhidi ya *Ummah.*

Dunia ya Kiislamu leo hii haina nguvu zozote. Hitimisho letu ni kuwa chombo cha *Khilafah*, ambacho kinaunda sehemu ya *Dar al-Islam* ni muhimu sana na hakiwezi kukosekana ikiwa pana lengo la kuifufua na kuipata upya nguvu inayokosekana. Bila ya nguvu hizo, pataongezeka kuwepo kwa Bosnia, Kashmiri, Algeria, Chechnya, Palestina n.k. Njia pekee ambayo itahakikisha kuwa hali hii ya kusikitisha inabadilika na kurudisha hali ya kupewa umuhimu wa awali kwa Uislamu ndani ya Jumuiya za Kiislamu na kwenye uhusiano baina ya nchi na mataifa mbalimbali ya Kiislamu, ni kuurudishia umuhimu huo wa awali wa Uislamu. Hiyo inahitaji kufufuliwa kwa *Dar al-Islam* na Khilafah. Hivyo basi, tunahitaji kuvitamka upya na kuvifafanua vifungu vinavyojenga Mfumo wa Maadili ya Jumuiya wa Kiislamu (*Dar al-Islam*) na Mtazamo wa Kiislamu wa Mfumo wa Kimataifa, na kuonyesha wazi ubora wake ukilinganishwa na mfumo wa kidunia ambao umeibuka kwenye utamaduni wa nchi za kimagharibi.

Pia inatubidi tutambue, kama vile ambavyo kijitabu hiki kimeweka wazi, kuwa haiwezekani, na itabaki kuwa haiwezekani, kuufufua *Khilafah* ilhali *Hejaz* itaendelea kuwa chini ya himaya ya *Wahhabi wa Saudia* na washirika wao. Nguvu za dola za Uislamu haziwezi kufufuliwa bila ya ukombozi wa *Haramain* na *Hejaz* kutoka kwenye himaya ya wale ambao wameshiriki kwenye kuivunja *Khilafah*.

Ukombozi wa *Haramain* na *Hejaz* utawezekana pale ambapo ushirika wa *Wahhabi wa Saudia* utakapokuwa umevunjika. Kuna dalili kuwa ushirika huo uko kwenye hali ngumu na yenye shinikizo na inawezekana ukaanguka. Wanapatikana *Ulama* wengi hivi sasa wa Ki-Saudia ambao wametiwa jela au wamefungwa kifungo cha majumbani mwao. Jambo ambalo huenda likaongeza shinikizo la kuvunjika kwa shirikisho hilo ni 'kulitambua' Taifa la Israeli – na hivyo basi umuhimu wa kazi yetu ya hivi karibuni yenye kichwa cha habari: '*Dini ya Abraham na Taifa la Israeli*,' ambamo tunachambua, kutokana na mtazamo wa dini ya Kiislamu, athari kwa Waislamu katika 'kulitambua' Taifa la Kiyahudi la Israeli.

Wale ambao wameelekeza nguvu na maisha yao kwenye mapambano ya kulirudisha Taifa la Khilafah la Kiislamu wanaonekana mara moja kwenye mwenendo wao wa kisiasa. Hawazitambui, wala kuonyesha dalili za kuyatambua mataifa ya kisasa ya Umoja wa Mataifa ambayo yamechukua nafasi ya Khilafah, aidha kwa kushiriki kwenye chaguzi au kupigania nafasi za uongozi kwenye nchi hizo.

Kupiga kura kwenye uchaguzi ndani ya taifa la kisasa ambalo ni Kiislamu na mwanachama wa Umoja wa Mataifa ni kitendo kinachouhalalisha mfumo wa Dajjal wa Taifa na inaashiria kuliacha na kulisaliti Taifa la Khilafah. Hivyo basi, vile vinavyoitwa vyama vya kisiasa, kama vile Ikhwan al-Muslimun cha Egypt, kinachopigania kura kwenye uchaguzi, na wanazuoni wa Kiislamu wanaoviongoza vyama hivyo vinavyojiita vya Kiislamu, lazima watambuliwe kuwa ni wapotovu kwa kiasi kikubwa.

# *Kiambatanisho na.1*

## *Kumbukumbu za Talaat Pasha (1874 -1921) - zimechapishwa baada ya kifo chake 1921*

Baada ya maafa yaliyoikumba Uturuki mwaka 1913, nchi hiyo ilibaki bila ya kuwa na Rafiki miongoni mwa mataifa ya bara la Ulaya.

Urusi iliibuka na madai kadhaa, na Uingereza ilitutupilia kwa Urusi. Katika hali hiyo ngumu, ni Ujerumani pekee ndiyo iliyotupa msaada, na ni kwa nguvu za kinga yao pekee ndiko kulikotusaidia japo kuyaahirisha madai ya Urusi.

Hali hii ya kirafiki kwa upande wa Ujerumani ndiyo iliyotupa msukumo wa kupendekeza kwa Balozi wa Ujerumani aliye Porte (ikim., Konstantinopol) kuwa huenda tukaingia mkataba wa ushirika wa kudumu na Wajerumani. Lakini, wakati Balozi alionekana kupendelea sana jambo hilo lifanyike, serikali ya Berlin haikutaka. Ilijibu kuwa Uturuki imekuwa dhaifu mno, na ushirika huo kwa sasa utakuwa hauna tija kwa serikali zote mbili.

Hii, kwa kweli, ndiyo sababu inayoelezea kushindwa kwetu kupata Rafiki kote tulikotafuta. Mataifa ya Ulaya yalihitaji washirika wenye nguvu tu, ambao wangeisaidia badala ya kuwa mzigo.

Mwezi wa Sita, 1914, hata hivyo, tulishangazwa na mabadiliko ya msimamo wa serikali ya Ujerumani, pale ilipotutaka tutafakari upya ule mpango wa uwezekano wa kushirikiana. Kwa kuwa bado tulikuwa kwenye hali ile ile mbaya na isiyofurahisha ya kutengwa kama ilivyokuwa kabla ya hapo, hapakuwa na sababu ya kukataa pendekezo hilo.

Ushirika ulijadiliwa katika mikutano kadhaa na Balozi wa Ujerumani, na makubaliano yalipatikana haraka na kwa wepesi. Makubaliano ya awali yalitayarishwa na kutiwa saini, yakiorodhesha masuala makuu yaliyojadiliwa na kukubaliwa ya ushirika huo, ambao ulikuwa ni katika fani za kijeshi na kisiasa.

Muda mfupi baadaye yalifuata matukio kadhaa ambayo yaliishia kuripuka kwa Vita Kuu ya Dunia. Tukagundua kuwa mabadiliko ya msimamo wa Ujerumani kwetu yalilazimishwa na wao kugundua kuwapo kwa uwezekano wa kutokea kwa aina Fulani ya vita, lakini tuliendelea kufikiri kuwa ushirikiano huu utakuwa wenye manufaa kwetu. Hakuna taifa lenye nguvu la Ulaya ambalo lingetukaribisha sisi bila ya kutarajia kupata faida ya aina fulani kutoka kwetu.

Katika miezi kadhaa ya mwanzo wa Vita hiyo hali yetu ilikuwa ngumu sana. Kimkataba tulikuwa tayari tumeshajumuika na Ujerumani, na kila siku Mabalozi wa Ujerumani na Austria walikuwa wakija kwangu na kunishinikiza tuingie mara moja kwenye Vita. Ingekuwa rahisi kuwaeleza kuwa Italia, japo imo kwenye ushirika, lakini haijajiingiza kwenye Vita, au kwa kuwaonyesha kuwa kwa kuivamia Ubelgiji, Ujerumani ilikuwa imepuuza na kuvunja moja ya vipengele vya ushirika huo.

Lakini hatukutaka kuvunja ushirika na kujitoa kabisa kwa kuwa tulikuwa wenyewe tumeutafuta kwa shauku kubwa na tuliupa thamani kubwa. Hivyo basi tukawaambia Watutoni kuwa tutajiunga nao kwenye Vita haraka iwezekanavyo, lakini kufanya hivyo wakati Bulgaria ikiwa bado ikitafakari na bado haijatoa uamuzi kutakuwa na hatari kubwa kwetu na kwao pia.

Konstantinopol yote ilikuwa haina kinga kabisa dhidi ya jeshi la Bulgaria. Na kwa kuwa watu wa Bulgaria hawawapendi watu wa Serbia, itawawia rahisi Wajerumani kuishawishi Bulgaria kujiunga na ushirika. Hapo ndipo, na si kabla yah apo, Uturuki ingeweza kutekeleza makubaliano yake ya kupigana kuisaidia Ujerumani.

Jibu hili linalokubalika kimantiki lilituwezesha kuchelewesha kuingia kwenye Vita. Hivyo basi tukasubiri huku tukiangalia mtiririko wa matukio. Baadaye Ujerumani ilitutaka nasi pia tufanye majadiliano na Bulgaria, na kwa kuwa hatukuweza kukataa moja kwa moja, Halil Bey na mimi binafsi tulienda Sofia kwa mazungumzo.

Huko, baada ya mikutano mingi na viongozi wa Bulgaria, tuligundua kuwa waliogopa kufanya lolote kwa kuhofia Rumania. Ikiwa Rumania itajiunga na Urusi, majeshi hayo kwa pamoja yangeweza mara moja kuyashinda majeshi ya Bulgaria, hivyo nao hawakuweza kutuahidi chochote isipokuwa pale ambapo tungewahakikishia usalama na msaada dhidi ya mashambulizi ya Rumania. Kwa sababu hiyo, tuliondoka Sofia na kuelekea Bukaresti.

Baada ya mikutano na majadiliano ya kutosha tuliamini kuwa Rumania walitaka kuhakikisha kuwa hawajihusishi na upande wowote. Radoslavoff,

Waziri Mkuu wa Bulgaria, alitusihi tupate ahadi hiyo ya kutofungamana kwa maandishi, lakini Bratianu, Waziri Mkuu wa Rumania, alikataa kutoa. Alisema kuwa hati hiyo ya kutofungamana itakuwa haijafungamana ikitolewa kwa maandishi, lakini ananihakikishia kwa kutamka, kuwa hata ikiwa itatokea Bulgaria kuishambulia Serbia, Rumania itaendelea kubaki nje ya kujihusisha na Vita hiyo (ikim., haitoingia vitani kuisaidia Serbia.)

Radoslavoff aliona ahadi hii kuwa na thamani kubwa japokuwa pia aliiona kuwa haitoshelezi. Hivyo tulirudi Konstantinopol tukiwa tumeshindwa kutimiza lengo lililotupeleka safarini kulitafuta.

Sina hakika ni kiasi gani wanasiasa wa ushirika walifahamu kuhusu jitihada zetu tulizozifanya Sofia na Bukaresti, lakini baada ya hapo hapakuwa na matukio yoyote muhimu yaliyotuhusisha tukiwa Konstantinopol. Wajerumani na Waaustria waliendelea kujaribu kuturubuni kwa hila ili tuingie kwenye vita, na ushirika ulijaribu kwa kila hali kukwepa ugomvi na mabishano baina yao.

Tulijikita kwenye mbinu za kujichelewesha kuingia kwenye Vita, lakini kadiri muda ulivyokuwa ukipita ilikuwa inatuwia vigumu Zaidi. Mabaharia wa kijerumani waliokuwa mjini ilituwia vigumu sana kuwadhibiti kitabia, na namba ya maofisa wa Kijerumani iliongezeka siku hadi siku. Athari za Ujerumani daima ziliongezeka na kupata nguvu Zaidi.

Ndipo likajitokeza sakata la Bahari Nyeusi. Admirali wetu wa kijerumani, Souchon, kwa makusudi kabisa alizichukua meli zetu bora kuliko zote [Goeben na nyingine] na kuzitumia kuzipiga mabomu meli za Kirusi na miji kadhaa ya Warusi. Kawaida tulipaswa kuwa tumeidhinisha haya yote yatokee, na wakati wa Vita, niliacha pajengwe imani kuwa hali ilikuwa ndivyo hivyo, kuliko kuhatarisha kugombana na Wajerumani.

Sasa kwa kuwa siko tena kwenye uongozi wa masuala yote hayo, ningependa kuweka ukweli na hali halisi wazi kuwa Wizara yetu haikujua chochote kuhusiana na shambulizi hilo wala mpango wake kabla. Siyo mimi binafsi, na wala si afisa mwingine yeyote yule, hakuna kati yetu aliyetoa na kuidhinisha amri hiyo. Kinyume chake, wote tulisikitishwa na kukasirishwa sana na kitendo hicho. Mawaziri wote walichukizwa sana na tuliitisha kikao cha dharura na baadhi yao walijiuzulu kwa kupinga tukio hilo. Tuliobaki tulikubaliana kuendelea kujaribu kusawazisha suala hilo.

Balozi wa Urusi, kwa haraka sana, alitutumia waraka wa kupinga na kulilalamikia tukio hilo. Wafaransa na Waingereza pia walifanya hivyo hivyo. Hao wawili wa mwisho, hata hivyo, waliendelea kuwa na imani ya kuwapo kwa amani, na walipendekeza kuwa tuweke wazi kutohusika kwetu kwa

kuwaondoa admiral wa Kijerumani na askari wake, na kuendelea kubaki na msimamo wa kutofungamana na upande wowote.

Hatukuweza tena kuendelea kushikilia msimamo na hali hiyo isiyokuwa yenye weledi. Kutimiza matakwa yao kwa kumuadhibu admiral Souchon mbele ya halaiki kungemaanisha kupoteza ushirika wetu na Wajerumani milele. Tuliitisha kikao kingine cha Baraza la Mawaziri, kikao muhimu sana nah apo tukapitisha uamuzi wa kuingia vitani.

Msimamo wangu ulikuwa japo tumekasirishwa na kitendo cha Bahari Nyeusi, niliendelea kuamini kuwa tulipaswa kuingia vitani kuisaidia Ujerumani. Washirika wa upande wa pili hawakuweza kutupatia chochote zaidi ya kurudia ahadi, ambazo mara nyingi walizivunja, za kuendelea kutuhakikishia usalama wa maeneo yetu ambayo tunayo hadi kufikia kipindi hiki. Hivyo hapakuwa na faida yoyote ambayo tungeipata kama tungejiunga nao.

Zaidi, kama tungekataa kutoa msaada kwa ushirika wet una Wajerumaniwakati wakiwa wanatuhitaji, nao wangekataa kutusaidia sisi laity kama wangeshinda. Na kama tungebaki bila kufungamana na upande wowote, upande wowote ambao ungeshinda, ungeipa Uturuki adhabu kwa kutoshirikiana nayo, na ungetekeleza mahitaji yao ya ardhi kwa kutunyang’anya sisi ardhi na maeneo yetu.

Nikiwa kama kiongozi wan chi yangu, hakika siwezi kuruhusu iwe kwenye hali mbaya isiyokuwa na matumaini kama hiyo. Hivyo basi, nikachagua kuingia vitani kwa upande wa Wajerumani. Kipindi tulipoingia vitani kilikuwa hakima umuhimu wa juu, japo kama ingewezekana, ningependelea kuingia kwenye kipindi kingine ambacho kingekuwa na uzito zaidi kuliko huo uliojitokeza.

Wakati wa majadiliano yetu ndani ya Baraza la Mawaziri, tulileteWa taarifa za mkusanyiko mkubwa wa majeshi ya Urusi kwenye mpaka wetu na maeneo ya Kaukasiani. Chuki baina ya majeshi huko tayari zilikuwa za hali ya juu kabisa. Hivyo nikashauri kuwa sakata na shambulizi la Bahari Nyeusi lilikuwa letu, na limefanywa na majeshi yetu, na kujenga picha nzuri kwa kadiri ilivyowezekana na kutoa tamko la vita dhidi ya ushirika wa Waingereza na Wafaransa.

Wengi kati ya Mawaziri wa Baraza langu waliniunga mkono, na masharti yaliyotolewa na Waingereza na Wafaransa yalikataliwa. Uturuki ikajiunga rasmi kwenye vita kwa upande wa Watutoni.”

Imechapishwa Mwezi wa Kumi (1921) kwenye toleo la New York Times, Historia ya Sasa.

# *Kiambatanisho na. 2*

## *Fatwa ya wa-Ottomani ya Jihad Iliyotolewa na Essad Effendi, Sheikh-Ul-Islam wa Taifa la wa-Ottomani, Mwezi wa Kumi na Moja 1914*

## *Fatwa*

Ikiwa maadui kadhaa wakijiunga ili kuupinga Uislamu, ikiwa nchi za Kiislamu zitafukuzwa, ikiwa maelfu ya Waislamu watauawa au kutekwa na ikiwa kwenye mazingira hayo Padishah akiendana na maneno matakatifu yaliyomo kwenye Qur'ani akatanganza *Jihad*, je, kuingia kwenye vita hii ni wajibu kwa Waislamu wote, vijana na wazee, wapanda farasi na waendao kwa miguu? Je, Waislamu wan chi zote waharakishe kujiunga kwa kutumia rasilimali zao na miili yao kuelekeza kwenye *Jihad?*

Jibu: "Ndiyo."

Waislamu wanaoishi Urusi, Ufaransa na Uingereza nan chi zote ambazo zinazoshirikiana na hizo katika mashambulizi yao ya ardhini, baharini na angani dhidi ya *Khilafah* kwa lengo la kuuondoa na kuufuta Uislamu, je, nao pia, wanatakiwa washiriki kwenye *Jihad* dhidi ya serikali ambazo wao kama raia wanazitegemea?

Jibu: "Ndiyo."

Wale ambao, wakati Waislamu wote wanaitwa kujiunga na kupigania Jihad, watakataa kujiunga nayo, je, hao wanajifungua kupokea laana ya Allah, kupata majanga makubwa na adhabu wanayostahili?

Jibu: "Ndiyo."

Ikiwa Waislamu raia wa nchi zilizotajwa watachukua silaha na kupigana na serikali ya Kiislamu, je, watakuwa wanatenda dhambi isiyosameheka, hata ikiwa kama wamelazimishwa kwenda kwenye vita kwa vitisho kuwa wataangamizwa na kuuawa wao na familia zao wasipofanya hivyo?

Jibu: “Ndiyo”

Waislamu ambao kwenye vita hii wako chini ya tawala za Uingereza, Ufaransa, Urusi, Serbia, Montenegro na wale ambao wanazipa misaada nchi hizi kupigana vita dhidi ya Ujerumani na Austria, washirika wa Uturuki, je, wanastahili kuadhibiwa kwa laana ya Allah wakiwa kama chanzo cha ubaya na uharibifu wa Khilafah na Uislamu?

Jibu: “Ndiyo.”

Chanzo: Rekodi za Vita Kuu, Toleo III, ed. Charles F. Horne, National Alumni 1923.

# *Kiambatanisho na. 3*

## *Tamko la Sharif Hussein bin Ali kwa Dunia ya Waislamu Tarehe 27 Mwezi wa Sita, 1916*

[Kuambatana na tamko hili, alitangaza rasmi kujitoa kutoka kwenye kuutambua na kuutumikia utawala wa *Khilafah* wa-Ottomani ambaye alimteua yeye kuwa *Sharif* wa Makkah, hapo hapo kujipa uhuru kutokana na mamlaka hayo, hivyo basi kutayarisha mazingira ya yeye binafsi kujinyakulia mamlaka ya *Khilafah*. Kukosekana kwa mamlaka juu ya Makkah na ibada ya kila mwaka ya *Hajj* kuliupa utawala wa *Khilafah* wa Ottomani pigo la kisaikolojia na la kifo lililoondoa uhalali wa kuwapo kwake.

Jambo ambalo tamko hilo halikulifanya, na ambalo lilipaswa lifanye, lilikuwa ni kuupa taarifa *Ummah* wa Waislamu ujue kwamba yeye, Hussein bin Ali, alikuwa amekubali pendekezo la Balozi wa Uingereza aliyekuwa akiiwakilisha nchi yake Egypt, na kuwa amekubali kuwa mteja na mshirika wa Uingereza iliyo chini ya mamlaka ya ushirika wa Wayahudi-Wakristo kwa malipo ya paundi milioni 7 kutoka kwenye serikali ya Uingereza. Hiki kilikuwa kiwango cha pesa ambacho ushirika huo ulilazimika kumlipa ili awe mteja wao.

Wale wanaojiita Mujahiddin ambao wamepokea pesa na silaha kutoka kwa shirikisho la Wazayonisti la Kiyahudi-Kikristo la NATO, ikiwemo misaada ya kimkakati ya ndege za kivita, ili kuupindua na kuuangusha utawala na serikali ya Libya, na ambao wanajaribu kurudia usaliti kama huo nchini Syria, ni watu ambao wanafuata nyayo dhalili za Hussain bin Ali.]

## *Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehma, Mwenye Kurehemu*

Hili ni tamko letu la ujumla kwa ndugu zetu wote wa Kiislamu

قَدِ ٱفْتَرَيْنَا عَلَى ٱللَّهِ كَذِبًا إِنْ عُدْنَا فِى مِلَّتِكُم بَعْدَ إِذْ نَجَّىٰنَا ٱللَّهُ مِنْهَا ۚ
وَمَا يَكُونُ لَنَآ أَن نَّعُودَ فِيهَآ إِلَّآ أَن يَشَآءَ ٱللَّهُ رَبُّنَا ۚ وَسِعَ رَبُّنَا كُلَّ شَىْءٍ
عِلْمًا ۚ عَلَى ٱللَّهِ تَوَكَّلْنَا ۚ رَبَّنَا ٱفْتَحْ بَيْنَنَا وَبَيْنَ قَوْمِنَا بِٱلْحَقِّ وَأَنتَ خَيْرُ
ٱلْفَٰتِحِينَ ﴿٨٩﴾

"…Ewe Mola Mlezi wetu! Tuhukumie baina yetu na kaumu yetu kwa haki, nawe ndiye mbora wa wanao hukumu."

(Qur'ani, al-Araf, 7:89)

Miongoni mwa Watawala na Maamiri, Amiri wa Makkah al-Mukarramah walikuwa wa kwanza kuitambua Serikali ya Uturuki.

Walifanya hivi ili kujenga umoja wa mtazamo wa Waislamu na kujenga jamii zao ziwe imara, wakijua kuwa Masultani shupavu wa Ottomani (Allah awape radhi zake) walikuwa wakitenda kwa mujibu wa miongozo ya Qur'ani, Kitabu cha Allah, na Sunnah za Mtume Muhammad (rehma na amani juu yake), walijikita kwa nguvu zote kwenye utekelezaji wake, huku wakibaki kuwa wafuasi kamilifu wa miongozo yote hii miwili.

Nikitilia mkazo hayo niliyoyataja hapo juu, hao Maamiri niliowataja walifuata hiyo miongozo kikamilifu bila kukosa. Mimi binafsi, nikiwa nalinda heshima ya Taifa, niliwahamasisha Waarabu wasimame na kuwapinga Waarabu wenzao mwaka 1327 (ukiwa ni mwaka 1909 kwa kalenda ya Kikristo) katika kuuzunguka mji wa Abha, na mwaka uliofuata, palitokea msukumo kama huo ambao ulifanyika chini ya mmoja wa wanangu.

Maamiri waliendelea kuliunga mkono Taifa la Ottomani hadi pale ambapo (wazalendo wa Kituruki) Umoja wa Jamii na Maendeleo ulipojitokeza na kujinyakulia madaraka kamili ya uongozi wa mambo yote yanayohusu utawala.

Matokeo ya utawala huu mpya ni kuwa Taifa lilipoteza maeneo yaliyokuwa chini ya mamlaka yake, hilo likasababisha kupungua kwa nguvu na uhalali wake na kukabiliwa na hali mbaya ya udhoofu iliyosababishwa na vita vilivyoibuka.

Hali hiyo ilipelekea watekeleze mpango wa kimkakati ambao mapungufu haya yalitoa mwanya wa kuutumia. Inatosha kusema kuwa hii ilipelekea Ufalme wa Kiislamu kukutwa na simanzi kubwa (katika zama hizi zinazoendeshwa na vita) kwa hatma za wakazi wake – Waislamu na wasiokuwa Waislamu – kwa kupoteza aidha mali zao au maisha yao kwa kunyongwa, kufukuzwa na kukimbilia uhamishoni, au kulazimika kuuza sehemu ya nyumba zao ili kuweza kupata pesa za kujikimu.

Ingeonekana kuwa matukio haya hayakutosheleza matakwa na mipangilio ya (wazalendo wa Kituruki wenye sera za kidunia) wa Umoja wa Jamii na Maendeleo.

Utawala mpya uliendelea kuvunja kiungo baina ya Ufalme wa Ottomani na jumuiya yote ya Waislamu, ikiwa ni, kuvunja kuwapo kwa kushikamana kwa jamii hiyo na Qur'ani na Sunnah.

Chini ya amri ya mtawala wa Ufalme wa Ottomani, kwa jina *Wazir* Mkuu, *Ulamaa* wote, mawaziri na masharifu, moja ya magazeti ya Konstantinopol – al-Ijtihad – lilichapisha makala likishutumu maisha ya Mtume Muhammad (rehma na amani juu yake). Likaendelea kuhusisha mabadiliko kwenye Qur'ani – neno la Mungu – hususan, kuhusiana na Sheria ya Urithi kwa kuwapa wanawake sehemu sawa sawa na wanaume kinyume na matakwa ya Qur'ani kuwa wanaume warithi sehemu mbili zaidi kuliko wanawake, na pia kutamka kuwa wakati wa mwezi wa Ramadhani wanajeshi ambao watakuwa vituoni Madina, Makkah na Damaskas wanaweza kuahirisha funga zao za Ramadhani kama vile jinsi ambavyo majeshi yaliyokuwa mstari wa mbele yakipigana vita mpakani na Urusi, hivyo basi kupoteza mwelekeo na amri ya amri ya Qur'ani – "kwa wale miongoni mwenu ambao watakuwa wagonjwa au wamo safarini."

Pamoja na kumnyang'anya Sultani haki za kuhukumu na haki ya kuchagua na kuteua Baraza la Mawaziri wa Ufalme, na muhimu zaidi kwa upande wa dini ya Kiislamu, kwa kuvunja katiba ya Khilafah, tuliyakubali mambo yote haya ya kibunifu ili tu tusije kufarikiana na kutengana baina yetu.

Hata hivyo, pazia lilivuliwa pale ambapo ilionekana wazi kuwa Ufalme umo mikononi mwa Enver Pasha, Djemal Pasha na Talaat Bey, ambao walikuwa wakiuendesha kwa mujibu wa matakwa yao.

Ushahidi wa nguvu kabisa na usiokuwa na shaka ulipatikana pale ambapo uamuzi ulipelekwa kwa *Qadhi* wa Korti ya Makkah, ambao ulimtaka kutoa hukumu kwa misingi ya Ushahidi ambao utakuwa umepatikana na kuandikwa mbele ya mahakama yake pekee, na kumlazimisha kutotilia maanani kabisa Ushahidi wowote utakokuwa umeandikwa na Waislamu wenyewe, hilo likiwa ni pingamizi na dharau ya aya iliyomo kwenye *Surah al-Baqarah.*

Ushahidi wa ziada unapatikana kwenye hukumu ambamo Waislamu 21 mashuhuri wa Kiarabu walihukumiwa kuuawa kwa kunyongwa, wakiwa ni baada ya wengine ambao

walipewa hukumu kama hiyo kabla ya hapo – Amiri Arif esh-Shihabi, Shefik Bey el-Moayyad, Shukri Bey elAsali, Abd el-Wahab, Taufk Bey el-Baset, Abd el-Hamis al Zahrawi na Abd el-Ghani el-Arisi.

Ukatili wa namna hiyo hauendani na sababu wala mantiki yoyote ya kimaadili. Kuwaua watu wenye thamani kubwa kwa jamii kama hao peke yake nit endo bayan a la kihalifu, ukiongezea ukweli kuwa walizisababishia familia zao kujikuta wanakabiliwa na hali ngumu sana kimaisha baada ya kuwapoteza wale waliokuwa chanzo cha kipato, hakuwezi kupata sababu zozote za utetezi.

Allah anasema kwenye Qur'ani: "Hakuna roho itakayobebeshwa mzigo usiokuwa wake." Hata kama tukiamua haya yote kuyaacha, tunawezaje kusamehe kwa wao kuwanyang'anya pesa na mali ya familia hizo baada ya kuwatia ukiwa wa kuwaondolea waume na wazazi wao?

Tendo baya kabisa kuliko yote na linalohitaji kulaaniwa kupita kiasi ni pale ambapo walipolichafua na kuliharibu kaburi la mja na mcha Mungu, Sherif Abd el-Qadri el-Jazairi el-Ilasani?

Haya yote yanatosheleza kuweka wazi ushahidi na mwenendo wa utawala huu, na tunaweza, kwa uchache, kuwaachia binaadamu kiujumla, na Waislamu hususan, kutoa maamuzi yao ni jinsi gani utawala huu upimwe.

Mifano hii pia inatoa ushahidi wa jinsi gani Waarabu walikuwa wakithaminiwa. Lakini Ushahidi wa ziada ulipatikana pale ambapo watu walijitokeza kuupinga na kudai uhuru wao (kutoka kwenye utawala wa Kituruki) na kushuhudia ukosefu wa adabu na heshima dhidi ya dini yao pale ambapo bunduki zilipiga risasi *Ka'aba* – Hekalu la Umoja wa Kiroho na *Qiblah* kwa *Ummah* wa Kiislamu, ambayo inasemwa, kwa maneno ya Allah, "Safisheni Nyumba Yangu kwa ajili ya wale watakaopita kuizunguka." Moja ya risasi zilizopigwa ilipiga eneo ambalo liko takriban yadi moja na nusu tu juu ya Jiwe Jeusi, na nyingine, yadi tatu pembeni yake. Kitambaa kinachofunika Ka'aba kilishika moto. Maelfu ya Waislamu walijitokeza na kupiga makelele ya kushitushwa na khofu wakielekea hapo kuzima moto huo. Walilazimika kufungua mlango wa Ka'aba na kuelekea juu kwenye dari. Adui alipiga mzinga wa tatu kuelekea Makam Ibrahim. Huku watu kati ya watatu au wanne wakiuawa kila siku ndani ya Ka'aba, hali hii ilisababisha ugumu wa hali ya juu kuweza kulifikia jingo hilo takatifu.

Tunaiachia jamii yote ya Waislamu wa dunia nzima, kuanzia Mashariki hadi Magharibi, watoe uamuzi wao kuhusu jambo hili la dharau, utovu wa nidhamu na kuikosea heshima Nyumba Takatifu. Lakini tunashikilia msimamo wetu bila kutetereka wa kutowacha haki zetu za kidini na kitaifa kuwa jambo la kuchezea mikononi mwa wazalendo wa Kituruki wenye sera za kidunia wa chama cha Umoja na Maendeleo.

Allah Mtukufu, ameahidi kuilinda ardhi hii kupitia kupinga ugandamizaji na hatimaye kupatikana kwa ushindi na maisha bora bila kujali kuathiriwa na utawala mbovu wa Kituruki na maafisa wao wa kijeshi.

Ardhi hii inajitofautisha kabisa ikilinganishwa na nchi ambazo zinagugumia chini ya utawala wa mabavu wa serikali ya chama cha Umoja na Maendeleo. Iko huru, katika kila maana ya neno hilo, ikiwa imekombolewa kutokana na utawala wa kigeni, na kusafishwa na kila aina ya athari zao. Misingi yake ni kutetea imani ya dini ya Kiislamu, kuwainua na kuwaenzi Waislamu, kujenga mwenendo wao kwa misingi ya Sharia, kuunda misingi ya haki kwa msimamo huo huo ukiendana na misingi ya dini, kutekeleza maadhimisho yake yakiendana na maendeleo ya kisasa na kutekeleza mapinduzi halisi kwa kuhakikisha kuwa hakuna kipingamizi kwenye kuwapatia elimu waumini wa ngazi zote.

Hii ndiyo misingi tuliyoichagua kuitekeleza ili kutimiza majukumu yetu ya kidini, tukiamini kuwa ndugu zetu wote wa Kiislamu wa Mashariki na Magharibi watafuata na kutimiza majukumu yao kwetu, ili pamoja tuweze kujenga na kuimarisha uhusiano na undugu wetu katika imani.

Tunainua mikono yetu juu kwa unyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu, kwa niaba ya Mtume wa Mfalme Mwenye Wingi wa Kila Kitu, ili atujaalie ushindi na mwongozo kwenye yote mazuri na yenye manufaa kwa Uislamu na Waislamu. Tunamtegemea Allah, ambaye Anajitosheleza kwa mahitaji yet una Mbora kuliko wote kwenye Kulinda.

Sharif na Amir wa Makkah, El Hussein Ibn Ali
25 Sha'ban 1334, (June 27, 1916).

Chanzo: Rekodi za Vita Kuu, Toleo IV, ed. Charles F. Horne,
Alumni ya Taifa 192.3

# *Faharisi*

# Faharisi

A

Abd al-Aziz ibn Saud
Abd al-Aziz al-Effendi
Abd al-Aziz Ibn Saud
Abd al-Rahman Azzam,
Abd el-Ghani el-Arisi
Abd el-Hamid al-Zahrawi
Abdd el-Wahab
Abdul Hamid
Abdul Majid
Abdul Majid
Abdullah Yusuf Ali
Abha
Abraham / Ibrahimu
Abu Bakr al-Siddiq
Al-Azhar
al-Baqarah
al-Din
al-Duniya
Ali-Imran
Aliimiyah Kitivo cha Masomo ya Kiislamu
Algeria
Al-Ghazzali
Al-Hajj
Ali Mustafa
Aligarh Chuo Kikuu cha Kiislamu
altabah Pasha
al-Jizyah
al-Kahf
Allah
Amin al-Hussaini
Allenby
Angora
Ankara
Anti-Christ
Aqaba
Aqsa Kongamano la Kiislamu
Arabia
Ardhi Takatifu
Arifah
Asad Muhammad
Abu Said al-Khudri
Abul Ala Maududi
Adam
Adi bin Hatim
Afghan
Afghanistani
Ahadith
Ahl al-Dhimmah
Ahl al-Halli wal-Aqd
Ahl al-Kitab
Akhir al-Zaman
al-Araf
al-Akbar
al-Aqsa
al-Balad
al-Maidah
al-Malik
al-Mawardi
al-Mu'tamar al-Islami al-Am
al-Mukarramah
al-Nahda
al-Nisa
al-Qiyamah
al-Rum
al-Sayyed Idris al-Sanusi
al-Isra
al-Zawahiri
al-Zukhruf
Amerika
Amiri
Amir al-Mu'minin
Austria
Ansari
Ayatullah
Azhar
Ghuba ya Arabia
Arnold, T.
Astrakan

B

Baghdad
Balfour
Bangladeshi
Barka
Bashir Ahmad Kino
Barka
Bey, Rustim,
Bey, Rustom
Bai'ah
Balfour (Tamko la)
Banu Hashim
Basel
Berlin
Bashir Ahmad Kino
Bid'ah
Bahari Nyeusi

Bratianu
Bunge
Byzantium
Bulgaria
Bunge Kuu la Taifa

C

Chama
Chama cha Wafd
Chama cha Jamii na Maendeleo
Charles F. Horne
Chechenia
China
Chuo Kikuu cha Hebrania (Hebrew)
Chuo Kikuu cha Kiislamu
Cyprus

D
Dajjal
Damaskas
Dar al-Harb
Dar al-Islam
David
Demokrasia
Dhikr
Dinari
Diplomasia ya Ufaransa
Diplomasia ya Uingereza
Djemal Pasha
Dr Muhammad Iqbal
Dr Abul Fadl Mohsin Ebrahim
Dr Waffie Muhammad
Dunia
Dinari ya dhahabu
Dini
Dini ya Kiislamu
Dini ya Kikristo

E
Edib Saroit
Egypt
Elie Kedourie
Elimu
Emir Arif esh-Shilabi
Emir Omar el-Jazairi
Enver Pasha
Eskatolojia ya Kiislamu
Essad Effendi

F
Fakhri Pasha
Faruqi, Kamal
Fatwa
Fikr
Fir'auni
Fitan
Fuad

Fujo

G
Gayana
Geneva
Ghuba
Gibb, H.A.R.

H
Hadith
Hadith al-Qudsi
Hague
Hajj
Halal
Halil Bey
Hamburg
Hanafi
Hanbali
Haqiqah
Haram
Haram al-Sharif
Haramain
Haribu
Hassan al-Banna
Hajj Amin
Hejaz
Herzl
Hijri
Historia
Holt Rinehart
Hud
Hukumah
Hussain bin Ali

I
Ibn Khaldun
Ibn Saud
Ibn Taimiyyah
Ihsan
Ijma'a
Ijtihad
Imam
Imam al-Mahdi
Iman
Imran N. Hosein
Indonesia
Injili
Iqbal
Iran
Iraq
Ismail
Isra na Miraj

J
Jacob de Haan
Jahiliyah
Jama'ah
Jama'at-e-Islam
James Robson
Jamii ya Waislamu
Jamii isiyomtambua Mungu
Java
Jaziratul Arab
Jamii ya Kiyahudi
Jaji
Jihad
Jordan

Jeddah
Jenerali Allenby
Jeshi la Egypt

K
Kairo
Khilafah
Khalifah
Kamati ya Umoja na Maendeleo ya Freemason
Katiba
Kifo
Kongamano
Kongamano la Jerusalem
Kongamano la Kiislamu la Kairo
Konstantinopol
Krimea
Krusedi
Kupiga marufuku
Ka’aba
Kafir
Karachi
Karbala
Kashmir
Kazan
Khulafa al-Rashidun
Kufa
Kuffar
Kufr

L
Laana ya Mwenyezi Mungu
Laana ya Kiroho
Lailatul M’iraj
London
Loret
Los Angeles

M
Madina
Majadiliano
Ma’juj
Majenerali
Makubaliano ya Lausanne
Mamluke Khedive
Makkah
Makazi ya Wayahudi Palestina
Mapinduzi ya Kifaransa
Marhoom Mohammad
Marhoom Syed Ahmed
Marhooma Syeda Khatoon
Masjid al-Haram
Mazungumzo
Mehmet Talaat Pasha
Mfumo
Mfumo wa uchaguzi
Mkutano Mkuu wa Khilafah ya Kiislamu
Mkutano Mkuu wa Kiislamu wa Jerusalem
Moto
Moyo
Mossad, Shirika la Kijasusi la Israeli
Mufti Mkuu
Mungu
Mwenendo wa Taifa
Mwisho wa dunia
Ma’an
Maghrib
Magog
Makam Ibrahim
Minhaj
Miji ya Hejaz
Mji Mtakatifu
Moto wa Jehannamu
Marmorstein, Emile
Maryam
Masjid al-Aqsa
Masjid
Mtume wa Allah
Mfumo wa Jumuiya ya Kiislamu
Monowara Begum
Montenegro
Morocco
Muhammad Abduh
Muhammad Abdul Aliim Siddiqui
Muhammad Abdul Wahab
Muhammad al-Ahmadi al-zawahiri
Muhammad Ali jauhar

Mwisho wa historia
Mwongozo
Muhammad saffie
Mushriqun
Muhammad Ali Khan
Muhammad Fadlur Rahmani Ansari
Mujahidin
Mustafa Kamal

N
Nabii Muhammad
Najd
NATO
Nguzo tano
Nielsen, A.
Nigeria
Nur
nurullah

O
Ottomani
Ottomani, jeshi la,
Ottomani, utawala wa
Ottomani, ufalme

P
Padishah
Pakistani
Palestina
Papa
Pepo
Peponi
Poland
Porte

Q
Qadhi Mkuu
Qawanin Majmuasi
Qibla
Qur’ani
Qur’ani (hukumu ya)
Quraish

R
Rabbai
Radoslav
Ramadhan
Raouf Zaman
Rashid Rida
Rashidun Khilafah
Reazuddin Fakhruddin
Riba
Riyadh
Rum

Rumania

S
Sad Zaghlul
Sahih Bukhari
Saladin
Salahuddin Ayyubi
Salafi
Samehe
Sanusi
Sardar Iqbal Ali Shah
Saudia
Saudi Wahhabi
Sayyed Amin al-Husseini
Sayyed Muhammad Kifayatullah
Serikali
Serikali ya Libya
Sekretarieti ya Jerusalem
Shaikh Mkuu

Shaukat Ali
Shariah
Sheria ya Kiislamu
Sultani wa Ottomani
Sharif Hussein bin Ali
Sofia
Solomon
Souchon
Shoaib Quraishi
Shu’ba
Shukri Bey el-Asali
Shurah
Siberia
Sudan
Sufi
Sultani
Sunan Tirmidhi
Sunnah
Sunni
Syria

T
Tabligh Jamaat
Taif
Taifa la Wayahudi-Wazungu
Taifa la Ottomani (Waottomani)
Tamko
Tamko la Balfour
Thalibi Effendi
Thebes
Theodor Herzl
Tariqah
Tasawwuf
Taufk Bey el-baset
Tawaf
Teutoni
Tobago
Torah
Toynbee
Transjordan
Tripoli
Trinidad
Tunisia

U
Uchaguzi
Uchaguzi wa kisiasa
Uchumi
Uchunguzi wa Kieskatolojia
Ufaransa
Uharibifu
Uhuru
Uislamu
Ujerumani
Ukristo
Ukristo wa Ulaya
Undugu wa Waislamu
Uhuru wa Saudia
Ulama Ahl al-Hadith
Umar
Umar al-Faruq
Ummah
Umrah
Uongozi
Uongozi wa Waturuki
Uongozi wa Saudia
Uongozi wa Uingereza

Ukuta wa Kilio / Maombolezo
Ulama
Ulama wa Saudia

Ulaya
Urafiki
Uraia
Urusi
Uraia wa Saudia
Ushirika
Usuluhisho wa migogoro
Utamaduni wa Kiislamu
Utamaduni wa Kizungu
Utamaduni usiomtambua Mungu
Umoja
Uongozi wa Marekani
Ushirika wa Wazayonisti wa Kiingereza na Ufaransa

V
Vijana wa Kituruki (wa Mustafa Kamal)
Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia
Vita Kuu ya Pili ya Dunia
Viza
Viza ya Saudia

W
Wahhabi wa Saudia
Wajumbe
Wajumbe wa Egypy
Wajumbe wa Hejaz
Wakala wa Kiyahudi
Wakristo
Wanazuoni
Waturuki wa ki-Ottomani
Wayahudi
Wazayonisti
Wazayonisti wa Kikristo-Kiyahudi
Wazir Mkuu

X

Y
Ya'juj
Yanbu
Yaziid
Yemen
Yesu

Z
Zawahiri